# UHAKIKI WA SITIARI NA TASFIDA KATIKA MAWASILIANO KUHUSU VVU/UKIMWI MIONGONI MWA WANAFUNZI WA VYUO VIKUU: KIFANI CHA CHUO KIKUU CHA MOI

**NA**

**LILIAN MOMANYI**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA MOI**

**2021**

# IKIRARI

**Ikirari la Mtahiniwa**

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada yoyote.

Sahihi:______________________________ Tarehe:_____________________

**Momanyi Lilian**

**SASS/PGK/11/09**

**Ikirari la Wasimamizi**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini ya wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi:______________________________ Tarehe:_____________________

**Prof. Nathan Ogechi**

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu Cha Moi

Sahihi:______________________________ Tarehe:_____________________

**Dkt. Mosol Kandagor**

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu Cha Moi.

## TABARUKU

Kwa familia yangu, wanangu Jesse Osongo na Mary Tessy Mwango na wote wenye shauku ya kuelewa sitiari na tasfida katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI.

Kwa marehemu babangu mpendwa John Maswari Oseko Momanyi na mamangu Wilter Kwamboka Maswari kwa kunitia moyo kila siku.

# SHUKURANI

Shukrani! Ninasema. Umbali huu Mola ndiye aliyeniongoza, kuniangazia, kunifunulia na kunipa siha njema mpaka sasa. Bila uwezo wa Maulana singeweza. Shukrani, utukufu na heshima ni zake. Katika harakati zangu za kuishughulikia kazi hii, wengi wamenifaa sana kwa njia tofauti tofauti, nawashukuru.

Hii kazi ingeniwia nzito nisiweze kuinua kufikia upeo huu. Shukrani tele! Nawavulia kofia na kuwapigia saluti wasimamizi wangu Prof. Nathan Oyori Ogechi na Dkt. Mosol Kandagor kwa uongozi wenu tangu mwanzo hadi tamati ya tasnifu hii. Uvumilivu wao, uelekezi na uongozi wao ulinifungua macho kuifanya tafiti yangu kwa njia ya kipekee. Shukrani tele kwa wahadhiri wengine walioniandaa kufikia kuikabili kazi hii ya kitaaluma namna hii. Wahadhiri, Marehemu Prof. Naomi Shitemi, Dkt. Mwamzandi Issa, Dkt. Noordin, Dkt. Robert, Dkt. Opijah, Dkt. Obuchi, Dkt. Samuel Obuchi, Bw. Munyua na marehemu Bw. Mukuria.

Wazazi wangu: Marehemu babangu mpendwa Maswari Oseko Momanyi na Wilter Kwamboka Maswari kwa kunitia moyo mambo yaliponiwia mazito, kunishauri na kunipa msaada wa hali na mali. Watoto wangu Jesse na Mary asante kwa uvumilivu wenu. Isitoshe, shukrani sufufu kwa ndugu zangu: Evans, Hindra na Geoffrey. Shukrani maalum ziwaendee familia ya Bw. na Bi. Okal Bukachi na watoto wao na Bw. na Bi. Albert Keere mlinifaa kuliko ndugu. Mbarikiwe sana.

Shukrani tele ziwaendee wazamili wenzangu Dkt. Toboso, Bw. Makori, Bw. Barasa na wengine ambao kwangu walinifaa kupita kiasi. Mlikuwa msaada kwangu. Urafiki, upendo, uchangamfu na undugu wenu uliniwezesha kufaulu na kuibuka salama. Mola awajazie neema tele. Heko! Heko! Asanteni.

# IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza sitiari na tasfida katika mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu kwa kujikita kwa wanafunzi wa chuo kikuu cha Moi nchini Kenya. Tangu kisa cha kwanza cha Virusi Vinavyosababisha UKIMWI kugunduliwa nchini Kenya 1984, suala la UKIMWI limejitokeza kuwa mada muhimu ya utafiti katika taaluma mbalimbali. Hata hivyo, tafiti zinazohusu tasfida na sitiari zinavyojitokeza katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI. Hata hivyo, hakujatokea utafiti makinifu katika tafiti za Kiswahili kuhusiana na matumizi haya ya stiari na tasfida.. Mawasiliano ni hatua muhimu katika mazungumzo yanayohusu VVU/UKIMWI na masuala husika. Hivyo basi, ili kufanikisha mawasiliano, ni muhimu kushughulikia vipengele vinavyotumiwa katika mawasiliano kwa lengo la kutathmini kama vinafanikisha mawasiliano au vinachangia katika kushutumu waathiriwa zaidi. Hili ndilo pengo ambalo utafiti huu ulilenga kuziba. Malengo yaliyoongoza utafiti huu ni pamoja na: kutambua sitiari zilizotumiwa katika mawasiliano yanayohusu VVU/UKIMWI na masuala husika, kubainisha tasfida zilizotumiwa katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika; na jukumu lililotekelezwa na sitiara na tasfida za Kiswahili kama njia ya mawasiliano na kampeni dhidi ya VVU/UKIMWI. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Umaanisho ya Grice na vilevile nadharia ya Mawasiliano ya Kiutambulisho ya Giles. Msingi wa nadharia ya Giles unaipalilia kauli kwamba watu hufanya marekebisho katika mitindo yao ya usemi kadri wanavyowasiliana na wenzao. Nadharia hii pia inaichukulia lugha kama tukio la utendaji wa kijamii. Nadharia ya Grice nayo inaeleza tofauti za kiutambuzi baina ya kile kinachosemwa moja kwa moja katika sentensi na kile ambacho kinadokezwa tu katika usemi wa maneno maalum. Kuambatana na malengo ya utafiti huu, Chuo Kikuu cha Moi kiliteuliwa kimakusudi kama eneo la utafiti. Uamuzi huu ulitokana na hoja kwamba eneo hili lina wingi wa data iliyotumiwa na kuchanganuliwa katika utafiti huu. Mtafiti alitumia uchunguzi kifani kama muundo wa utafiti ili kuruhusu uchunguzi wa kina zaidi. Uteuzi wa sampuli kiuelekezano na mbinu ya kimakusudi ya uteuzi wa sampuli zilitumiwa kuwateua wasailiwa kutoka kwa sampuli nzima kuambatana na malengo maalum ya utafiti huu. Waliolengwa katika utafiti huu walikuwa vijana ambao wamo kati ya umri wa miaka kumi na nane na miaka thelathini na nane. Utafiti ulitumia mwongozo wa kuendesha mahojiano na hojaji katika kukusanya data ya utafiti. Data iliyokusanywa ilijumuisha vipengele vya kileksia na kauli kamilifu kama zilivyotumiwa katika maingiliano yanayohusu VVU/UKIMWI. Data ilichanganuliwa kwa msingi wa nadharia ya Umaanisho ya Grice na nadharia ya Mawasiliano ya Kiutambuisho ya Giles. Matokeo ya utafiti yaliashiria kwamba wanafunzi wengi walitumia tasfida na kauli za kisitiari kuwasiliana masuala yanayohusu VVU/UKIMWI miongoni mwa vijana katika Chuo Kikuu cha Moi. Isitoshe, mahusiano ya kijamii miongoni mwa vijana yanatekeleza dhima muhimu kama mbinu ya mawasiliano katika jamii. Utafiti vilevile ulibainisha kwamba maana iliyokusudiwa katika kauli za kisitiari pakubwa hueleweka katika msingi wa uamali. Utafiti huu ulihitimisha kwamba wanafunzi wengi huwasilisha ujumbe waliokusudiwa kupitia kwa mbinu za tasfida na sitiari kuambatana na matarajio ya jamii kuhusu adabu katika matumizi ya lugha, ikiwemo kutumia maumbo ya lugha ambayo hayaudhi na yanayokuza maingiliano mazuri ya kimawasiliano miongoni mwa wanajamii. Matokeo ya utafiti huu yatakuwa muhimu kwa makundi kadhaa ikiwemo wanafunzi wa Kiswahili, Wanaisimujamii, Wachanganuzi wa Diskosi na semi, na watafiti wengine ambao wana ari ya kuchunguza matumizi ya lugha katika mazingira asilia. Utafiti huu ni mchango muhimu kwa kongoo iliyopo tayari kuhusu sitiari na tasfida katika isimu na katika fasihi. Utafiti unapendekeza kwamba tafiti za baadaye zinapaswa kupanua upeo wa uchunguzi kwa kuangazia fani zingine za fasihi na isimu. Aidha, tunapendekeza kwamba watafiti wa baadaye wachunguze mielekeo mingine ya kinadharia katika kuchunguza data pamoja na masuala yaliyoibuliwa.

## ABSTRACT

This study analysed the forms of metaphors and euphemism that are used in communicating HIV/AIDS themes among the youth in Universities: a case study of Moi University,Kenya. Since the discovery of HIV/AIDS in Kenya, a lot of metaphoric expressions and euphemisms have been coined and used in communicating HIV/AIDS themes. However, scholarly studies on metaphors and euphemism on HIV/AIDS have not featured prominently in Kiswahili scholarship. Communication is very important in the daily happenings of a human being especially on issues pertaining to HIV/AIDS and emerging issues. It is an integral tool through which a person is able to pass information to the intended recipient when communicating on HIV and AIDS and its related matters with an aim of passing a message. Thus, the aim of this research was to analyze how metaphors and euphemism statements effects communication on HIV/AIDS and its related matters. This study was guided by the following objectives: to identify metaphors used on HIV/AIDS communication and its related matters, identify euphemism used on HIV/AIDS communication and its related matters; and the role played by Kiswahili metaphors and euphemism as media of communication and campaign against HIV/AIDS. This study was guided by Grice's theory of Implictures as well as Giles' theory of Communication and Accomodation. The basis of Gile's theory lies in the idea that people adjust (or accommodate) their speech styles as they interact with each other. The theory also views language as a form of social practice. Grice's theory, attempts to clarify the intuitive difference between what is expressed literally in a sentence and what is merely suggested or hinted at by an utterance of the same string of words. In line with the objectives of this study, Moi University was chosen purposely as the study area. This is because the site is largely rich with the significant data which was used/analysed in this research. The researcher employed case study as the main research design to allow for a more focused investigation. Snowball and purposive sampling techniques were used to select the respondents from the sample frame, in tandem with the specific objectives of this study. The target population were the youth who fall in the age bracket of eighteen and thirty eight years. The study employed interview schedule, questionnaire techniques to collect data. The collected data comprised of purposefully selected lexical items and fairly complete utterances as used in the HIV/AIDS interactional encounters. Data was analysed based on the prisms of Grice's theory of Implictures and Giles' theory of Communication and Accomodation. The findings indicated that most students use euphemism and metaphorical statements to communicate HIV/AIDS concerns among the youth in Moi University. Further, the youth's social relations in the society play a major role as a medium of communication. Another finding of this study is that the intended meaning of metaphorical statements are largely understood pragmatically. This research concluded that most students communicate their intended messages through euphemism and metaphoric expressions in consonance with the society's expectations with regards to decency in language use, including embracing non-offensive language forms that enhance good communication mannerisms among members of the society. The findings of the research will be benefit a number of parties, including Kiswahili students, sociolinguistics, Discourse Analysts, and other resarchers who may be interested in language use in natural settings.This study is a significant contribution to the already existing literature on metaphors and euphemism in linguistics as well as in literary studies. The study recommends that future researchers consider widening the scope of the investigation by considering other areas as literature and linguistics. Further, we recommend that future researchers consider other theoretical orientations in explicating the data as well as the issues raised.

# YALIYOMO

IKIRARI ........................................................................................................ ii
TABARUKU .................................................................................................. iii
SHUKURANI ................................................................................................. iv
IKISIRI ............................................................................................................v
ABSTRACT.................................................................................................... vi
YALIYOMO.................................................................................................. vii
MAELEZO YA AKRONIMU......................................................................... xi
**SURA YA KWANZA ......................................................................................1**
**MISINGI YA UTAFITI .....................................................................................1**
1.0 Utangulizi......................................................................................................1
1.1 Usuli wa Utafiti..............................................................................................1
1.2 Suala la Utafiti ...............................................................................................4
1.3 Malengo ya Utafiti .........................................................................................5
1.4 Nadharia Tete.................................................................................................5
1.5 Umuhimu wa Utafiti ......................................................................................6
1.6 Sababu za Kuchagua Mada ............................................................................7
1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti.............................................................................8
1.8 Hitimisho........................................................................................................9
**SURA YA PILI..............................................................................................10**
**MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA............................10**
2.0 Utangulizi....................................................................................................10
2.1 Mapitio ya Maandishi ..................................................................................10
2.1.1 Historia fupi ya VVU/UKIMWI .................................................................10
2.1.2 Mawasiliano na VVU/UKIMWI..................................................................12
2.1.3 Tamathali za Usemi ...................................................................................13
2.2 Nadharia ya Utafiti.......................................................................................27
2.2.1 Nadharia ya Umaanisho ............................................................................27
2.2.2 Nadharia ya Mawasiliano ya Kiutambulisho .............................................31
2.2.2.1 Mawazo makuu katika Nadharia ya Utambulisho ..................................32
2.2.2.2 Dhana ya utambulisho.............................................................................33
2.3 Hitimisho......................................................................................................36

**SURA YA TATU ........................................................................................37**
**MBINU ZA UTAFITI ..................................................................................37**
3.0 Utangulizi ..................................................................................................37
3.1 Eneo la Utafiti ...........................................................................................37
3.2 Sampuli na Usampulishaji .........................................................................38
3.2.1 Usampulishaji wa kinasibu sahili ..........................................................38
3.2.2 Usampulishaji wa kimfuatano ................................................................38
3.2.3 Usampulishaji wa kimatilaba .................................................................38
3.3 Ukusanyaji wa Data ...................................................................................39
3.3.1 Mahojiano ...............................................................................................40
3.3.2 Utazamaji nyanjani .................................................................................40
3.3.3 Kundi Lengwa la Majadiliano ................................................................41
3.4 Vifaa vya Ukusanyaji Data ........................................................................42
3.4.1 Hojaji ......................................................................................................42
3.4.2 Kinasa sauti ............................................................................................42
3.5 Uchanganuzi wa Data ................................................................................42
3.6 Masuala ya Etikeli .....................................................................................44
3.7 Changamoto za Utafiti ...............................................................................44
3.8 Hitimisho ...................................................................................................45
**SURA YA NNE ........................................................................................46**
**MATUMIZI YA SITIARI KATIKA MAWASILIANO YA VVU/UKIMWI MIONGONI MWA WANAFUNZI WA CHUO KIKUU CHA MOI ..................46**
4.0 Utangulizi ..................................................................................................46
4.1 Dhana ya Sitiari .........................................................................................46
4.2 Matumizi ya Sitiari ya Ngono Miongoni mwa Wanafunzi .........................51
4.2.1 Msamiati wa kurejelea ngono .................................................................51
4.2.2 Msamiati wa kurejelea uuke ...................................................................57
4.2.3 Msamiati wa kurejelea uume ..................................................................61
4.2.4 Msamiati wa kurejelea VVU/UKIMWI ..................................................64
4.2.5 Msamiati wa kurejelea kondomu ............................................................66
4.2.6 Msamiati wa kurejelea mtu aliye na VVU/UKIMWI ..............................68
4.3 Hitimisho ...................................................................................................70

**SURA YA TANO ......................................................................................................71**
**TASFIDA KATIKA MAWASILIANO YA VVU/UKIMWI MIONGONI MWA WANAFUNZI ..........................................................................................................71**
5.0 Utangulizi.........................................................................................................71
5.1 Dhana ya Tasfida .............................................................................................71
5.2 Uainishaji wa Tasfida .......................................................................................75
5.2.1 Tasfida zinazowakilisha ngono.......................................................................75
5.2.2 Tasfida zinazohusikana sehemu za siri za mwanamke ...................................80
5.2.3 Tasfida zinazowakilisha sehemu za siri za wanaume (Uume).........................83
5.3 Tasfida za VVU/UKIMWI ...............................................................................85
5.4 Tasfida Zinazorejelea Kondomu.......................................................................88
5.5 Hitimisho..........................................................................................................92
**SURA YA SITA.......................................................................................................93**
**DHIMA YA SITIARI NA TASFIDA KATIKA MAWASILIANO YA VVU/UKIMWI MIONGONI MWA WANAFUNZI ............................................93**
6.0 Utangulizi.........................................................................................................93
6.1 Dhima ya Sitiari katika Mawasiliano ya VVU/UKIMWI ...................................93
6.1.1 Kufikirisha jamii ...........................................................................................94
6.1.2 Hukuza na kufunza maadili ...........................................................................94
6.1.3 Kuweka mipaka miongoni mwa wanajamii....................................................95
6.1.4 Kuendeleza utamaduni wa jamii ....................................................................96
6.1.5 Kitambulisho cha jamii ..................................................................................96
6.2 Dhima ya Tasfida katika Mawasiliano ya VVU/UKIMWI .................................97
6.2.1 Kupunguza kutoelewana................................................................................98
6.2.2 Kupunguza Makali.........................................................................................98
6.3 Hitimisho........................................................................................................100
**SURA YA SABA ....................................................................................................101**
**MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI ...........101**
7.0 Utangulizi.......................................................................................................101
7.1 Muhtasari wa Tasnifu .....................................................................................101
7.2 Mahitimisho ya Utafiti....................................................................................102
7.2.1 Matumizi ya sitiari katika kukuza mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika ................................................................................103

7.2.2 Nafasi ya tasfida katika kuendeleza mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi ..........103
7.2.3 Dhima ya sitiari na tasfida katika kukuza mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi ....104
7.3 Mchango wa Utafiti ..........105
7.4 Mapendekezo ya Utafiti ..........105
7.5 Hitimisho ..........106
MAREJELEO ..........107
VIAMBATISHO ..........113
Kiambatisho A: Kiambatisho cha mwongozo wa mahojiano na watafitiwa ..........113
Kiambatisho B: Baadhi ya Data ..........116

# MAELEZO YA AKRONIMU

| | |
|---|---|
| UKIMWI | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| UNAIDS | United Nations Programme on HIV/AIDS |
| VVU | Virusi vya UKIMWI |

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Katika sehemu hii tutashughulikia yafuatayo: misingi ya utafiti huu kwa kutoa taarifa za kiusuli kuhusiana na mada ya utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia tete ya utafiti, umuhimu wa utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti na hitimisho.

## 1.1 Usuli wa Utafiti

Tangu kisa cha kwanza cha virusi vinavyosababisha UKIMWI kugunduliwa nchini Kenya, swala la UKIMWI limejitokeza kuwa mada muhimu ya utafiti katika taaluma mbalimbali. Hata hivyo serikali imeweka mikakati anuwai ili kuangamiza janga hili la VVU/UKIMWI. UKIMWI (ukosefu wa kinga mwilini) ni hali au ugonjwa unaosababishwa na VVU (virusi vya UKIMWI). Ugonjwa huu uligunduliwa mnamo mwaka wa 1980 (UNAIDS, 2008) na iliaminika kwamba ugonjwa huu ulikuwa aina fulani ya saratani iliyosambaa miongoni mwa wanaume mashoga katika miji ya San Francisco, Los Angeles na New York nchini Marekani.

Watafiti walipoendelea kufanya utafiti zaidi juu ya ugonjwa huu, waligundua kwamba haukuwa ugonjwa wa mashoga wala saratani bali ni aina ya virusi vinavyosambazwa kupitia kwa damu na manii (Sontag, 1989). Ngono ikiwa mojawapo ya visababishi vya UKIMWI imechangia asilimia kubwa ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Hata hivyo kuna visababishi vingine kama ukeketaji wa wasichana na kutahiri kwa wavulana kwa kutumia kifaa kimoja; kutumia kwa pamoja vitu vinavyotoboa ngozi kama nyembe na sindano hivyo basi kusababisha kuchanganyika kwa damu; mila na desturi za jamii mbalimbali kama kurithi wajane

ambao labda wanaume wao waliaga dunia kutokana na hali hii; kuwa na wapenzi wa kando wengi bila kutumia kinga na kadhalika (UNAIDS, 2008). Hivyo basi tangu ugonjwa huu ugunduliwe, umekuwa chanzo kuu cha maafa katika mataifa mengi ya kusini mwa Afrika, taifa la Afrika Kusini likiwa na idadi kubwa zaidi ya maambukizi katika ulimwengu wote (Visser na wenzake, 2004).

Ripoti ya Kenya AIDS epidemic updates (2020), inaonyesha kwamba idadi ya watu wanaoambukizwa virusi vya UKIMWI inaendelea kuongezeka. Mkoa wa Nyanza unaongoza katika idadi ya maambukizi na maafa ya watu walioambukizwa. Kulingana na ripoti za Kenya AIDS epidemic, idadi ya maambukizi ni milioni moja na nusu.

Kulingana na ripoti ya UNAIDS (2020) idadi ya watu walioambukizwa na VVU nchini Kenya ni milioni 2.2, na watu milioni 1.5 tayari wamefariki. Kati ya idadi ya hawa waathirika, walioathirika zaidi ni wanawake na vijana kati ya umri wa miaka 14 – 24. Kulingana na taarifa hizi ni kwamba ugonjwa huu ni tatizo kubwa nchini Kenya, jambo ambalo limetatiza maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa hivyo, kuna haja ya kubadilisha tabia, imani na mitazamo ya binadamu kuhusu ngono iwapo tutafaulu katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI.

Lugha kama kifaa cha kupiga vita ugonjwa huu, ni kifaa ambacho hutumiwa kuwezesha watu kupata ufahamu juu ya ugonjwa wa UKIMWI. Hivyo basi, mawasiliano ni muhimu katika maisha ya binadamu katika kuangamiza UKIMWI nchini Kenya. Nchini Kenya mawasiliano hutekelezwa katika miktadha tofautitofauti ambayo huwa na mahitaji tofauti tofauti vilevile. Hivyo basi kuna miktadha ambayo huhitaji matumizi ya lugha fiche (sitiari) au tasfida, kwa sababu ya miiko za kijamii barani Afrika.

Sitiari na tasfida kama vipengele vya lugha ni mbinu ambazo hisia zinaweza kufinyanga bila kupoteza uwazi wa maana yake (Whalley, 1953). Matumizi ya sitiari na tasfida katika mawasiliano ya UKIMWI yana umuhimu kwa sababu hueleza mambo ambayo hayaelezeki kwa urahisi kwa kutumia lugha wazi kwa kina na uthabiti. Hata hivyo, vipengele hivi hutumiwa ili kutoa ufafanuzi wa maana bila kutumia maelezo mengi. Hutekeleza wajibu huu kwa kuleta pamoja miktadha inayotofautiana lakini yenye uhusiano ili kuwasilisha habari dokezi au lengwa.

Sitiari na tasfida kama vipengele vya lugha havijafanyiwa utafiti mwingi na wa kina katika muktadha wa mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI kati na baina ya wanafunzi wa vyuo, licha ya kuwa tangu ugonjwa huu ugunduliwe, jamii mbalimbali zimeibua sitiari na tasfida anuwai kuurejelea katika mawasiliano yao ya kila siku. Hivyo basi nimechanganua sitiari na tasfida zinazotumika katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika kama ngono, kondomu ya kuzuia maambukizi ya VVU, mwathiriwa na sehemu za siri za kike na kiume. Aidha, hakuna utafiti uliowahi kufanywa kuhusu sitiari na tasfida zinazotumiwa katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika katika Kiswahili, kati na baina ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi. Ni kutokana na hali hii ambapo utafiti huu umefanywa.

Nyandiba (2013), anadai kwamba mawasiliano ni muhimu katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI. Utafiti wake ulitambua athari ya uteuzi wa mikakati ya mawasiliano ya washauri na washauriwa katika vituo vya unasihi na upimaji wa hiari katika jamii ya Abagusii. Utafiti wa Nyandiba ulilenga kuchunguza jinsi imani na desturi za Abagusii kuhusu ngono huathiri uteuzi wa mikakati ya mawasiliano katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI.

Sontag (1989), hakulishughulikia suala la sitiari kwa kina. Hata hivyo, anadai kuwa sitiari zilizoibuliwa ni za kuwashutumu waathiriwa. Tofauti na utafiti huu ni kwamba sitiari na tasfida zinazotumiwa katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI hazishutumu tu, bali pia zina majukumu mengine kama, kurahisisha mawasiliano, kupamba lugha, kukuza maadili, na hivyo basi kuwezesha mawasiliano kutekelezwa juu ya VVU/UKIMWI miongoni mwa watu katika jamii bila kuvunja miiko iliyowekwa na tamaduni husika. Hili ndilo pengo ambalo utafiti huu ulilenga kuziba. Pengo ambalo lilikuwa kichocheo cha utafiti huu. Utafiti huu umebainisha na kuhakiki sitiari na tasfida zinazotumika katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI kati na baina ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi na kubainisha dhima ya vipelengele hivi katika jamii ya Afrika. Haya yalitekelezwa chini ya uongozi wa nadharia ya Umaanisho ya Grice (1978, 1975) na nadharia ya Mawasiliano ya Kiutambulisho ya Giles (1972 & 1982).

## 1.2 Suala la Utafiti

Kuna tafiti nyingi ambazo zimewahi kufanywa kuhusu suala la lugha na VVU/UKIMWI. Hata hivyo, kutokana na mapitio yetu ya maandishi mbalimbali, tunaweza kutoa kauli kwamba hakuna utafiti ambao umefanywa juu ya matumizi ya sitiari na tasfida hasa miongoni mwa wanafunzi. Katika utafiti huu, tumepania kuzifuatilia sitiari na tasfida ambazo hutumika kwa wingi katika maingiliano kati na baina ya wanafunzi wanapojishughulisha na mada mbalimbali kuhusu VVU/UKIMWI, ngono, sehemu za siri za mwanamke na mwanamume miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi.

Vipengele vinavyotumiwa katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI ni pamoja na sitiari na tasfida, kwa sababu barani Afrika ni mwiko kutamka masuala juu ya ngono na

VVU/UKIMWI hadharani. Hivyo basi, utafiti huu umepania kujibu maswali yafuatayo ya kimsingi: Je, sitiari na tasfida zinazotumiwa katika maingiliano kati na baina ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi ni zipi na zina athari gani katika kukuza na kuendeleza mada mbalimbali zinazohusu VVU/UKIMWI, ngono, uume, uuke miongoni mwa vipengele vingine? Je, ni sababu gani zinazopelekea uteuzi na matumizi ya sitiari na tasfida katika maingiliano hayo?

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo yafuatayo:

i) Kuzichanganua sitiari mbalimbali zinazotumiwa katika mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi kuhusu VVU/UKIMWI.

ii) Kujadili tasfida zinazotokea katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi.

iii) Kutathmini dhima ya sitiari na tasfida katika kukuza mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi kuhusu VVU/UKIMWI.

## 1.4 Nadharia Tete

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

i) Katika maingiliano kati na baina ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi tasfida na sitiari hutumika kwa wingi katika kukuza mtagusano, ukuruba na maingiliano baina yao kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika.

ii) Kutokana na maingiliano ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi, tasfida za ainaaina hutumiwa katika kupunguza makali, hasa wahusika wanapojadili mada nyeti.

iii) Tasfida na sitiari zimetumiwa kwa wingi katika kuendeleza na kukuza mawasiliano, ukuruba na mtagusano miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi.

**1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Tasnifu hii ni zao la utafiti uliofanywa kuhusu vipengele vinavyotumika katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI miongoni mwa vijana katika Chuo Kikuu cha Moi. Sitiari na tasfida kama vipengele vya lugha, vimeenea kimatumizi katika mazungumzo ya kawaida (Kiswahili) kuhusu VVU/UKIMWI. Licha ya kuenea huku ni watafiti wachache ambao wamevishughulikia vipengele hivi vya lugha katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo ni vipengele ambavyo huchukuliwa kuwa vya fasihi zaidi kuliko taaluma ya isimu. Hivyo basi utafiti huu ulichanganua matokeo ya data za sitiari na tasfida zinazotumiwa katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika katika Kiswahili. Tasnifu hii basi, ina umuhimu wa kutoa mchango wa kitaaluma kwa njia mbalimbali zifuatazo:

Kwanza, uchunguzi wa vipengele hivi vya lugha katika kitengo cha isimujamii ni jambo muhimu, hasa katika kuelewa matumizi ya lugha katika mada tofauti, umri mbalimbali na miktadha mbalimbali katika jamii. Hivyo basi, utafiti huu utawasaidia wanajamii kuelewa vipengele ambavyo ni sitiari na tasfida ambavyo hutumika katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika.

Pili, utafiti huu una umuhimu kwa taaluma ya isimujamii kwa kuwa unaelezea matumizi ya vipengele hivi vya lugha katika muktadha wa kijamii. Utafiti huu unaelezea uhusiano uliopo kati ya isimu na jamii, na hasa jinsi ambavyo wanajamii hutumia lugha katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika

Tatu, utafiti huu ni muhimu katika kuongeza idadi ya maandishi ya kitaaluma kuhusu mawasiliano ya VVU/UKIMWI. Mbali na kuongeza idadi ya maandishi, utafiti huu utawapa shauku watafiti wa baadaye wa Kiswahili watakaotaka kuchangia suala hili kwa kulifanyia utafiti mpana zaidi.

**1.6 Sababu za Kuchagua Mada**

Mada hii ya utafiti iliteuliwa kwa misingi kwamba, VVU/UKIMWI ni jambo ambalo linaathiri wanajamii kwa jumla, hivyo basi niliona si vyema jambo hili kushughulikiwa na wanasayansi tu bali linafaa pia kushughulikwa na wataalamu mbalimbali katika nyanja mbalimbali, wakiwemo wataalamu wa isimujamii.

Kwa vile lugha hutumika kuashiria mfumo wa jamii husika, inaashiria kwamba, kuna uhusiano mkubwa baina ya lugha na jamii ambamo lugha hiyo hutumika. (Harry, 1954). Franz (1978) anasema, lugha inayotumiwa na watu wote katika jamii ndiyo hasa hubeba utamaduni wa watu hao. Kulingana na Hymes (2000), utamaduni ni jumla ya matatizo, kaida, malengo na maadili yanayotambulisha asasi, shirika, au kundi fulani la watu.

Mamoridou (2000) naye anasema kwamba, lugha huchukuliwa kama mojawapo ya kipimo katika kufanikisha mawasiliano na katika hali hii mchakato wa habari ambao ndio mawasiliano hufanyika. Kulingana na misingi ya kazi hizi za Harry (1954), Franz (1978), Hymes (2000) na Marmoridou (2000), ni kweli kabisa kwamba tasfida na sitiari kama vipengele vya lugha katika jamii huundwa kutokana na utamaduni wa jamii husika. Hivyo basi, matumizi ya tasfida na sitiari katika lugha hutegemea jinsi utamaduni ulivyomuumba binadamu wa kike na wa kiume. Kwa hivyo, matumizi ya vipengele hivi katika miktadha mbalimbali ya mazungumzo ya vijana katika jamii yanategemea jinsi utamaduni umewaumba vijana hao. Ni kwa sababu hii basi,

vipengele hivi vilitafitiwa ili kuchunguza kama vina umuhimu katika kupiga vita maambukizi ya VVU/UKIMWI kupitia mawasiliano ya VVU/UKIMWI; lugha ikiwa kama njia moja ya kupunguza unyanyapaa na maambukizi ya janga hili kwa vile tiba ya UKIMWI bado haijapatikana.

Licha ya kuwepo kwa tafiti nyingi zinazoangazia VVU/UKIMWI, inabainika wazi kuwa hakuna utafiti wowote wa kina uliowahi kufanywa kulihusu swala la mawasiliano kisitiari na kitasfida hasa katika lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi kuhusu masuala nyeti.

**1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu umejadili sitiari na tasfida zinazotumika katika mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika kati na baina ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi. Kuna aina nyingi za sitiari na tasfida katika jamii lakini utafiti huu umejikita katika sitiari na tasfida zinazotumika katika muktadha wa mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika tu.

Utafiti huu umetathmini uhusiano uliopo kati ya kauli za sitiari na tasfida zilizokusanywa na dhana ambazo zinarejelewa katika lugha ya Kiswahili. Tumeshughulikia uhusiano uliopo kati ya vipengele hivyo ***(yaani maana asili na maana pokezi)*** na umuhimu pekee wala hatukuzungumzia suala lingine.

Sitiari na tasfida hizi zimekusanywa katika Chuo Kikuu Cha Moi, mjini Eldoret. Nilichagua Chuo hiki kwa sababu ya wingi wa wanafunzi. Wanafunzi ambao wamelengwa ni wa umri wa miaka 18-38. Utafiti huu umechunguza sitiari na tasfida zinazotumika katika mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika kati na baina ya makundi mbalimbali ya wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Moi yaliyoteuliwa. Utafiti huu ulihusu sitiari na tasfida ambazo hutumiwa katika

mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika tu kama ngono, sehemu za siri za kike na kiume, VVU/UKIMWI, kondomu na mwathiriwa. Kuna aina nyingi za sitiari na tasfida katika jamii lakini utafiti huu umejikita katika sitiari na tasfida zinazotumiwa katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika kama ngono miongoni mwa wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Moi katika mazungumzo teule.

**1.8 Hitimisho**

Sura hii ilishughulikia vipengele vya kiutangulizi kama vile utangulizi wa utafiti, usuli wa utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia tete, umuhimu wa utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti. Vipengele hivi ni vya muhimu sana kwa sababu vimeweka msingi kwa utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.0 Utangulizi

Sura hii imefafanua mapitio ya maandishi na kiunzi cha nadharia. Katika mapitio ya maandishi, historia fupi ya VVU/UKIMWI imejadiliwa kwani hiki ndicho kiini cha utafiti huu, pia vipengele vya lugha (tasfida na sitiari) katika mawasiliano mbalimbali vimeelezwa kutokana na maandishi ya awali. Nadharia zilizoongoza utafiti na viunzi vyake vimejadiliwa pia katika sehemu hii, kwa kuonyesha namna mihimili maalum ilivyotumiwa katika uchanganuzi wa data.

## 2.1 Mapitio ya Maandishi

Mapitio ya maandishi ni kile kitendo cha kusoma, kuchanganua na kuchunguza kwa urazini maandishi mbalimbali. Kazi za hapo awali za watafiti watangulizi hudurusiwa na mtafiti ili kupata uhusiano na mapengo yanayojitokeza na hatimaye kuyatafitia mapengo hayo kwa njia ya kiusomi na kamilifu (Boswell & Cannon, 2009).

Nilipitia maandishi anuwai, yaliyohusu historia ya VVU/UKIMWI, matumizi ya lugha na UKIMWI, kauli ibuka zilizotumika katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na sehemu za siri za binadamu, umuhimu wa kauli hizi katika mawasiliano ya kupiga vita hali hii, ili kupunguza maambukizi zaidi ya VVU/UKIMWI.

### 2.1.1 Historia fupi ya VVU/UKIMWI

Kulingana na UNAIDS (2008), mgonjwa wa kwanza mwenye dalili za VVU/UKIMWI alionekana Marekani mwanzoni mwa miaka ya 1980. Wanaume mashoga wa miji ya San Francisco na New York walianza kupatwa na maradhi adimu kuonekana pamoja na kansa ambayo ilikuwa kidonda ndugu. Punde ndipo palipogunduliwa kwamba ni VVU ambavyo vilithibitishwa kuwa ndivyo visababishi

vya ugonjwa wa UKIMWI. Virusi hivi vilibainika kuwa vinatoka kwenye kundi la virusi vya “lentivirus” ambavyo hushambulia na kuharibu kinga ya mwili wa kiumbe. Vilevile huweza kukaa kwa muda mrefu ndani ya mwili wa kiumbe pasipo kuonyesha dalili. Inaaminika kuwa VVU/UKIMWI vilitokana na binadamu kushiriki ngono na nyani. Mtu anapoambukizwa VVU, virusi hivyo hukaa kwenye chembechembe nyeupe za damu zinazoleta kinga ya mwili. Chembechembe hizo huitwa CD4. Virusi hivi hushambulia na kuua chembechembe za CD4 na kusababisha kupungua kwa kinga ya mwili na hivyo kusababisha maambukizi ya magonjwa mwilini kwa njia rahisi na hivyo kusababisha hali ya UKIMWI. Mtu mwenye afya njema huwa na chembechembe za CD4 kati ya 500 na 1500 katika mililita moja ya damu. Ugonjwa wa UKIMWI unaanza kujitokeza pale ambapo chembechembe hizo hupungua na kufikia chini ya 200.

Sontag (1989) anadai kwamba katika miaka ya awali, maradhi ya UKIMWI yalilinganishwa na saratani. Maradhi hayo wakati huo yalikuwa ya kutisha kiasi kwamba waliofariki kutokana na hali hii hawakutangazwa hadharani. Yalionekana kama maradhi ya laana, aibu na adhabu. Baada ya maradhi ya VVU/UKIMWI kugunduliwa, yalichukua nafasi ya saratani katika kutisha na kuogofya. Waliogua maradhi haya walikumbwa na hukumu mbaya zaidi na unyanyapaa ambao wagonjwa wa saratani walikumbana nao.

Mbali na saratani, maradhi ya UKIMWI pia yalilinganishwa na maradhi ya kaswende. Iliaminika kwamba maradhi ya UKIMWI na kaswende yalikuwa na mshabaha mmoja katika hali ya uambukizaji na hatua ambazo mgonjwa alipitia kabla ya kifo chake (Sontag, 1989). Jinsi ilivyo katika maradhi ya kaswende, maradhi ya UKIMWI huwa ya kutisha zaidi katika hatua zake za mwisho kabla ya mgonjwa kufariki.

Sitiari ambazo Sontag (1989), aliziibua kuhusiana na UKIMWI na masuala yake ni pamoja na uvamizi (anadai kuwa ugonjwa huu unavamia na kwa hivyo unafaa kuvamiwa pia), uchafuzi, vita (kumaanisha ugonjwa huu unafaa kupigwa vita) na tauni (analinganisha UKIMWI na tauni).

Kulingana na Sontag (1989), sitiari hizi zilizoibuliwa zilikuwa za kuwashutumu na kuwashtua wanajamii ndio wajiepushe na ngono za kiholela holela, pia zilikuwa za kuwashutumu walioambukizwa. Maelezo haya ni ya muhimu sana katika utafiti wangu. Hata hivyo tofauti na utafiti huu ni kuwa sitiari zilizoibuliwa katika utafiti wangu zilisheheni dhima anuwai. Hata hivyo dhima kuu ya kauli za kisitiari zilizoibuliwa ziliwezesha mawasiliano kutekelezwa ,ya VVU/UKIMWI na masuala husika, bila unyanyapaa au kuwashutumu walioathirika.

### 2.1.2 Mawasiliano na VVU/UKIMWI

Kimsingi mawasiliano ni utaratibu ambao huwawezesha viumbe kupashana habari/ujumbe. Utaratibu huu ni wa njia mbili ambapo kuna anayetoa ujumbe na anayepokea au mlengwa wa ujumbe.

Utaratibu huu huhusisha:

i. Kuhamasisha mawazo, taarifa, mwelekeo, fikira na hisia kutoka kwa mwasilishi hadi kwa mlengwa wa mawasiliano.
ii. Njia za kuwasilisha ujumbe. Hizi huhusisha maandishi, mdomo, simu na redio.
iii. Kupokelewa kwa ujumbe, kufasiriwa, kutekeleza kulingana na mahitaji ya ujumbe au fasiri ya mpokezi wa ujumbe

Ili mawasiliano yawepo baina ya mwanadamu na mwenzake, ni muhimu pawepo na lugha ambayo inatumiwa na kueleweka na wote. Aidha, pana haja ya kutumia na

kuelewa ishara alizobuni mwanadamu na kuzipa maana ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano. Mathalani, mwanadamu amebuni ishara ya tabasamu kuleta maana ya kufurahi, kuchangamka huku kununa kukiwakilisha ukosefu wa furaha na hasira.

Mwanaisimujamii husema kuwa katika mawasiliano ya mwanadamu, asilimia 85% hujumuisha ishara na 15% ndiyo hujumuisha maneno. Aghalabu, ishara huhusisha matumizi ya viungo vya mwili, namna watu wanavyotagusana au kugusana wanapowasiliana au wanapozungumza, kiasi cha kukaribiana au kuwa mbali kati ya wazungumzaji, mavazi yao na namna sauti inavyotoka. Sauti inaweza kutolewa kwa uketo wa juu, kadri au chini. Ishara za mwili huweza kuwasilisha ujumbe fulani kutegemea utamaduni wa wahusika. Mathalani kukonyeza au kupia macho ni ishara ya mapenzi.

### 2.1.3 Tamathali za Usemi

Wamitila (2012), anasema kwamba tamathali ni neno au kifungu ambacho kina maana iliyofichwa. Matumizi ya tamathali za usemi yamezoeleka sana sio tu katika riwaya au kazi za kifasihi bali pia katika lugha ya kawaida. Tamathali za usemi zina mchango mkubwa katika kuifanya kazi ivutie na iwe na msisitizo na mnato mkubwa.

Tamathali za usemi ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii ili kutia nguvu katika maana, mitindo na hata sauti katika maandishi ama kusema. Wakati mwingine hutumiwa kama njia ya kuipamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu wa lugha. Hii ina maana kwamba ili msomaji wa kazi yoyote ya fasihi apate ujumbe hana budi kufikiri kwa kina.

Pia tamathali za usemi ni fungu la maneno lililogeuzwa maana yake kamili ili liwakilishe maana nyingine (Msokile, 1992). Msokile ana maana kuwa katika

tamathali zipo maana asili ya neno na matumizi mengine ya kisanii ambayo msanii anapaswa kuyatumia ili aweze kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira.

Tamathali za usemi ni viwakilisho au vifananisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti zinazofanana. Huu ni usemi unaobadilisha maana dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu ya fasihi iliyokusudiwa na msanii (Mwamanda, 2008). Kwa ujumla tamathali za semi ni maneno au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii au waandishi wa kazi za fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata katika sauti za kusema au maandishi. Hutumika katika maongezi ya kawaida kwa lengo la kuipamba lugha na kuongeza utamu katika lugha inayotumika. Tamathali hizi huweza kugawanyika katika vipengele tofautitofauti kama vile tamathali za mlinganisho, tamathali za mafumbo, tamathali za msisitizo pamoja na tamathali nyingine za semi. Vipengele vya tamathali za semi ni muhimu sana katika kuunda au kutoa msisitizo wa maana pamoja na kuunda maana mpya katika lugha husika.

Kobia (2008) anadai kuwa sitiari zinazotumika kuwasilisha masuala ya VVU/UKIMWI katika lugha ya Oluluyia, ni ishara ya jinsi ugonjwa huu wa UKIMWI ulivyoenea na utambuzi wake katika jamii hii. Anaendelea kusema kuwa aina za sitiari zilizoibuliwa ni za uambukizaji, dalili na za jinsi ya kuangamiza ugonjwa huu. Sitiari hizi zina umuhimu kama: kufahamisha, kutahadharisha, kuonya na kuogofya. Kobia anasema kuwa uibuaji, uundaji na uchanganuzi wa sitiari unatokana na tamaduni za jamii inayotumia lugha ya oluluyia. Ingawa idadi ya watu wanaoambukizwa inaendelea kuongezeka, Kobia anasema kuwa, wanajamii wameelimishwa kutoka kwa vyombo vya habari mbalimbali, ila hawataki kubadili tabia zao. Utafiti wa Kobia unatofautiana na utafiti huu kwa njia hii; utafiti huu

ulijikita katika kauli za kisitiari na kitasfida zinazotumiwa katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala yake, kati na baina ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi katika Kiswahili. Kisha nilizichanganua kwa misingi ya kuangalia asili, uhusiano na majukumu ya sitiari katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika, uchanganuzi ulioendeshwa na nadharia ya Umaanisho na Mawasiliano ya Kiutambulisho.

Momanyi (2004), ametumia neno ‘dudu’ kurejelea janga la UKIMWI ambalo limeshambulia miji mbalimbali ya Kenya. Jambo linalojitokeza katika kazi ya Momanyi ni kwamba sitiari kama kipengele cha lugha kinachotumika katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI, hakijaelezwa kwa kina na majukumu yake hayajitokezi bayana. Hata hivyo, kuna kauli nyingi za kisitiari zinazotumiwa kuwasilisha masuala ya VVU/UKIMWI wala si sitiari moja tu vile Momanyi anavyodai.

Ogechi (2005) ameangazia kwa kina lugha (sheng) inayotumiwa na vijana katika Chuo Kikuu cha Moi kurejelea masuala ya ngono na UKIMWI. Anaeleza kwamba, vijana kwa kutumia msimbo wao wa ‘sheng’ na ‘engsh’ wana misamiati anuwai ya kurejelea ngono na VVU/UKIMWI. Tofauti na utafiti wangu ni kuwa, nilikusanya kauli za tamathali za usemi ambazo ni sitiari na tasfida ambazo hutumiwa katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI katika mazungumzo yao ya kawaida katika Kiswahili.

Mawadza (2004) anadai kuwa nchini Zimbabwe, tangu ugonjwa huu ugunduliwe sitiara zimeibuliwa zinazorejelea hali hii ya UKIMWI pamoja na watu walio na virusi vinavyosababisha hali hii. Sitiari hizi ambazo zimeorodheshwa hapa chini zinaashiria hali ya VVU/UKIMWI, nazo ni: Akatenga stand (mtu aliye na VVU), ava

mudepasture launge (yumo katika chumba cha kusafiri), akakwira bhazi (amepanda basi la kifo), Bhazi rakasvika (basi la kifo limefika). Sitiari za matanga: Manje manje masofa panze (matanga ya mtu wa VVU), Tinomunwira manje manje (Maana yake hivi karibuni tutakunywa bia katika matanga ya mtu aliyeaga kutokana na VVU/UKIMWI).

Mawadza (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa wingi wa sitiari hizi ni kuzua uoga, hofu na uelewaji wa ugonjwa huu. Utafiti huu unatofautiana na utafiti wangu, kwa njia hii, kauli za kisitiari na kitasfida ambazo zimeibuliwa katika utafiti wangu ni kwa minajili ya kurahisisha mawasiliano juu ya VVU/UKIMWI. Hata hivyo, zina majukumu mengi kama kukuza maadili ya kijamii bali si kuwapa woga tu wanajamii au kuwashutumu walio na hali hiyo au wanajamii. Aidha, zimechangia katika upanuzi wa kimaana wa kauli tofautitofauti ambazo katika miktadha tofauti huwa na maana tofauti.

Naye Bwanali (2004) nchini Malawi anadai kuwa sitiari zimeibuka katika lugha ya Cilewa kuhusiana na hali ya VVU/UKIMWI ili kufanikisha mawasiliano, kwa sababu nchini Malawi kuzungumzia VVU/UKIMWI na masuala husika waziwazi ni jambo la aibu. Mfano wa sitiari zilizoibuliwa kwa minajili ya kurejelea VVU/UKIMWI ni pamoja na: magawagawa, kaliwondewonde, edzi, hang’al na mdulamoyo.

Wanawake waandishi wa Zimbabwe, wametumia kauli mbalimbali za kisitiari katika uandishi wao wa hadithi fupi juu ya masuala ya VVU/UKIMWI na ngono. Hii ni kwa sababu utamaduni wa Shona haumruhusu yeyote kusema bayana masuala haya kwa sababu ni jambo la mwiiko. Kati ya hadithi 24 walizoziandika, hadithi 14 ndizo zimetumia kipengele cha sitiari kuwasilisha masuala ya VVU/UKIMWI. Wanadai kwamba, kupitia kwa kipengele hiki cha sitiari mawasiliano yametekelezwa bila

kuvunja miiko ya jamii. Wanaendelea kudai kuwa, ili maana kusudiwa iweze kufahamika lazima msemaji na msikilizaji wahusishe kauli tumizi katika miktadha husika. Waandishi hawa wanadai kuwa chanzo cha maambukizi ya VVU/UKIMWI ni uasherati. Mfano wa sitiari walizoziibua ni pamoja na vitenzi vinavyohusiana na ngono; Kuroyiwa (kurogwa), Kuruma (to bite), Kurwara (nguva ndefu – kuwa mgonjwa kwa muda mrefu), Kujuruja (kuvuna), Kudya ( kula), Kuwanza (kuwa na wapenzi wengi). Nomino zinazohusishwa na VVU/UKIMWI ni pamoja na: Mbonje (madoa doa), Tsvina (uchafu), Ngwena (mamba), Majuru (mchwa).

Utafiti uliotekelezwa nchini Lesotho (2009), kuhusu lugha iliyotumiwa kuwasilisha masuala ya VVU/UKIMWI, ngono na kitendo cha kuwa na wapenzi wengi, ilibainika kwamba ilikuwa na wingi wa kauli za kisitiari. Ilibainika kuwa sitiari hizo hutumika kuwasilisha masuala haya, kwa sababu wazungumzaji wa Lesotho hawazungumzii masuala haya waziwazi. Katika utamaduni wa Lesotho ni mwiko kuzungumzia masuala ya VVU/UKIMWI na ngono, hivyo basi wana Lesotho wameibua sitiari za kuwasilisha masuala haya. Hata hivyo kulingana na kitoa ujumbe mmoja, alisema kwamba, kuwa na wapenzi wa kando ni sehemu ya utamaduni wao, jambo ambalo linasababisha maambukizi ya VVU/UKIMWI kuongezeka. Tofauti na utafiti wangu ni kwamba, nilikusanya data yangu kutoka kwa vijana wa Chuo Kikuu cha Moi katika lugha ya Kiswahili. Pia nimechunguza asili na majukumu mengine ya kauli za kisitiari na tasfida mbali na kuwasiliana tu.

Lugha inayotumika kuwasilisha masuala ya ngono na UKIMWI nchini Zambia ni ya tasfida, lugha isiyo wazi na iliyo ya uana sana. Mfano wa tasfida zinazotumiwa ni kama vile Chirombo, kumrejelea mwanamume (fahali), yaani mwanamume ni mwenye nguvu anayetawala katika jamii. Magawagawa (mgawo) VVU/UKIMWI

kwa maana kuwa ugonjwa huu unaambukizwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine (Moto, 2004).

Mulokozi na Kahigi (1979) wanasema kwamba, sitiari ni tamathali ambayo athari yake hutegemea uhamishaji wa maana na hisi kutoka kwa kitu au dhana moja hadi nyingine tofauti. Vitu hivyo viwili vyenye kuhusishwa kwa kawaida huwa havina uhusiano wa moja kwa moja. Maelezo haya ni ya kimsingi kwa utafiti huu.

Wamitila (2003) anasema, sitiari ni tamathali ya semi ielezeayo sifa za kitu fulani kwa kusema kingine. Anaendelea kufafanua kuwa, sitiari huhusisha vitu viwili ambavyo ni tofauti kitabia na kimaumbile. Wamitila (2008) anadai kwamba sitiari ni ulinganishi pasipo na matumizi ya maneno yanayoashiria ulinganishi kama: ja, mfano wa na mithili ya. Anaendelea kusema kwamba dhana ya sitiari inatawala si tu katika mazungumzo bali pia katika maandishi kwa kiasi kwamba inafaa kuchunguzwa pekee badala ya kujumuishwa na tamathali nyinginezo. Msingi wa sitiari ni uhamishaji wa maana. Wamitila anaendelea kusema kwamba, sitiari ni tamathali ya usemi ambayo kwayo kitu, matendo au vitu vyenye hulka na sura mbalimbali hulinganishwa na hali sawasawa na maumbile au jinsi ya utendaji. Maneno ‘kama’, ‘kwa mfano’ na ‘kama vile’ hayatumiki.

Aidha, Wamitila (keshatajwa) anaendelea kusema kwamba, maana huwa inahamishwa kwa vile hakuna matumizi ya viungo. Kwa mfano, unaposema: *Yule ana mdudu.* Kauli hii ina maana kuwa mwashiriwa ana virusi vya UKIMWI. Ulinganishi huu wa kiubunifu huweka msisitizo katika kile kinachosemwa. Katika kuelewa kauli hii, msemaji anayabana maneno mengi na badala yake anatumia neno moja ambalo msikilizaji wake atalipanua kwa kutumia ufaafu kufikia maana iliyokusudiwa, kwamba mwathiriwa ana virusi vya UKIMWI na hali hiyo imefananishwa na mdudu

ambaye kwa kawaida tunamjua ni kiumbe mdogo ambaye huharibu mimea shambani, jinsi VVU/UKIMWI hufanya katika mwili wa mtu. Uchunguzi wa Wamitila wa sitiari kama kipengele cha lugha kitumikacho katika mawasiliano, ulifaa katika utafiti huu kwa sababu ulimpa mtafiti msingi wa kuelezea jinsi wanafunzi wanavyowasilisha masuala nyeti kwa kutumia kauli mbalimbali za kusimba maana katika mazungumzo yao kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika katika miktadha yao teule kimajibizano katika kuangazia masuala yanayowakumba kimaisha.

Sitiari ni dhana inayotokana na neno ‘sitiri’, lenye maana ya kuficha au kufunika. Kuhenga (1977), anasema kwamba matumizi ya sitiari, ni kitendo cha kufunika maneno ambayo yana ukali kwa masikio ya msikilizaji. Kwa mujibu wa Islam na wenzake (2009), tasfida ni matumizi ya lugha kwa njia ya kuepuka kutaja mambo yanayohusiana na uchafu wa matusi au karaha ya aina fulani. Lugha huwa haitumiwi kwa njia wazi kutokana na miiko ya jamii inayohitaji baadhi ya mambo kuwekwa siri au kusemwa kiungwana au kiadabu. Anaendelea kusema kwamba, watu wa kila jumuiya huwa na tabia ya kutaja mambo yanayofikiriwa hayafai kutajwa hadharani kwa kuyafunika kwa maneno tofauti. Mfano Waswahili hutumia maneno kama, *kwenda haja badala ya kwenda kunya*.

Wamitila (2008) anasema kuwa tasfida ni mbinu inayotumiwa katika maongezi au lugha ya kila siku kufichia ubaya, uozo au uovu fulani kwa kutumia maneno au lugha ambayo inapunguza makali au uozo, ubaya au uovu unaozungumziwa. Tasfida ni mbinu inayotawala au kutumika kwa mapana si tu katika maandishi bali pia katika mazungumzo ya kila siku. Wamitila anaendelea kusema kuwa, tasfida ni neno au mfululizo wa maneno ambayo huchukua nafasi ya maneno ambayo si safi au mawazo

ya kushangaza kwa yale laini na ya heshima. Kwa mfano kauli kama hii, *kutoka maisha*, ni maelezo yanayotumika kurejelea kifo.

Tasfida humsaidia mnenaji kujieleza kwa njia ya kupendeza na kumfurahisha mtazamaji na msikilizaji. Anaendelea kusema kwamba, tasfida ni mbinu inayotawala au kutumika kwa mapana si tu katika lugha ya kila siku bali pia katika matini mbalimbali.

Mazrui (1992), mbinu ya sitiari inafanana sana na ile ya tashibiha (ni yale maneno yanayofananisha kitu au kitendo kimoja na kingine. Mfano, anafanya kazi kipunda. Tofauti iliyopo ni kwamba katika tashibiha, yale mambo mawili yanayofananishwa hutokea waziwazi, moja likawekwa kando ya lenziwe, pindi katika sitiara mambo yenyewe huunganishwa na kuwa dhana moja.

Katika matumizi ya kawaida ya lugha, Fromkim na Rodman (1988), wanasema kwamba jamii katika hali yake ya uvumbuzi wa lugha hubuni maneno na kisha huamua kile kinafaa kuzungumzwa kwa upole na kile ambacho hakifai. Wanadai kwamba maneno yote yako wazi kwa mzungumzaji ili ayatumie lakini muktadha wa jamii huamua kile husemwa, na kisemwe wapi na lini. Wanaendelea kusema uchafu na urembo wa lugha hutambulika katika sikio la msikilizaji au sikio la jamii nzima kwa jumla. Maelezo haya yalinifaa katika utafiti huu kwani ni msingi bora kwa kazi hii. Nilikusudia kubainisha sitiari na tasfida zinazotumika kati na baina ya wanafunzi katika mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika. Vipengele ambavyo vimeibuliwa na wanafunzi ili kuwasiliana bila kuwakera wenzao.

Hymes (1964) kwa kumnukuu Nadel (1954), na Wardhaugh (2002) amewataja Wanupe wa Afrika Magharibi kama mojawapo wa watu wapole ulimwenguni kwa kufanya uteuzi mwafaka wa maneno yanayofaa zaidi na yasiyofaa katika

mazungumzo. Hutumia tasfida moja kwa moja ili kutaja sehemu nyeti za mwili. Trudgill (2002), anasema kwamba katika jamii nyingi mazungumzo ya jinsia tofauti, vyeo na umri hutofautiana na sio kwa hayo tu bali pia hutofautiana kulingana na muktadha wa kijamii ambapo mzungumzaji hujipata. Maelezo haya yalikuwa ya manufaa kwetu kwani tulichunguza jinsi hali na miktadha ya jamii lugha, humsaidia mnenaji kuibua na kutumia sitiari na tasfida anuwai katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI.

Njeri (2007) alichunguza tasfida katika mazungumzo kuhusu VVU/UKIMWI na kusema kwamba kunao wakati ambapo tasfida hukwamiza mawasiliano hasa pale ambapo pana uana, umri na hata kazi wazifanyazo wazungumzaji na wasikilizaji. Anasema ingawa tasfida hutumiwa kama mikakati ya kupunguza athari hasi, baadhi yazo zina athari za uso bado. Utafiti huu ulitufaa kwani, mtafiti amechunguza umuhimu wa matumizi ya tasfida katika mawasiliano kuhusu ugonjwa wa UKIMWI, kwa kutumia lugha ya Kikikuyu. Maelezo haya ni bora katika utafiti huu. Hata hivyo, tofauti na utafiti wetu ni kwamba unabainisha na kuchunguza kauli za kisitiari na kitasfida zitumiwazo na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi, kuwasiliana kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika. Utafiti huu pia umeshughulikia dhima ya tamathali hizi (tasfida na sitiari) katika kuwasiliana kuhusu hali ya VVU/UKIMWI na masuala husika, bila kumshutumu yeyote aliye na hali hii ya VVU/UKIMWI, katika lugha ya Kiswahili.

Mukaria (2011) anazungumzia aina tofauti za tasfida anapoandika kuhusu maneno ya miiko na tasfida katika lahaja ya Kiimenti. Kazi yake, ilitufaa kwa sababu, ameeleza dhana ya tasfida kisha ameziainisha tasfida katika makundi tofautitofauti kulingana na malengo yake ya utafiti. Uchunguzi huu ulitufaa kwa sababu ulimpa mtafiti msingi

wa kuelezea tasfida na jinsi ya kuziainisha katika makundi na kuzichanganua kulingana na malengo ya utafiti katika lugha ya Kiswahili.

Wambua (2009) alitafiti kuhusu tofauti ya matumizi ya kilahaja na mitazamo ya leksika za miiko na tafsida katika jamii ya Kikamba. Alitofautisha jinsi mitazamo tofauti inavyojitokeza katika matumizi na maana ya leksika za miiko na tasfida kwa kulinganisha lahaja za lugha ya Kikamba. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu, umeshughulikia nafasi ya kauli za kisitiari na kitasfida zinazotumiwa katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi, kwa mwongozo wa nadharia ya Umaanisho ya Grice (1975) na ya Mawasiliano Kiutambulisho ya Giles (1982), nadharia ambazo ni tofauti na ya mtafiti huyu.

Mutiso (2005) amezungumzia maneno ya miiko ambayo hutumiwa katika lugha ya Kikamba hasa katika hali ya kumdunisha mwanamke. Kazi yake ni muhimu katika utafiti huu, kwa vile inatupa msingi wa mitazamo mbalimbali ya uana katika jamii za Kiafrika. Hata hivyo, utafiti wake unatofautiana na wetu kwa kuwa ameshughulikia jinsia ya kike kwa kuilinganisha na ya kiume. Ameonyesha jinsi jinsia moja imedhalilishwa na jinsia nyingine, nasi tumetafitia kwa kina jinsi matumizi ya tasfida na sitiari hurahisisha mawasiliano katika muktadha wa VVU/UKIMWI na masuala husika bali si kumnyanyasa tu mwanamke katika jamii za Kiafrika.

Neno tasfida linatokana na neno la Kigiriki, ambalo lina maana ya "matumizi ya maneno mazuri," kwa masikio. Kwa mujibu wa Islam na wenzake (2009), tasfida ni matumizi ya lugha kwa njia ya kuepuka kutaja mambo yanayohusiana na uchafu wa matusi au karaha ya aina fulani. Lugha huwa haitumiwi kwa njia wazi kutokana na miiko ya jamii inayohitaji baadhi ya mambo kuwekwa siri au kusemwa kiungwana au kiadabu.

Watu wa kila jumuiya huwa na tabia ya kutaja mambo yanayofikiriwa hayafai kutajwa hadharani kwa kuyafunika kwa maneno tofauti. Dhana ya tasfida imeelezwa na wanaisimu wengi kwa njia tofautitofauti. Kwa mfano, Allan na Burridge (1991) wanasema kwamba tasfida ni neno, ambalo ni tafsiri kutoka kwa neno *'Euphemism'* ambalo pia limeundwa kutokana na uambatanishi wa viambajengo vya Kigiriki '*eu'* kumaanisha 'nzuri' na '*pheme*' ambalo humaanisha kuzungumza. Kwa hivyo neno tasfida ambalo ni tafsiri ya '*eupheme*' humaanisha kuzungumza kwa maneno mazuri au kuzungumza kwa usemi usioudhi na kumdhuru mtu.

Gatambuki (2009) akirejelea mawazo ya Bright (1985) na Allan na Burridge (1991), anaeleza kuwa tasfida ni kutumia maneno mazuri, matamu, yanayopendeza, yaliyotiwa nakshi yakavutia. Pia anasema ni kutokusema maneno moja kwa moja ili kuepuka kudhuru uso wa msikilizaji. Harry (1954) anasema kwamba lugha huashiria mfumo wa jamii husika, na kwa hivyo kuna uhusiano wa lugha na jamii ambapo lugha hiyo hutumika. Katika kila jamii huwa kuna namna lugha hutumiwa na wakati mwingine huleta aibu ama hata kuwa vigumu kuyatumia maneno fulani katika lugha kwani ni mwiko. Kwa sababu hii watumiaji lugha huweza kukwepa hali hiyo kwa kutumia lugha inayoonekana nzuri au yenye adabu nayo huitwa tasfida. Hivyo basi tasfida ni hali ya kutumia maneno yenye adabu.

Tunakubaliana na maelezo haya kwa sababu, utafiti wetu ulidhihirisha kwamba wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi huunda kauli za kitasfida kutoka kwa mazingira yao ili waweze kuwasiliana kwa urahisi, kwa upole na kwa adabu bila kumshtumu yeyote mwenye ameathirika kwa njia moja au nyingine kutokana na hali hii ya VVU/UKIMWI. Hivyo basi tunaweza kusema kwamba tasfida ni maneno

yanayoundwa na kila jamii ili kurahisisha mawasiliano, kuyafanikisha na pia kuhifadhi nyuso za wanaowasiliana.

Katamba (1985), anaeleza tasfida kama neno linalotumika kufafanulia lugha, mawazo na dhana ambazo hupunguza uchukivu unaoletwa na istilahi tofautitofauti katika tamaduni za jamii au kundi lolote la watu. Nakubaliana na mawazo ya Katamba kwani katika mawasiliano kunaweza kuzuka hali za kutoelewana kutokana na matumizi ya lugha yasiyo na adabu au hata isiyozingatia miiko ya jamii za Kiafrika. Nakubaliana pia na Katamba (keshatajwa) kwamba tasfida zinapotumiwa hupunguza kutoelewana na uchukivu unaotokana na matumizi ya miiko kwa kutojali hali za wengine. Katamba anaendelea kusema kwamba tasfida ni leksimu inayodhihirisha upole. Upole huzuia chuki na kutoelewana kwa watu katika jamii fulani au watu katika vikundi mbalimbali.

Ortony (1993) naye anasema, tasfida ni kule kusema kitu kwa namna ambayo mtu huchukua tahadhari ili asiseme mambo ambayo huchukiza na kumwaibisha mzungumzaji au hadhira yake. Maelezo haya yalinifaa kwani vijana wameibua kauli anuwai za kitasfida na kisitiari ambazo huwasaidia kuwasiliana kuhusu VVU/UKIMWI bila kumwaibisha mzungumzaji, msikilizaji, wazungumzaji au hadhira.

Leech (1983) anaeleza tasfida kama ile hali ya kutoa maana hasi na kutia maneno nakshi ili yaonekane kuwa mazuri. Anaelezea zaidi kwa kusema kwamba mambo haya huwa katika kila jamii kutoka zamani ili kukwepa mijadala ambayo haifurahishi wengine. Mambo kama ngono, kifo, magonjwa na sehemu mbalimbali za mwili wa binadamu huwa mwiko kuyataja waziwazi, jambo ambalo huifanya jamii lugha husika kuunda tasfida ili kuwasiliana kwa upole, bila kumshutumu yeyote. Kulingana

na TUKI (1990), tasfida au usafidi ni matumizi ya maneno ya staha badala ya yale halisi. Maelezo haya ni muhimu kwetu kwani yalitupa mwanga zaidi kuhusu matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi hasa tamathali za usemi.

Wardhaugh (2002) anasema kuwa lugha ya tasfida huruhusu watumizi lugha kufunika hali katika maisha na kuziwasilisha kwa njia ifaayo, kwa upole na kwa njia kubalifu kwa hadhira. Tasfida huruhusu wanajamii kuzungumzia vitu visivyofaa kwa njia ifaayo ili kupunguza makali masikioni mwa wasikilizaji. Kwa mfano tasfida hutumika katika kueleza kitendo cha kujamiana, kifo, sehemu za siri za kiume na za kike na hali ya ugonjwa wa VVU/UKIMWI kwa namna ya upole sana. Tasfida pia huwawezesha watumizi lugha kuvipa vitu visivyofaa vibandiko na hata majina ya kuvifanya vipendeze, hivyo basi kufanikisha mawasiliano katika jamii.

Ullman (2005) anasema kwamba kila utamaduni huwa na mambo ambayo hayazungumzwi wazi ambayo huitwa miiko. Haya ni mambo au chochote kilichokatazwa katika jamii kwa sababu za kidini au za kiutamaduni. Katika matumizi ya lugha watu huyakwepa matumizi ya miiko na kujikita kwa kutumia lugha inayoonekana kuwa nzuri katika miktadha tofauti kulingana na mazingira, na hii ndiyo huitwa tasfida.

Kutokana na utafiti wetu tumetambua kwamba kauli za kitasfida huundwa na watumizi lugha wa jamii yenye utamaduni mmoja. Tasfida hizi huundwa kama njia mojawapo ya kueleza mambo au kusema jambo kwa njia ya kutumia maneno au lugha ya adabu. Ili mambo yanayoonekana mabaya au yanayoaibisha na kuleta unyanyapaa, tasfida hutumiwa kama njia ya kupunguza makali ya maneno kwa upole na adabu ili kuhifadhi uso wa mtu mwingine.

Rawson (1981) aliainisha tasfida katika kategoria chanya na hasi. Tasfida chanya kulingana na Rawson hutiwa chuku na huonekana muhimu sana kuliko vile ilivyo. Rawson anaeleza kuwa, Waingereza na Wamarekani hupendelea tasfida ambazo zimetiwa chuku hasa kutasfidi kitu ambacho hakipendezi na kinadhuru. Rawson pia anasema kuwa tasfida zinazohusu watu wanaofanya kazi ndogondogo na duni huinua hadhi ya kazi hizo ili kustiri nyuso za wafanyikazi wa kazi hizo au kuzifanya kazi zenyewe zionekane nzuri. Maneno ya tasfida chanya hutiwa nakshi katika matumizi ya misamiati ya kisiasa, kijeshi na hali mbalimbali za kijamii kama vile VVU/UKIMWI. Maoni haya yalikuwa ya muhimu katika utafiti huu kwani yalituwezesha kubainisha aina za tasfida mbalimbali katika utafiti wetu, yaani kukusanya tasfida chanya na hasi.

Kandagor (2013), anadai kwamba lugha ina nafasi maalumu na muhimu katika vita dhiti ya UKIMWI. Hayo yote hufanyika kupitia kwa mbinu na mikakati anuwai ambayo imewekwa ili kuwasilisha ujumbe unaobeba maandishi au picha zinazoeleza njia za kujiepusha au kupiga vita ugonjwa huu. Anaendelea kusema kwamba mawasiliano ni njia fulani inayoweza kuwaleta watu pamoja, jambo ambalo husababisha mtagusano ambao huleta athari ambazo zaweza kuwa chanya au hasi. Aidha, anadai kwamba utamaduni huibua lugha, tabia, ishara na maana na zinatokana na mambo fulani. Katika jamii tunajifunza kutambua ni maneno gani tunaweza kutumia katika mawasiliano, maneno yepi yanafaa kuteuliwa na kutumika katika mawasiliano mbalimbali. Katika uchunguzi wake, alijikita katika nafasi ya lugha na vyombo vya kimawasiliano katika vita dhidi ya UKIMWI nchini Kenya. Tofauti nyingine ni kuwa utafiti wake ulifanywa katika taasisi mbalimbali zinazohusika na utafiti wa UKIMWI na pia wagonjwa wenyewe kwa kutathimini nafasi ya lugha katika harakati zao za kukabiliana na ugonjwa huo.

Hata hivyo, japo kuna tofauti za kiuchunguzi, kazi ya Kandagor (keshatajwa) ilikuwa na umuhimu katika utafiti wetu, kwa kuwa tulipata mwanga zaidi kuhusiana na namna lugha ilivyotumika kuwasilisha ujumbe kuhusu UKIMWI kwa minajili ya kupiga vita ugonjwa huu. Utafiti wetu unajikita katika kuchanganua kauli za kistiari na kitasfida zinazotumiwa katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI kati na baina ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi.

## 2.2 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya Umaanisho na Nadharia ya Mawasiliano Kiutambulisho.

### 2.2.1 Nadharia ya Umaanisho

Nadharia ya Umaanisho iliasisiwa na Paul Grice (1978, 1995). Katika nadharia hii anaeleza jinsi watumiaji lugha katika mawasiliano hufahamu kauli tofauti ambazo hazihusiani katika diskosi na kuzifasiri kama zilivyokusudiwa. Aidha, anadai kuwa msikilizaji huwa na uwezo wa kufasiri na kuratibu ujumbe wa kiisimu na usio wa kiisimu katika ufahamu wake.

Nadharia hii pia imejengwa katika kanuni ya ushirikiano, ambapo umaanisho umo ndani ya ushirikiano. Ushirikiano huzua umaanisho wa jambo lililomaanishwa na kauli tofauti kisha jambo hilo lieleweke na kufasiriwa ipasavyo na msikilizaji husika. Hivyo basi, kuna ushirikiano baina ya dhana ya umaanisho na ile ya ushirikiano. Kulingana na Grice, kuna aina mbili za maana katika usemi au kauli yoyote. Maana hizi ni maana ya lugha na maana ya msemaji. Maana ya lugha ni maana inayotokana na vipashio vya sentensi ilhali maana ya msemaji ni maana inayoibuka kutokana na matumizi ya maneno yanayoteuliwa na kutumika katika mawasiliano.

Mawazo haya ni muhimu katika utafiti wetu, kwamba vijana waliweza kurejelea dhana ambazo zina maana tofauti ili ziweze kuwakilisha maana kusudiwa katika mazingira tofauti, jambo ambalo liliwawezesha kuwasiliana juu ya VVU/UKIMWI na masuala husika kwa kutumia kauli mbalimbali ambazo zina maana tofauti kabisa ya kimsingi.

Kwa mujibu wa Grice, nadharia ya umaanisho imekuwa nadharia muhimu sana katika tawi la isimu. Hii ni kwa sababu umaanisho hushughulikia maana inayojitokeza kutokana na maneno ya msemaji. Grice anasema kuwa msemaji husema au hutoa maana ambayo haijitokezi katika vipashio vya kisarufi kama vile maana za maneno katika tungo zozote katika lugha na mawasiliano. Kwa mfano katika mazungumzo haya, jibu la (b) halikubaliani na swali la msemaji. a) Nipe kalamu. b) Nimepoteza funguo. Tukirejelea mazungumzo hapo juu, ikiwa (a) atauliza, kwa nini hujafungua dawati? Jibu litakuwa lilelile lakini wakati huo ikiwa na maana tofauti. Hivyo msemaji humaanisha mambo mengine tofauti na anavyosema ama kulingana na muktadha.

Kwa upande mwingine, Levinson (1983) anasema kuwa umaanisho ni nadharia inayoonyesha kwamba kuna uwezo wa kumaanisha jambo tofauti na linalosemwa katika tungo. Katika muktadha huo basi, ni muhimu kutaja kuwa katika mchakato wowote wa mawasiliano, maana anuwai huibuka kutegemea nia ya msemaji pamoja na hisia anayotaka kuibua kwa mpokeaji ujumbe. Grice (1975) anaongezea kwa kusema kuwa maana hupatikana kutokana na ushirikiano baina ya wasemaji na wasikilizaji. Ni katika ushirikiano huu ambapo msikilizaji huweza kutambua kwa nini msemaji anasema anachosema na analenga nini kwa kusema hivyo. Ili kusisitiza hoja

yake Grice anapendekeza mambo muhimu ya kuzingatiwa katika mawasiliano yoyote. Mambo hayo muhimu ameyaita kanuni ya ushirikiano.

Kwa mfano katika utafiti wetu, watafitiwa walihamisha kauli kutoka muktadha mmoja hadi mwingine na katika kufanya hivyo, kauli hizo ziliweza kudokeza maana tofauti kabisa na maana ya kimsingi. Hivyo basi kutokana na ushirikiano wa wazungumzaji wakaweza kuwasiliana bila ya kuibua hisia mbaya kwa msikilizaji au wasikilizaji bila ya kuvuruga imani ya wanajamii.

Vifuatavyo ni vipengele muhimu katika kanuni ya ushirikiano:

1) *Kipengele cha idadi*. Katika kipengele hiki, anasema kuwa msemaji anapaswa kusema mambo yanayotosheleza katika mawasiliano husika. Yaani, katika kujieleza msemaji hafai kuzidisha wala kupunguza maelezo yake. Kwa kufanya hivyo, hoja yake itaeleweka bila taklifu yoyote.
2) *Kipengele cha ukweli*. Katika kipengele hiki, anasema kuwa msemaji ahakikishe kuwa anasema ukweli unaouamini na kuujua ili mawasiliano yasitatizwe. Hata hivyo, anaendelea kueleza kuwa, kuna tamaduni ambapo vitu na watu fulani hawarejelewi kwa majina yao halisi pengine kwa sababu za imani zao. Katika jamii kama hizo pengine kuna wingi wa majina ya kuelezea watu au dhana zingine.
3) *Kipengele cha uhusiano*. Katika kipengele hiki, Grice anasema kwamba mambo yatakayosemwa yarejelee kisemwacho. Yaani sema yanayohusiana na mada kwa wepesi wa kueleweka. Usitoe habari kwa mzunguko wa maelezo.
4) *Kipengele cha namna au jinsi*. Katika kipengele hiki Grice anasema kwamba, msemaji anapaswa kusema mambo yaliyo bayana, wazi na yaliyodhahiri bila kuficha chochote. Ujumbe usiwe na utata, uwe na mpangilio na utaratibu

mzuri aidha uwe mfupi, lugha inayotumika pia lazima ieleweke na msikilizaji wake bila tatizo lolote.

Schroeder (2005), anasema kuwa mwingiliano wa watu kutoka jamii tofauti husababisha utata katika mawasiliano. Jambo hili linaweza kusababisha msikilizaji kuwa na uhusishi usiofaa katika ujumbe, kisha kutoelewa ujumbe huo. Utata huo hutokea kwa sababu jamii tofauti huwa na chukulizi tofauti. Anaendelea kueleza kuwa ufahamu wa jambo hukwama kwani kanuni ya uhusiano hupata ujumbe usio sahihi na kuupeleka kwa mpokezi bila usahihi unaofaa.

Katika mkabala huo basi, ni muhimu kwa wanaoshiriki katika mawasiliano kuelewana vyema. Anaendelea kudai kuwa katika kila jamii kote ulimwenguni kuna maneno ambayo huchukuliwa kama mwiko. Hata hivyo, jamii husika ndiyo huamua ni mambo gani yawe mwiko na ni gani yasiwe mwiko kutegemea tamaduni za jamii husika. Maelezo haya ya nadharia ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu, kauli zilizoibuliwa na wazungumzaji zilihusisha maana na kufahamika kwazo kulingana na uhusiano uliopo baina ya msikilizaji na mzungumzaji ambalo ni jambo la kimsingi katika utafiti wetu. Katika utafiti huu baadhi ya istilahi za kisitiari na tasfida zilipata maana, kulingana na jinsi zilivyohusishwa kutoka kwa muktadha chanzi hadi muktadha pokezi. Muktadha ni kipengele muhimu sana katika utafiti wetu kwa sababu, istilahi zilizoibuliwa na wanafunzi zilipata maana kutokana na muktadha wa matumizi na tamaduni za wazungumzaji.

Utafiti wetu umeeleza kuwa kuna baadhi ya mambo ambayo ni miiko kuyazungumzia katika jamii za Afrika hasa yanayohusu VVU/UKIMWI, ngono na masuala husika sababu kuu ya vijana kubuni au kuhamisha kauli mbalimbali kutoka muktadha asilia hadi muktadha pokezi. Kwa kuzingatia kanuni za Grice, wasemaji na wasikilizaji

waliweza kushirikiana na kufahamiana, jambo ambalo huwezesha kufanikisha mawasiliano ipasavyo baina ya wazungumazaji. Muktadha katika masharti ya kweli ni muhimu, na huhusisha semantiki na pragmatiki kwa pamoja ili kubainisha maana kusudiwa.

Katika uchanganuzi wetu ilibainika kuwa miktadha tofauti kama ya kitamaduni, ya diskosi, ya kijamii, ya kitambuzi na ya ufahamu wa dhana fulani ni muhimu ili kuelewa uhusiano uliopo wa kimaana katika vipengele hivi vya kisitiari na kitasfida vilivyobuniwa na vijana kwa ajili ya mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika. Hapa ni wakati ambapo neno huwa na maana zaidi ya moja kulingana na muktadha wa matumizi, hivyo istilahi moja kurejelea mambo tofauti. Ilibainika kwamba hili hutokea kwa sababu, baadhi ya maneno hubadilisha maana yanapotumika katika miktadha tofauti.

Mihimili hii muhimu katika utafiti wetu, kwa kuwa ilituwezesha kuchambua data iliyoendana na malengo mawili yafuatayo: Kuzichanganua sitiari mbalimbali zinazotumiwa katika mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi kuhusu VVU/UKIMWI; na kujadili tasfida zinazotokea katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi.

### 2.2.2 Nadharia ya Mawasiliano ya Kiutambulisho

Nadharia ya pili iliyotuongoza katika utafiti huu ni nadharia ya Mawasiliano ya Utambulisho, iliyoasisiwa na mwanaisimu Giles (1972, 1982). Nadharia hii inarejelea dhana ya utambulisho kama kigezo maalumu kinachotumiwa kumtambulisha mtu, kundi la watu, jamii au taifa fulani. Nadharia hii imeendelezwa kutoka kwa Nadharia ya Mawasiliano ya Usemi (Speech Communication Theory) ya Leech (1976). Giles na wenzake (2005), wanasema kuwa nadharia ya Mawasiliano ya Usemi ilinuia

kueleza hali inayosababisha mabadiliko katika usemaji kwenye maingiliano ya watu na matokeo ya ubadilishaji huo. Nadharia hii imepanuka kwani haishughulikii namna ya unenaji pekee, bali pia maingiliano mengine ambayo si ya unenaji kama ishara na maandishi. Nadharia hii ilitufaa katika utafiti wetu kwani ilituwezesha kuchunguza mawasiliano miongoni mwa vijana, mawasiliano ambayo yanahusu sitiari na tasfida.

Kwa mujibu wa nadharia hii, utambulisho huwa na vibainishi muhimu vinavyojumuisha lugha, mahali, uchumi, utamaduni, siasa, mavazi, na chakula. Haya yote hutumiwa kuukamilisha utambulisho.

#### 2.2.2.1 Mawazo makuu katika Nadharia ya Utambulisho

a) Huhusika na mahusiano kati ya lugha, muktadha na utambulisho. Giles na wenzake (2005) wanasema kwamba nadharia hii huhusika na mahusiano kati ya lugha, muktadha na utambulisho. Wanasema kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya matumizi ya lugha, muktadha na utambulisho wa kundi lengwa. Katika utafiti wetu ilibainika kwamba vijana hutumia lugha kwa namna yao ya kipekee. Jambo ambalo huwatambulisha katika jamii.

b) Nadharia hii huangazia kuwa watu wanapotangamana wanabadilishana usemi, sauti na hata ishara ili kujihusisha na wengine (Turner na Richard, 2010). Mawazo haya ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu, utafiti wetu ulibaini kuwa vijana waliweza kuwasiliana, kutangamana na kubadilishana mawazo kutokana na vipengele hivi vya lugha (sitiari na tasfida).Aidha ilibainika kwamba, haya matumizi ya lugha huwawezesha kuwasiliana bila ya kuwashutumu au kuwaudhi wasikilizaji na kujitambulisha katika jamii.

c) Nadharia hii, hutalii sababu ambazo huwafanya watu kusisitiza kupunguza tofauti kati yao wakati wa mazungumzo. Huangazia sifa za kibinafsi na za

makundi ambazo husababisha ujihusishaji na pia huchunguza namna mamlaka, miktadha ya kimaikro na kimakro huathiri tabia za mawasiliano.

d) Aidha, nadharia hii inaeleza kuwa tamaduni na tajriba ni vigezo muhimu sana katika mawasiliano. Maelezo haya ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu, ni kutokana na mila na desturi za jamii za Afrika ambazo zimesababisha vijana kuibua istilahi za tasfida na sitiari kwa minajili ya kuwasiliana masuala ya VVU/UKIMWI ambayo ni mwiko kuyataja bayana katika jamii za Kiafrika.

e) Vilevile, anafafanua kuwa tajriba ya wazungumzaji ni muhimu katika mawasiliano yoyote. Hii inatokana na sababu kwamba tajriba ya wazungumzaji ni kipengele muhimu sana ambacho huwawezesha kuhamisha istilahi kutoka kwa muktadha asilia hadi muktadha tofauti na kuweza kudokeza maana tofauti. Hivyo basi usemaji na tajiriba ya wasemaji hutawala katika mazungumzo.

#### 2.2.2.2 Dhana ya utambulisho

Dhana ya utambulisho ni pana mno kwa sababu inafumbata mambo mengi ndani yake. Utambulisho ni jumla ya vigezo maalum vinavyotumiwa kumtambulisha mtu, kundi la watu, jamii au taifa fulani. Vigezo hivi hubainisha kuwa kundi fulani ni tofauti na lingine, jamii moja ni tofauti na nyingine, mtu mmoja ni tofauti na mwingine au taifa moja kuwa tofauti na lingine.

Kihore na wenzake (2009), wanasema vigezo ambavyo hubainisha utambulisho wa mtu au jamii vinaitwa vibainishi navyo ni; lugha, utamaduni, historia ya jamii, siasa, uchumi, dini na mavazi. Weiner (1998) akinukuliwa na Wardhaugh anasema kuwa nadharia ya Utambulisho inaweza kutumiwa kuelezea namna mbalimbali za uteuzi wa

lugha. Anaeleza namna jamiilugha moja inaweza kuamua kutumia lugha kujihusisha na jamiilugha nyingine (makutano) ama ikatumia lugha kujitenga na jamiilugha nyingine (mwachano). Jamiilugha inaweza kugawika katika ngazi au matabaka mbalimbali kutegemea umri, elimu, mapato, dini na tabaka la kijamii, kazi na jinsia. Tofauti hizi za kitabaka huathiri mielekeo ya wanajamii kuhusu lugha yao na athari kama hizo pia huathiri matumizi ya lugha kwa kila mwanajamii. Kila mtu binafsi katika jamiilugha hujihusisha na mitindo ya matumizi ya lugha inayoambatana na tabaka lake kama njia ya kujitambulisha katika tabaka hilo. Tofauti katika matumizi ya lugha kwa mtu binafsi hutokea kutokana na uigaji wa mitindo ya kitabaka, matumizi ya lugha kimafumbo au katika lugha bunifu.

Kihore na wenzake (keshatajwa), wanayaunga mkono maoni haya ya Wardhaugh pale wanaposema kuwa, jamiilugha mbili zinapokutana na kuacha kutumia lugha yao na kuanza kutumia lugha ya jamiilugha nyingine, hapa ndipo tunasema kuwa kuna mkutano kwa jamiilugha mbili. Hii ni kwa sababu jamii lugha hizi mbili huendelea kutumia hii moja inayodumishwa na kutumiwa kwa utambulisho wa jamiilugha hiyo pana. Jamiilugha hizi zikiwa na nguvu tofauti, jamiilugha dhaifu hushindwa na ile yenye nguvu zaidi. Hali hii inaonyesha kuwa jamiilugha dhaifu haithamini lugha yake pamoja na utamaduni wake.

Iwapo makutano haya yanahusisha kikundi cha wanajamii ambao wanaacha kutumia lugha yao kabisa ili wajitambulishe na jamii lugha nyingine, hali hii inaweza kusababisha kufa kwa lugha. Makutano haya yanaweza kuwa yanaelekea juu iwapo mtu anajihusisha na tabia za watu wa tabaka la juu.Vilevile makutano haya yanaweza kuwa yanaelekea chini iwapo mtu anajihusisha na tabia za watu wa tabaka la chini.

Keller (1989) anaeleza kuwa utambulisho wa mtu umefungamana na mambo mengine kama vile lugha, utamaduni, historia ya jamii, siasa, uchumi, dini na vyakula. Kinachojitokeza hapo juu ni kuwa, kipengele kimoja au viwili havitoshi kubainisha utambulisho wa mtu, jamii au taifa. Kimsingi utambulisho wa mtu umejikita ndani ya utamaduni wa jamiilugha ambako mzungumzaji anayetakiwa kubainisha utambulisho wake ni sehemu yake. Keller anasisitiza dhana ya utambulisho kwa kutaja sifa bainifu tatu za msingi za kuzingatia katika kubainisha mzungumzaji.

a) Kwanza, ni kigezo cha lugha ya mzungumzaji ambapo anauita utambulisho wa nje unaosikika.
b) Pili, ni kigezo cha mahali alikozaliwa mzungumzaji ambako lugha anayotumia ndiyo lugha kuu ya mawasiliano.
c) Tatu, zaidi ya yote mzungumzaji anapaswa kujiona kuwa sehemu ya jamiilugha na kuwa ataendelea kuitumia lugha yake ili kuidumisha.

Kwa hivyo katika kueleza utambulisho, lugha ya mzungumzaji ni kibainishi muhimu sana. Vibainishi kama uchumi, siasa, utamaduni, historia ya jamii, dini, mavazi na vyakula hutumiwa kuukamilisha utambulisho wa mtu. Hii inamaanisha kuwa ni vigumu kubainisha utambulisho wa mzungumzaji kwa kutumia lugha peke yake bila uchanganuzi wake kwa kuzingatia jamiilugha anamotoka ambako masuala ya utamaduni, mila na desturi ni sehemu muhimu na kiungo cha umoja wa jamiilugha hiyo. Lugha ya mzungumzaji na utambulisho wake ni mambo mawili ambayo hayawezi kutenganishwa, ni kama pande mbili za sarafu moja. Maelezo kuhusu nadharia yalikuwa ya umuhimu katika utafiti wetu kwani tuliweza kuelewa kwa nini vijana waliweza kubuni istilahi za kitasfida na kistiari kwa ajili ya mawasiliano.

Nadharia zilizoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu Umaanisho na ya Utambulisho zilitufaa sana katika kuhakiki data za utafiti. Nadharia ya Umaanisho ilitusaidia katika kubainisha maana zilizoibuliwa kutokana na tasfida na sitiari zilizotumika na vijana. Kwa upande mwingine, nadharia ya Utambulisho ilikuwa muhimu kwa sababu sitiari na tasfida walizoziteua na kuzitumia vijana ziliwatambulisha katika kundi lao maalum, ambapo maneno mengi waliyoyatumia katika mawasiliano yalieleweka katika muktadha wao maalum.

Nadharia ya Utambulisho ilituwezesha kuhakiki data kuhusiana na dhima ya sitiari na tasfida katika kukuza mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi kuhusu VVU/UKIMWI: hivyo ilituwezesha kuhakiki data kuhusu vipengele mbalimbali kama vile ngono, uuke, uume, waathiriwa.

**2.3 Hitimisho**

Sura hii imeangazia mapitio ya maandishi, historia fupi ya VVU/UKIMWI, matumizi ya vipengele vya lugha yaani tasfida na sitiari katika mawasiliano mbalimbali kutokana na maandishi ya awali. Vilevile katika sehemu hii, nadharia ya utafiti na viunzi vyake vilivyotumiwa katika utafiti huu vimejadiliwa.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inahusu mbinu zilizotumika katika mchakato wa kukusanya data nyanjani kwa ajili ya utafiti huu. Katika sehemu hii nimefafanua sehemu zifuatazo: eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanya data, vifaa vya utafiti pamoja na uchanganuzi wa data.

## 3.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulitekelezwa katika Chuo Kikuu cha Moi (bewa kuu), Kenya. Chuo hiki kina idadi ya wanafunzi takribani 40,000 (wavuti wa Chuo Kikuu cha Moi, 2020), watafitiwa walikuwa wanafunzi waliosajiliwa katika taaluma za Kiswahili, yaani isimu, fasihi na lugha. Wanafunzi hao ambao walishirikishwa katika utafiti huu walitapakaa katika viwango vyote vya shahada ya msingi; yaani wanafunzi kumi kumi kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa nne na wanafunzi 5 wa uzamili kutoka Chuo Kikuu cha Moi ambao waliteuliwa kimaksudi. Waigizaji 5 kutoka klabu cha uigizaji 'Moi University know AIDS Association' pia walishirikishwa. Msimamizi kutoka kituo cha ushauri na upimaji wa hiari cha Chuo Kikuu cha Moi (bewa kuu) tulishirikisha mmoja wa washauriwa, ambapo mtafiti aliweza kurekodi mazungumzo baina ya mshauri na mshauriwa. Nikiongozwa na malengo ya utafiti huu nilifanikiwa kuwashirikisha wanafunzi wanaosomea taaluma za Kiswahili kwa sababu hapa ndiko kunakofundishwa vipengele hivi vya lugha, na hivyo basi wanafunzi walioshirikishwa katika utafiti huu wana uelewa mpana wa vipengele hivi na vingine katika maingiliano halisi.

## 3.2 Sampuli na Usampulishaji

Kulingana na Mugenda na Mugenda (2003), Nicholas Walliman (2005) na Kothari (2004), sampuli ni sehemu ndogo ya idadi jumla ya utafiti. Hivyo basi, sampuli ni kiasi cha watafitiwa ambacho huchaguliwa kutokana na idadi kubwa. Tulitumia sampuli ya maksudi iliyoendana na mahitaji ya malengo ya utafiti huu. Katika utafiti huu, walioshirikishwa ni watu walio na umri kati ya miaka 18 na 38. Tulichukulia kwamba washirikishwa hawa, wana umilisi na uelewa mpana wa lugha hasa inayoruhusu matumizi ya tamathali mbalimbali za usemi, mathalan, tasfida na sitiari. Katika kila kundi lililochaguliwa kupitia njia ya sampuli ya maksudi, tuliwahoji wanafunzi 10.

### 3.2.1 Usampulishaji wa kinasibu sahili

Usampuli wa kinasibu sahili ulitumika katika uteuzi wa wasailiwa kutoka kwa kundi lengwa ili kupata habari zilizokusudiwa. Kwa mfano mtafiti aliawateua wasichana (5) na wavulana (5). Hii ni kuhakikisha kuwa matokeo ya utafiti yanazingatia masuala ya uana hali hii imepigwa jeki na katiba ya Kenya (2010) ambayo inaeleza waziwazi kwamba jinsia au uana unafaa kuzingatiwa katika shughuli zote zinazowahusu wanajamii.

### 3.2.2 Usampulishaji wa kimfuatano

Usampuli huu, ulimwezesha mtafiti kuwarejelea wasailiwa ambao walituwezesha kuwafikia wasailiwa wengine. Usampulishaji huu ulianza kwa watu wachache na kisha waliongezeka kadiri wasailiwa wengine walivyotajwa na wasailiwa wa kwanza.

### 3.2.3 Usampulishaji wa kimatilaba

Katika usampuli huu mtafiti alilenga kundi la watu walioelekea kutegemewa kutokana na mahitaji na malengo ya utafiti huu. Hivyo mtafiti aliweza kuwateua

watafitiwa waliofaa katika juhudi ya kuhakikisha kuwa wangekuwa tayari kushiriki kikamilifu katika kutoa data iliyochukuana na malengo ya utafiti huu. Katika muktadha wa eneo la utafiti, mtafitiwa (mwanafunzi) mmoja tuliyemteua alituelekeza kwa mwanafunzi mwingine ambaye alifaa kushirikishwa katika shughuli hii ya utafiti. Kwa hivyo, mtafiti aliweza kuwateua watafitiwa/wanafunzi kumi kutoka idara ya Kiswahili kutoka kwa kila mwaka katika Chuo Kikuu cha Moi.

Ifahamike kuwa idadi hii (ya wanafunzi 10 kutoka kila kiwango) iliongozwa na mahitaji ya malengo ya utafiti. Kila msailiwa aliyeteuliwa alifaa kama mshiriki katika shughuli nzima ya kuisaka data ya utafiti huu. Aidha, wasailiwa hawa waliotapakaa katika viwango vya masomo vilivyotajwa walielekea kuwa na ukuruba kwani walitagusana na kuingiliana kwa wepesi, hali ambayo ilituwezesha kusaka na kupata data ya kutegemewa kuhusu tamathali hizi mbili: Sitiari na Tasfida.

Ifahamike kuwa wasailiwa hawa wana umilisi mpana wa lugha zaidi ya moja. Hali hii, basi bila na shaka, hudhihirisha uwezo wa wasailiwa katika kutumia tamathali hizi mbili katika kuzimudu mada mbalimbali ambazo zinajitokeza katika maingiliano yanayohusu masuala mbalimbali kama VVU/UKIMWI miongoni mwa masuala mengine yanayojiri katika maingiliano hayo.

### 3.3 Ukusanyaji wa Data

Utafiti wetu umefanyika nyanjani, na hapa tuna maana kwamba tulijikita katika Chuo Kikuu cha Moi ambapo wasailiwa washirikishwa walipatikana. Data iliyokusanywa inafungamana na matumizi ya sitiari na tasfida katika hali halisi ya maingiliano kati na baina ya wanafunzi waliosomea taaluma mbalimbali za Kiswahili katika mwaka wa 2012-2013. Data iliyokusanywa ni ya kistahilifu kwa maana ya kwamba ilichukuana na mahitaji ya malengo ya utafiti huu. Data iliyokusanywa

ilichanganuliwa katika hatua mbalimbali, kwa mfano niliziorodhesha na kuzipanga sitiari na tasfida za kila aina katika makundi mbalimbali kutegemea vipengele vilivyoshughulikiwa katika utafiti huu, ambavyo ni: maana msingi na maana dokezi, maana ya kiuhusiano, dhima ya sitiari na tasfida zilizotumiwa katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika.

Data iliyokusanywa ilitosheleza mahitaji ya utafiti huu, kwa sababu iliafikiana na malengo yaliyomwongoza mtafiti. Vipengele hivi viwili vya lugha (sitiari na tasfida) vilielekea kujitokeza sana katika maingiliano baina ya wanafunzi kwenye miktadha mbalimbali mlimojitokeza mada mbalimbali kuhusu VVU/UKIMWI.

Mbinu za ukusanyaji data mara nyingi huamuliwa kwa kutegemea mambo kama malengo ya utafiti, taaluma husika, mahali pa utafiti na matumizi ya data inayokusudiwa kukusanywa. Kutokana na hali hizi basi utafiti huu ulitumia mbinu zifuatazo mahojiano, utazamaji, kundi lengwa la majadiliano na uchanganuzi wa hati (*document analysis*).

### 3.3.1 Mahojiano

Niliwahoji wasailiwa mbalimbali kama walivyopangwa katika sehemu ya 3.1 (Eneo la Utafiti). Mtafiti alitumia hojaji zilizosheheni maswali yaliyomwongoza katika kuwasaili watafitiwa na kunakili majibu waliyoyatoa.

### 3.3.2 Utazamaji nyanjani

Katika mbinu hii, habari zilikusanywa kupitia utazamaji wa mtafiti wa moja kwa moja badala ya kuuliza wasailiwa maswali. Aina ya utazamaji niliotumia ni utazamaji wa kutoshiriki. Nilihudhuria vikao ukumbini mwa kundi la klabu cha uigizaji wa masuala la VVU/UKIMWI, kwa kutumia kinasa sauti nilirekodi vipindi/maigizo ya klabu cha uigizaji wa masuala ya VVUUKIMWI. Matukio yaliyorekodiwa

yalinakiliwa kimaandishi na kuambatishwa kama sehemu ya data iliyochambuliwa na mtafiti.

### 3.3.3 Kundi Lengwa la Majadiliano

Mbinu hii ilikuwa na idadi ya wasailiwa kati ya 5 na 10 wakiwa chini ya wasaidizi wa mtafiti. Wasailiwa katika kila kundi walipewa uhuru wa kutoa maoni yao kuhusu mada mahususi zilizojenga msingi wa utafiti huu. Watafitiwa walihojiwa katika kundi dogo la wanafunzi takribani sita kila mara nilipotumia mbinu hii. Kwa mfano mtafiti alikuwa na makundi matatu yaani: kundi la vijana wa kiume pekee, lingine la vijana wa kike pekee, njia hii ilifaa kwa sababu vijana wa kike huona aibu kuzungumzia masuala ya VVU/UKIMWI kama ngono wanaume au vijana wavulana wakiwepo. Kundi la tatu lilijumuisha mseto wa wasichana na wavulana. Hii ni kwa sababu kuna wavulana/wasichana ambao hawakuona uzito kuyazungumza masuala haya mbele ya wenzao wa jinsia tofauti.

Mbinu ya kundi lengwa la majadiliano ilikuwa ya manufaa katika utafiti wangu kama ifuatavyo: Ilinisaidia kupata/kukusanya aina za sitiari na tasfida katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika kutoka kwa makundi niliyoyapendekeza. Vilevile iliwezesha kukusanya habari nyingi zilizotolewa kwa hiari katika kipindi kifupi na kwa gharama nafuu. Pia ilikuwa rahisi kupanua kiwango cha usampuli katika ripoti kwa kuwasaili watafitiwa kadhaa mara moja.

### 3.4 Vifaa vya Ukusanyaji Data

Nilitumia vifaa anuwai katika kukusanya data ya utafiti huu. Vifaa hivyo ni pamoja na:

#### 3.4.1 Hojaji

Utafiti huu ulitumia mwongozo wa hojaji, ambao ulikuwa na maswali wazi na funge ambayo yalimwongoza mtafiti katika kuwasaili watafitiwa kisha kunakili majibu.

#### 3.4.2 Kinasa sauti

Kifaa kingine ambacho nilikitumia ni kinasa sauti cha aina ya SDHC CARD. Hiki ni kinasa sauti chenye uwezo wa kunasa mazungumzo katika umbali wa takribani mita ishirini. Kinasa sauti hiki, kiliweza kunasa mazungumzo yote yaliyojiri katika maingiliano yaliyolengwa, kisha kuchanganuliwa baadaye.

### 3.5 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data ya utafiti huu uliongozwa na malengo mahususi, ambapo vifungu mbalimbali vya data zilizokusanywa kutoka nyanjani kuhusu, sitiari na tasfida zilichanganuliwa kwa kurejelea Nadharia ya Umaanisho ya Paul Grice (1978, 1975) na nadharia ya Mawasiliano ya Kiutambulisho ya Giles (1972 & 1982). Kwa hiyo, tulinakili sitiari na tasfida kutokana na wasailiwa. Kisha, mtafiti alinakili mazungumzo kutoka kwenye kanda za kunasa sauti. Hapa, nilitumia vipokea sauti vya masikio katika kusikiliza na kunakili mazungumzo yote niliyoyarekodi. Kwa njia hii niliweza kuhamisha mazungumzo kutoka maumbo ya sauti kwenye kanda ndogo za kunasia sauti hadi kwenye maandishi. Data hii pia ilichambuliwa ili kuonyesha aina za sitiari na tasfida zilizotumiwa na wanafunzi wakitagusana na kuingiliana kila siku, hasa kuhusiana na masuala mbalimbali yaliyojiri, miongoni mwayo, yakiwa masuala ya VVU na UKIMWI. Hatua ya mwisho katika uchanganuzi huu, ilikuwa

kuainisha sitiari na tasfida katika makundi kulingana na masuala mahsusi yaliyofuatiliwa na mtafiti, mathalan: UKIMWI, ngono, waathiriwa wa janga la UKIMWI, kondomu, sehemu za siri za mwili za mwanamke na mwanamume kisha kuzitolea uchanganuzi wa kimaelezo kulingana na malengo ya utafiti huu.

Vilevile, katika uchanganuzi wa data, mtafiti aliongozwa na Nadharia ya Umaanisho ya Paul Grice (1978, 1975) na nadharia ya Mawasiliano ya Kiutambulisho ya Giles (1972 & 1982), ambapo kunatokea haja ya kutumia tamathali zenye kuficha makali. Kulingana na Grice (1975, 1978), watumiaji wa lugha katika mawasiliano hufahamu kauli tofauti ambazo hazihusiani katika diskosi na kuzifasiri kama zilivyokusudiwa. Aidha, anadai kuwa msikilizaji huwa na uwezo wa kufasiri na kuratibu ujumbe wa kiisimu na usio wa kiisimu katika ufahamu wake. Tukitumia msingi wa nadharia hii, tuliweza kuchambua data huku tukionyesha jinsi watafitiwa waliweza kuhamisha kauli tofautitofauti kutoka maana msingi hadi muktadha wa maana pokezi na hivyo kudokeza hoja au azma yao.

Kwa mujibu wa Giles (1972, 1982), nadharia hii inarejelea dhana ya utambulisho kama kigezo maalumu kinachotumiwa kumtambulisha mtu, kundi la watu, jamii au taifa fulani. Nao Giles na wenzake (2005), wanasema kuwa nadharia ya Mawasiliano ya Usemi ilinuia kueleza hali inayosababisha mabadiliko katika usemaji kwenye maingiliano ya wanajamii. Nadharia hii ilitufaa katika utafiti huu, kwani ilituwezesha kuchambua vifungu mbalimbali vya data kuhusiana na ukuzaji wa mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi kuhusu VVU/UKIMWI. Tukirejelea nadharia hii tunajenga kauli kwamba wasailiwa hawa wanajitambulisha kama wanafunzi ambao wamo katika mazingira mamoja na wana tajriba zinazokaribiana. Wasailiwa hawa hupata nafasi ya kutagusana, kukurubiana na

kuingiliana kwa wepesi katika muktadha unaoruhusu matumizi ya tasfida, sitiari na tamathali zingine za lugha. Ni katika muktadha wa maingiliano kati na baina ya vijana ambapo tasfida na sitiari hutumiwa kwa wingi katika jamii zenye kuzingatia miiko inayokashifu matumizi ya lugha wazi au bayana wakati wa kuzungumza mambo ya UKIMWI na masuala husika.

### 3.6 Masuala ya Etikeli

Data ilitumiwa kulingana na mahitaji ya utafiti ambao uliongozwa na malengo maalumu. Katika utafiti huu, wasailiwa walitaka kujua, kwa nini mtu atake kutafitia maneno ambayo ni mwiko kuyazungumza hadharani katika jamii za Kiafrika na hasa yanayohusu ngono, VVU/UKIMWI na masuala husika. Jambo hili lilizua shaka lakini mtafiti aliwahakikishia watafitiwa kwamba hamna taarifa zozote ama kwenye data au katika uchambuzi wa kimaelezo ambazo kwa namna yoyote, zingewatambulisha walioshiriki kama wasailiwa. Niliwaeleza kwamba masuala haya ni sehemu ya utafiti katika tawi la isimu. Niliwahakikishia kwamba maelezo watakoyonipa yatanifaa na yatahifadhiwa kwa siri. Majina ya wasailiwa/watafitiwa yalibanwa. Hii ndiyo sababu kuwa katika hojaji zangu hakuna sehemu ambayo wasailiwa walihitajika kuandika majina yao.

### 3.7 Changamoto za Utafiti

Japo mtafiti aliukamilisha utafiti huu, si kwamba haukukumbwa na changamoto. Utafiti ulikumbwa na changamoto kadhaa, hata hivyo mtafiti alijikaza ili kuhakikisha kwamba ameukamilisha. Utafiti huu ulihusu VVU/UKIMWI na masuala husika, jambo ambalo lilizua shaka na watafitiwa wengi waliona aya kujibu maswali na kufikia hata kuziacha nafasi katika hojaji. Jambo hili lilinivunja moyo sana, lakini nilijitahidi pamoja na wasaidizi wangu hadi tamati na kukusanya data za kutosha.

Maumbo ya kisitiari au tasfida ni mengi mno, hasa ikizingatiwa kuwa tulijihusisha na wanafunzi ambao huzibuni kila siku kutegemea miktadha ya matumizi. Wakati mwingine tulipata changamoto wakati wa kuziteua zile ambazo zilichukuliwa kuwa mwafaka kwa minajili ya utafiti huu. Kwa hivyo wakati mwingi ulitumika katika kukamilisha shughuli hii ya uteuzi wa sampuli iliyotumika katika uchunguzi. Licha ya changamoto hii, mtafiti alifanikiwa kufukua habari muhimu zilizotumika katika utafiti wake.

### 3.8 Hitimisho

Sura hii inahusu mbinu zilizotumika katika mchakato wa kukusanya data nyanjani kwa ajili ya kuyafikia na kuyatimiza malengo ya utafiti huu. Katika sehemu hii mtafiti amefafanua sehemu zifuatazo: eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanya data, vifaa vya utafiti na uchanganuzi wa data.

# SURA YA NNE

# MATUMIZI YA SITIARI KATIKA MAWASILIANO YA VVU/UKIMWI MIONGONI MWA WANAFUNZI WA CHUO KIKUU CHA MOI

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii nimejadili dhana tamathali za usemi kwa minajili ya kuleta kwa uwazi dhana sitiari na aina za sitiari zilizokusanywa. Vilevile nimejadili dhana ya mawasiliano kwa sababu ndipo sitiari hutumika. Kisha nilifafanua sitiari katika hali ya kilinganishi na kilinganishwa katika msingi wa sitiari zilizokusanywa.

## 4.1 Dhana ya Sitiari

Mulokozi na Kahigi (1979) wanasema kwamba, sitiari ni tamathali ambayo athari yake hutegemea uhamishaji wa maana na hisi kutoka katika kitu au dhana moja hadi nyingine. Vitu hivyo viwili vyenye kuhusishwa kwa kawaida huwa havina uhusiano wa moja kwa moja. Naye Wamitila (2003) anasema, sitiari ni tamathali ya semi ielezayo sifa za kitu fulani kwa kutaja kingine. Anaendelea kufafanua kuwa, sitiari huhusisha vitu viwili ambavyo ni tofauti kitabia na kimaumbile. Pia, Wamitila (2008), anadai kwamba sitiari ni tamathali ya ulinganishi wa bila ya kutumiwa maneno yanayoashiria ulinganishi kama *ja*, *mfano wa* na *mithili ya.*

Dhana ya sitiari inatawala si tu mazungumzo bali maandishi kwa kiasi kwamba inafaa kuchunguzwa pekee badala ya kuwekwa pamoja na tamathali nyinginezo. Msingi wa sitiari ni uhamishaji wa maana. Kwa mfano, tunaposema kuwa, ‘ujana ni moshi,’ pana uhamishaji wa maana (ujana kupewa sifa ya moshi). Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo kwayo kitu, matendo au vitu vyenye hulka na sura mbalimbali hulinganishwa na hali sawasawa na maumbile au jinsi ya utendaji. Maneno ‘kama,’ ‘kwa mfano’ na

'kama vile' hayatumiki. Kuhenga (1977), anasema kuwa, sitiari ni dhana inayotokana na neno 'sitiri,' lenye maana ya kuficha au kufunika.

Wamitila (2003), anafafanua sitiari kama dhana inayoeleza sifa za kitu fulani kwa kukilinganisha na kingine. Yaani kuhamisha maana kutoka muktadha mmoja hadi mwingine bila matumizi ya vilinganishi. Kwa mfano unaposema kwamba, yule ana mdudu, kauli hii ina maana kuwa mwashiriwa ana virusi vya UKIMWI. Ulinganishi huu wa kiubunifu huweka msisitizo katika kile kinachosemwa. Katika kuelewa kauli hii, msemaji huyabana maneno mengi na badala yake kutumia neno moja ambalo msikilizaji wake atalipanua kwa kutumia maelezo faafu ili kufikia maana iliyokusudiwa, kwamba mwashiriwa ana virusi vya UKIMWI. Hali hii imefananishwa na mdudu ambaye kwa kawaida tunajua ni kiumbe mdogo anayeruka au kutambaa ambaye huharibu mimea shambani, jinsi hali ya VVU/UKIMWI inavyosababisha ukosefu wa kinga katika mwili wa mtu.

Uchunguzi wa sitiari hauwezi kukamilika bila ya kuchunguza dhana tatu muhimu ambazo ni nguzo katika kutofautisha dhana mbili kuu: Kilinganishi (ni kile kinachotumiwa kama msingi wa kufananisha), kilinganishwa (ni dhana inayofananishwa) na msingi **(**ni ile sifa yenyewe ya ulinganishi). Gottsched katika Radman (1995), anasema kwamba katika karne ya kumi na nane, sitiari ilichukuliwa kumaanisha matumizi ya neno moja lenye sifa linganishi ili kuwakilisha kitu, hali au dhana nyingine katika hali ya kawaida. Wanaumbuji katika enzi ya mwamko walidhani kuwa sitiari ilikuwa na maana mbili: maana ya nje, na ambayo hupatikana katika matumizi ya kawaida ya lugha; na maana fiche, ambayo hujitokeza katika tamathali. Kwa mfano, katika data tulizokusanya neno sufuria lilitumika kumaanisha

sehemu za siri za mwanamke. Maelezo hayo ndiyo ya maana ya ndani ya sitiari. Maana ya nje ya sitiari ni maana ya kawaida (maana isimu) ya neno sufuria.

Kwa mujibu wa Mazrui (1992), mbinu ya sitiari inafanana sana na ile ya tashibiha (ni yale maneno yanayofananisha au yanayoshabihisha kitu au kitendo kimoja na kingine mfano anafanya kazi kipunda) kwani zote zinashabihisha sifa ya kitu kimoja na kingine. Tofauti iliyopo ni kwamba katika tashibiha, yale mambo mawili yanayoshabihishwa hutokezwa waziwazi, moja likawekwa kando ya lenziwe, katika sitiari mambo yenyewe huunganishwa na kuwa dhana moja. Hivyo basi, sitiari ni tamathali ya semi ambayo ni sawa na tashibiha lakini hulinganisha vitu ama watu lakini bila kutumia viunganishi linganishi vya mithili ya, sawa na, kama na kama vile. Hivyo, katika tamathali hii vitu au watu hulinganishwa na vitu au watu wengine kana kwamba vitu na watu ni sawa kabisa, au hali na hali ni sawa.

Robert (1970) alisema kwamba sitiari ni matumizi ya maneno yaliyo potovu. Richards (1965) kwa upande wake alisema kwamba sitiari ni ufafanuzi wa jambo fulani kwa kutumia yaliyomo katika jambo hilo. Aliongezea kwamba ni kulinganisha vitu viwili bila kutumia neno ‘kama’ kwa mfano dunia ni jukwaa. Ufafanuzi huu wa Richards ni dhahiri kuliko wa wataalamu wengine hapo juu kwani unaonyesha mlingano na fafanuzi nyingine zinazozungumzia kuhamisha maana kutoka muktadha mmoja hadi mwingine. Uhamishaji wa maana unatokana na uwezo wa msemaji wa kulinganisha mambo tofautitofauti maishani. Aidha, sitiari ni matumizi ya neno au kirai, kimawazo, na kutoa wasifu wa kitu au mtu fulani kama kitu kingine ili kuonyesha kwamba vyote vina sifa sawa; na kufanya ufafanuzi kuwa thabiti zaidi. Kwa mfano, matumizi ya neno ‘jiwe’ katika sentensi: “Ana moyo wa jiwe.” Hii inamaanisha kwamba mtu fulani ana moyo mgumu sana.

Mwanaisimu Walpole (1941), naye alichangia maana ya dokezo za sitiari kwa kuunda nadharia ya Uhamishaji Maana yenye msingi wa sitiari. Kwake, sitiari ni ni hali ya kuazima jina la kitu kingine. Kwamba, sitiari ni kipengele cha kila lugha na kwa hivyo matumizi ya sitiari yalianza na chanzo cha lugha au matumizi ya maneno katika lugha yoyote. Maigizo ya sitiari ni jambo la zamani za kale tangu chanzo cha maisha ya binadamu. Alisema kwamba kutoka chanzo cha dunia wanadamu wa kila mbari walitambua umuhimu wa kutumia kumbukumbu zao kuhusu kitu fulani kutafakari kitu kingine kwa njia ya kuvimithilisha. Kutokana na jambo hilo, Walpole (1941) aliunda nadharia ya Uhamishaji Maana yenye kanuni ifuatayo: Katika msemo wenye sitiari, ishara hurushwa kutoka muktadha mmoja kwenda mwingine ulio tofauti kabisa lakini katika msingi wa kumithilisha vipengele vilivyomo katika miktadha hiyo miwili.

Kwa mujibu wa Aristotle, tamathali ya sitiari imekuwepo kwa muda mrefu zaidi. Inaaminika kuwa sitiari ni sifa na tukio la lugha; hivyo basi dhana hii imekuwa ikitokea katika mazungumzo ya binadamu tangu zamani, anafasiri sitiari kuwa uhamisho wa neno geni. Mwelekeo huu wa Aristotle ndio uliofanya sitiari kuonekana kuwa sifa ya lugha na siyo ya fikra.

Kwa mujibu wa maoni ya Giambatsta (1968), uundaji wa sitiari ni kipawa azaliwacho nacho mtumiaji wa lugha na ni ishara ya hekima. Naye Radman (1995), anasema kuwa, sitiari ni matumizi ya neno moja lenye sifa linganishi ili kuwakilisha kitu, hali au dhana nyingine katika hali ya kawaida. Anadai kuwa sitiari ni mbinu ya kutoa maelezo ambayo yalikusudiwa wale ambao hawangeweza kuelewa maana ya msemo moja kwa moja kupitia mantiki.

Whalley (1953), anaifafanua sitiari kuwa mbinu ambamo hisia zinaweza kufinyangwa bila kupoteza uwazi wa maana yake. Hivyo, Whalley aliiona sitiari kuwa mbinu ya kimsingi ya kupitishia hisia katika lugha. Kwa upande wao Deutsch (1958) na Peet na Robinson (1972) wanaieleza sitiari kama lugha inayoashiria uhusiano baina ya vitu viwili na ambapo mfanano ndiyo sifa yake kuu.

Sewell (1964) anaeleza kuwa sitiari ni mojawapo ya nguvu za kimsingi na muhimu sana katika fikra za binadamu. Anaendelea kufafanua kuwa ni uwezo ufanikiwao pale ambapo ufahamu alio nao mtu huchuja na kuoanisha vitu vinavyohusika, vinavyobuniwa na vinavyobwiwa. Kwa maneno mengine, sitiari ni upanuzi wa maana ya maneno bila kuongeza maneno (Wheeler, 1966). Wheeler anasema kwamba asili ya neno la Kiingereza "metaphor" ni neno la Kigiriki lenye maana ya uhamisho. Anaeleza kuwa uhamisho hutokea katika sitiari na huwa kimuktadha kutegemea neno linalotumika pamoja na mazingira ya matumizi. Hii ndiyo maana, Butler na Fowler (1971) wanasema kuwa sitiari ni ubadilisho wa neno kutoka katika matumizi ya lugha halisi na ya kawaida hadi kwenye matumizi yasiyo ya kawaida.

Shibles (1972), anasema kuwa sitiari ni tashbiha iliyobanwa na kufinyangwa. Dhana ya sitiari hutumika kuashiria uhamisho wa sifa kutoka hali moja hadi nyingine. Wheeler (1966), anadai kuwa sitiari ni tamathali ambayo ina maana ya uhamisho. Anazidi kueleza kuwa uhamisho utokeao katika sitiari ni wa kimuktadha kutegemea neno lililotumika pamoja na mazingira ya matumizi.

Kwa mujibu wa Shibles (keshatajwa), sitiari ni tashbiha iliyobanwa na kufinyangwa. Matumizi haya ya lugha hutokea katika taaluma nyingi, kama vile taaluma ya lugha. Katika lugha Shibles anasema kuwa, dhana ya sitiari hutumika kuashiria uhamisho wa sifa kutoka hali moja hadi nyingine. Anaendelea kusema kuwa hakuna maana moja

ya dhana ya sitiari. Kwa mujibu wa maoni yake, maana ya sitiari iliibuka zamani wakati wa Aristotle na tangu wakati huo dhana hii imekuwa ikikua na kubadilika.

Hawkes (1972), anaona sitiari kama uziada katika lugha. Sifa hii huhusu jamii, wakati na muktadha kwani vipengele hivi vyote hubadilikabadilika. Hivyo basi, sitiari kama kipengele kinachotumika katika mawasiliano hakina budi kubadilika. Kutokana na maelezo haya basi kwake Hawkes, sitiari ni zao la hisia za jamii ya lugha fulani.

Gibbe (1978), anaieleza sitiari kama tamathali ambayo hulinganisha vitu viwili. Ulinganishi huu husemwa kwa kudokezwa tu. Anaendelea kusema kwamba vitu vinavyohusishwa kwa kawaida huwa havina uhusiano wa moja kwa moja. Ortony (1979), anasema kuwa sitiari ni mbano wa lugha ya uhusisho wa fikra, picha au ishara ili kuleta uwazi, uchangamano, au undani wa ulinganisho huo husika. Ubunifu wa sitiari huzifanya kuvutia na hivyo kuwa kama aina kuu ya tamathali za lugha.

## 4.2 Matumizi ya Sitiari ya Ngono Miongoni mwa Wanafunzi

Katika sehemu hii nimeangazia namna ambavyo wanafunzi wa vyuo vikuu hutumia kipengele cha lugha sitiari inayohusiana na ngono. Sehemu hii basi imegawika katika vijisehemu vifuatavyo: ngono, uuke, uume, VVU/UKUMWI, kondomu na muathiriwa wa ugonjwa wa UKIMWI.

### 4.2.1 Msamiati wa kurejelea ngono

1. *Mkutano*

Kwa kawaida, mkutano ni wakati ambapo watu huja pamoja kwa sababu fulani kutegemea makubaliano au ajenda yao. Kutokana na utafiti wetu, neno hili mkutano limetumiwa na vijana wakirejelea tendo la ngono katika muktadha wa mawasiliano yao. Wanadai kwamba ili waweze kukutana kwa shughuli hiyo lazima kuwe na

makubaliano kati yao, yaani msichana na mvulana hivyo basi kurejelea suala la ngono kama mkutano ni sahihi.

Wanasema kwamba kutumia neno mkutano kuwasiliana bila yeyote ambaye si wa umri wao kujua kile wanachokimaanisha ila kundi lengwa tu. Hivyo basi sitiari kama hii huwawezesha kujadili masuala ya VVU/UKIMWI na ngono bila tatizo au kuona aya kama vile wangetumia maneno bayana yanayorejelea masuala ya ngono katika hali ya kawaida, jambo ambalo ni mwiko katika jamii ya Afrika. Pia ilibainika kuwa dhana hii imeonyesha jinsi lugha ilivyo hai au wingi wa manufaa kwani neno laweza kupata maana tofauti linapotumiwa katika muktadha tumizi ambao si halisi.

2. *Lima*

Maana ya kimsingi ya dhana lima, huchukuliwa kama kitendo cha kuchukua jembe na kuanza kuondoa magugu shambani. Kutokana na utafiti huu kitendo hiki kimetumika kurejelea tendo la ngono. Vifaa ambavyo hutumika katika shughuli ya kulima navyo ni: jembe, panga na mti. Vijana wamevifananisha vifaa hivi na sehemu za siri za mwanamume na shamba sehemu za siri za mwanamke. Tendo la kufanya ngono wamelifananisha kama kuondoa kwekwe 'shambani.' Nilitaka kujua kwa nini walitumia dhana zile kurejelea tendo lile. Majibu yao yalitolewa ifuatavyo: Sehemu zao za siri zina makali kama ya vifaa hivi na ndiyo sababu huweza kuyaondoa magugu katika mashamba tofautitofauti.

Kutokana na maelezo haya, inabainika wazi kwamba jamii za Afrika huwachukulia wanaume kama viumbe wenye nguvu, makali na watendaji na wanawake kama wapokezi wa athari. Kulingana na vijana, kitendo lima, ni kitendo ambacho huhitaji nguvu na silaha mbalimbali ambazo mkulima huzihitaji shambani. Hivyo basi vijana

wamechukulia kitenzi ***lima*** kama tendo la ngono, kwa sababu ni tendo ambalo huhitaji nguvu na washiriki huhitaji silaha kama vile kondomu.

Vijana waliongezea kwa kusema kuwa, dhana lima (sitiari) imewawezesha kuwasiliana au kuzungumzia masuala ya ngono na VVU/UKIMWI bila kumkera yeyote au kuvunja kanuni za mila na desturi za jamii za Afrika.

3. *Kuuma*

Kimsingi neno kuuma linaashiria tendo la kukata kitu kwa kutumia meno. Vijana walisikika wakisema kwamba; *"bana hii kitu unauma poleepole na kutafuna bila pupa, bora ni kitu safi."* Sehemu za siri za mwanamume zimelinganishwa na meno na tendo la ngono ni kuuma. Katika muktadha huu, sehemu za mwanamke zimefananishwa na chakula au kitu chochote cha kuumwa na kutafunwa au kulika vilevile, na kwamba cha kulika ni lazima kiwe safi kulingana na watafitiwa.

Kulingana na watafitiwa, mwanamume akifanya tendo la ngono na mwanamke, kuna athari mbalimbali ambazo hutokana na tendo hilo. Athari hizo ndizo zimesababisha sehemu za siri za nwanamume kuitwa meno na sehemu za kike kuitwa chakula. Wasailiwa walichukulia kwamba hakuna kitendo cha ngono ambacho hakina madhara kama kuchipuka, kuchukua mimba au kuambukizwa na magonjwa ya zinaa, ndiposa wakasisitiza kwamba chochote cha kulika lazima kiwe kisafi.

Kwa maoni ya wasailiwa, wanapotumia neno hili wakati wanapanga kukutana (wapenzi) hakuna atakayeelewa mazungumzo yao isipokuwa wao wenyewe, jambo ambalo limewaondolea aibu katika maongezi yao ya kila siku na kuhifadhi siri zao vilevile. Sitiari hii ilibainisha wazi mtazamo wa jamii kwa binadamu wa kike na ule wa binadamu wa kiume katika jamii. Kwamba binadamu wa kike ni wa kulika na

usafi wake unachunguzwa dhana ambayo haikudhihirika kwa binadamu wa jinsia ya kiume.

4. *Tafuna*

Maana ya kimsingi ya kitenzi, tafuna ni kitendo cha kusaga chakula au kitu fulani kwa kutumia meno. Kwa maoni ya wasailiwa, kitendo hiki cha kutafuna wamekitumia kurejelea kitendo cha ngono, kwa sababu wakati wanapofanya mapenzi kuna kile kitendo cha kusaga ili kutoa utamu.

Kutokana na istilahi hii iliyotumiwa na vijana kurejelea ngono, ilibainika kwamba jamii za Afrika zimempa mwanamume nguvu na kumdunisha mwanamke. Mwanamke amechukuliwa kama kitu cha kutumika tu ili kumpa starehe au raha mwanamume. Haya yanadhihirika katika ile hali ya kutafunwa na kitafunwacho lazima kiwe kisafi na kiwe na ladha na mume amerejelewa kama mmliki na mtendewa katika muktadha huu na mke ni kitendwa yaani anayepokea athari.

Kutokana maelezo haya, ilibainika kuwa matumizi ya kitenzi tafuna yameweza kuficha siri na kuondoa aibu vijana wanapozungumzia masuala ya ngono na VVU/UKIMWI bila kumshutumu yeyote, na hivyo basi kurahisisha mawasiliano miongoni mwao. Vile vile dhana za umilisi na utendaji zilidhihirika kwa watafitiwa jambo liloashiria uelewa wao wa lugha na ubunifu wao wa hali ya juu, kwamba waliweza kuhamisha neno kutoka muktadha mmoja hadi mwingine na likawakilisha maana jipya kulingana na matakwa yao.

5. *Mombasa raha*

Mombasa ni mji upatikanao katika nchi ya Kenya. Katika mji huu kuna mandhari ya kupendeza labda sababu ya bahari na sehemu zingine za kufurahisha ambazo watalii hutembelea kwa minajili ya kufurahisha macho yao na nyoyo zao.

Hivyo basi kutokana na starehe zote watalii na wenyeji wazipatao Mombasa zimesababisha mjini huo kutumiwa kurejelea tendo la ngono. Wasailiwa walitumia msemo unaopendwa kutumiwa unaosema kwamba, ***'Mombasa kwenda raha kurudi matata.'*** Walieleza kuwa wanapojamiana wao husikia raha ambayo mara nyingi huwawia vigumu kuachana na mpenzi wake hata wakati mwingine wao hushindwa kuenda masomo kama mpenzi wake yuko chumbani. Hali hii ilisababisha kurejelea ngono kama Mombasa raha kwani walidai kuwa ni jambo ambalo huwaletea matata baadaye kama ndoa za mapema, mimba za mapema, magonjwa ya zinaa, VVU/UKIMWI na mauaji wakati mwingine. Hivyo basi, wasailiwa wanadai kwamba sitiari hii huwasaidia kuwasiliana kwa urahisi bila kutia yeyote aibu, kwa sababu ni mwiko jamii za Kiafrika kutaja tendo la ngono au masuala yahusikao na ngono bayana. Vilevile kuonyesha umahiri wao wa kutumia lugha, yaani unaowawezesha kuhamisha neno kutoka muktadha asilia hadi muktadha pokezi na kupata maana jipya (kusudiwa).

6. *Bao*

Dhana ya bao kimsingi ni kule kushinda timu nyingine kwa kuifunga bao wakati wa kucheza kandanda. Hivyo basi, kule kufunga bao katika muktadha huu kumetumika ili kurejelea tendo la ngono. Katika uchambuzi wa kina, inabainika kwamba, mchezo wa ngono umelinganishwa na mchezo wa kandanda uwanjani. Kulingana na watafitiwa timu A ni mwanamume na timu B ni mwanamke, ambapo kilele cha tendo la ngono huwa ni kufunga bao. Shughuli zingine zote katika ile harakati ni kucheza kandanda.

Wasailiwa walirejelea neno hili kuwa sitiari, kwa sababu huweza kuficha siri na kero katika jamii ikiwa wangetumia neno bayana. Jambo hili liliwawezesha wasailiwa

kuwasiliana bila kuwachukiza wenzao. Sitiari hii iliweza kufafanua hisia na maoni ya wasemaji kuhusu jambo wanalolizungumzia. Watafitiwa walisema kuwa kufunga bao kunaweza kuleta madhara mbalimbali: mimba, magonjwa ya zinaa na mauaji. Baadhi ya matukio haya huonekana pale ambapo timu nyingine imefungwa au imeshindwa kwa mfano kupigana kwa kutumia mawe.

7. *Mpigo*

Maana ya kimsingi ya dhana ya mpigo ni namna ya upigaji wa kitu kwa kutumia kitwangio. Wasailiwa wametumia istilahi hii kurejelea ngono kwa sababu ya mchakato katika shughuli zote za ngono. Kulingana na utafiti huu, anayepokea athari ni mwanamke na mtenda ni mwanamume. Hivyo basi ilibainika kwamba jamii imemchukulia kijana wa kiume kuwa mwenye nguvu ikilinganishwa na kijana wa kike. Kufanya ngono kumechukuliwa kama kumwadhibu kijana wa kike. Jambo hili halikuwafurahisha vijana wa kike. Hii ilibainika wakati niliwasaili watafiti wa jinsia ya kike. Kulingana na maoni yao, kutopendezwa na istilahi ibuka kulibainika wazi.

Watafitiwa wa jinsia ya kike walionekana kuwa na maoni tofauti, kulingana na maoni yao ngono ni tendo la kufurahia kwa pande zote, ila kwamba vijana wa kiume walichukulia kitendo hiki kama njia ya kumwadhibu kijana wa kike jambo ambalo lilijitokeza kama kero kwao. Sababu ni kwamba tendo la ngono ni makubaliano katika pande zote. Hata hivyo sitiari hii iliwawezesha kuwasiliana masuala ya VVU/UKIMWI na masuala husika bila kuvunja miiko na mila za jamii nying za Afrika ambapo kuzungumza dhana zenyewe bayana ni tabuu.

8. *Sarakasi*

Kulingana na maelezo kutoka kamusi, sarakasi ni mchezo unaochezwa kwa ustadi mkubwa unaohusisha matumizi ya viungo vya mwili. Wasailiwa walirejelea tendo la

ngono kama sarakasi kutokana na yale watazamayo katika mtandao. Walisema kwamba kuna ustadi mkubwa wa kufanya mapenzi. Sababu yao kuu ya kuashiria tendo la ngono kama sarakasi. Kutokana na sitiari hii tulibaini kwamba kwao vijana kitendo cha ngono ni kitendo ambacho huhitaji ustadi mkubwa na ushirikiano wa hali ya juu kati ya wahusika wawili au zaidi. Kitendo ambacho huchangia upotovu wa maadili katika jamii. Hata hivyo, hii ni mojawapo ya sitiari ambayo wanafunzi wameibua kwa minajili ya kuwasiliana juu ya suala la ngono chanzo kuu ya maambukizi ya VVU/UKIMWI.

Waliendelea kudai kwamba ndio sababu ngono hutekelezwa katika mahali fiche pasipo na furugu yoyote. Haya yalikuwa maelezo ya wanafunzi wa chuo kikuu.

### 4.2.2 Msamiati wa kurejelea uuke

9. *Migingo*

Migingo ni ziwa linalopatikana katika mpaka wa Kenya na Uganda. Ziwa hili lina maji maenge na samaki wengi, hali ambayo imesababisha mgogoro kati ya wananchi wa Kenya na Uganda. Sehemu za siri za mwanamke zimefananishwa na kisiwa cha Migingo kwa sababu ya ‘‘manufaa’’ yake. Katika utafiti huu ilibainika kuwa mwanamke katika jamii ana manufaa mengi, kwamba uuke wake ni chemichemi ya uhai, kama walivyodai wasailiwa. Jamii huongezeka na kutunzwa na wanawake. Hii ndiyo sababu utawapata wanaume wakipigana kwa sababu ya mwanamke ikiwa kuna mwanamume anayetaka kumnyanganya mwanamume mke wake.

Waliendelea kusema kwamba uzuri wa mwanamke ni uuke wake ni kama uzuri wa Migingo. Hivyo basi ikiwa kuna mmoja atakayejaribu kumnyanganya mme mke wake au kijana wa kiume mpenziwe vita vinaweza kuzuka kama vilivyozuka kati ya Kenya na Uganda.

10. *Maua ya maulana*

Maana ya kimsingi ya dhana ya maua ni sehemu ya mmea inayozalisha mbegu yenye kuzungukwa na petali zenye rangi inayompa mtu hali ya afueni baada ya kupata maumivu au janga. Sehemu hii ya mti pia hupendeza, hivyo basi uuke umerejelewa kwa dhana ya maua ambayo yanapendeza wakati yanachanua na humpa mtu 'afueni.'

Watafitiwa walieleza kuwa kuna maumbo mbalimbali ya maua na pia harufu tofauti ambazo zaweza kuwa za kuchukiza au nzuri. Hivyo ndivyo sehemu za uuke zilivyo, kulingana na watafitiwa. Waliendelea kusema kwamba jinsi maua huchanua na kunyauka ndivyo sehemu za uuke za mwanamke hunyauka akijifungua na huchanua baada ya muda.

Hivyo basi, walisema kwamba hizi ndizo sababu kuu za kurejelea maua kuashiria uuke bila ya kutumia neno bayana "***kuma***" ili kuwasiliana bila kukwaza yeyote au kumshutumu yeyote katika jamii. Jambo hili limewarahisishia mazungumzo kuhusu masuala ya ngono na VVU/UKIMWI bila kuwashutumu wahusika katika mazungumzo.

11. *Kapedo*

Kapedo ni sehemu katika nchi ya Kenya ambayo kwa sasa watu hawapendi kusafiri huko kwa sababu ya maafa yaliyotekelezwa huko katika kipindi fulani maalum. Katika mwaka wa 2016 kuna askari polisi waliotumwa Kapedo kurejesha amani miongoni mwa jamii ya Turkana na Pokot ambazo zilikuwa zikizozana.

Kutokana na utafiti huu, ilibainika kwamba vijana wamehamisha maana ya Kapedo kurejelea uuke, kwa sababu wengi huchukulia kwamba wanawake ndio huambukiza wanaume virusi vya UKIMWI. Aidha watafiti wanadai kwamba, wanawake ndio husababisha vifo vingi, kwa mfano wanaume huuana kwa sababu ya wanawake na

vilevile wanawake huuana kwa sababu ya wao wenyewe. Hata hivyo ubunifu huu umewawezesha kuwasiliana kuhusu masuala ya ngono hali ambayo imesababisha kuthibiti hali hii ya VVU/UKIMWI.

12. *Sufuria*

Hiki ni chombo kinachotumiwa jikoni katika upishi wa chakula au hutumika kuchota maji. Kulingana na watafitiwa umuhimu na umbo la sufuria ndilo lilosababisha kurejelea sehemu za uuke sufuria.

Ilibainika kwamba, sehemu za mwanamke zimelinganishwa na sufuria kwa sababu mwanamke huchukua mimba, hutunza na kujifungua baada ya muda fulani. Vilevile wasailiwa wa kiume walidai kuwa umbo la uuke ni kama sufuria.

Wasailiwa wa kike walidai kuwa kutumia sitiari kama hii, huwachukulia kama chombo cha kutumika tu, ingawa hurahisisha mawasiliano na kuficha maneno ambayo ni mwiko yanapotamkwa bayana.

13. *Shamba*

Kimsingi, neno shamba ni kipande cha ardhi ambapo watu hulima, hupanda, hupalilia na kuvuna, hivyo basi shughuli zinazotekelezwa huko zimesababisha vijana kutumia neno hili kurejelea uuke au dhima za wanawake katika jamii. Kwamba kitendo cha ngono ni kulima au kupalilia na mtu akichukua mimba ni kama kupandwa kwa shamba na kuota mimea.

Shughuli zinazoendeshwa mle shambani zimelinganishwa na shughuli ambazo hufanyika katika sehemu za siri za kike. Kwa mfano data iliyochanganuliwa katika sehemu ya ngono ilibainika kwamba kufanya ngono kulilinganishwa na *kulima* (tazama mf 2 pale juu) na mahali pa kulimwa ni sehemu za siri za kike ambazo

zimerejelewa kama shamba. Kutokana na sitiari hii ilibainika kwamba wanawake huchukuliwa kama wapokeaji wa tendo na wanaume kama watendaji. Vile shamba linavyomsubiri mwenyewe alime ndivyo ilivyo katika sehemu za mwanamke.

Shughuli za kuvuna zililinganishwa na wakati wa kujifungua kwa mwanamke. Wasailiwa walisikika wakisema kwamba, '*mtu ni kulima shamba kwelikweli, kupanda na kupalilia."* Watafiti tulishangazwa na vijana juu ya unongonishaji wao wa misamiati katika miktadha tofautitofauti. Kwani waliweza kuhamisha misamiati kutoka mandhari asilia hadi mandhari pokezi na kuzalisha maana waliokusudia.

14. *Chakula*

Dhana hii kimsingi inarejelea kitu chochote ambacho mimea hufyonza kwa minajili ya kuota na kukua ili kuendeleza maisha na ukuaji. Chakula pia ni muhimu katika uhai wa wanyama na binadamu kwa minajili ya ukuaji. Mtu hula chakula ili atunze afya yake apate nguvu za kufanya kazi katika jamii. Hivyo basi kutokana na utafiti wetu ilibainika kwamba sehemu za siri za mwanamke zimerejelewa na dhana hii. Watafiti tulitaka tujue sababu za vijana kurejelea sehemu ya uuke chakula. Sababu ambazo tulipata ni kwamba katika sehemu hii kuna raha ambayo mhusika hupata na kufurahia na 'kushiba." Kutokana na hali hiyo, mwanamke hupata mimba na kujifungua. Hivyo basi, dhana ya kufanya mapenzi imelinganishwa na kitendo cha kupika na kuandaliwa kwa chakula.

Vijana wamelinganisha chakula na ngono, wakidai kwamba ni tendo ambalo hutuliza mawazo ya mtu hadi akatulia na kushikwa na usingizi, jambo linalotekelezwa na mlo. Walieleza kwamba wakati mwingine sehemu ile huleta maafa, kutokana na magonjwa ya zinaa na hata kifo (mauaji) ikiwa mpenzi ana wapenzi wengi wa kando. Mambo

ambayo hutokea ikiwa chakula cha msingi kinacholiwa hakijaandaliwa kwa njia nzuri, vile vile huweza kuleta madhara kwa afya ya mwanadamu.

Wasailiwa waliongeza kuwa dhana hizi za kisitiari zimewasaidia katika kutekeleza mawasiliano kuhusu ngono, VVU/UKIMWI na masuala husika katika muktadha wa Kiafrika ambapo kutaja mambo kwa majina yake bayana ni mwiko. Maana kusudiwa katika urejeleaji wa dhana ya chakula kuashiria ngono ni kuwa mwanamke anafaa kumakinika katika kumtosheleza mpenziwe katika haki za kimapenzi, jinsi ambavyo wapishi humakinika wakati wa kuandaa chakula kitamu kinacholiwa na kushibisha.

### 4.2.3 Msamiati wa kurejelea uume

15. *Msumeno*

Maana ya kimsingi ya neno hili ni kifaa chenye meno anachotumia seremala kukereza ili kukata mbao au vyuma. Watafitiwa wamelinganisha sehemu za uume na msumeno kwa sababu katika muktadha wa kufanya mapenzi mwanamume hukereza sehemu za siri za mwanamke. Hii ndiyo sababu mwanamke hutokwa na damu ikiwa yu bikira.

Kutokana na utafiti wetu ilibainika wazi kwamba, jamii imewachukulia wanaume kama watu jasiri. Ni kutokana na muktadha huu ambapo uume wao umerejelewa kama msumeno ambao hukata sehemu za uuke na kuuvunja ubikira wao. Tendo lililosababisha kurejelea uume msumeno. Ingawa nyingi za kauli zinazotolewa na watafitiwa ni dhahiri kimaana, baadhi huhitaji urejeleo wa muktadha na tajriba husika ili kung'amua maana kusudiwa. Hali ambayo ilitufafanulia zaidi juu ya umuhimu wa muktadha katika mawasiliano.

16. *Kipofu*

Kipofu ni mtu asiye na uwezo wa kuona. Uume umelinganishwa na kipofu ambaye huweza kutekeleza mambo bila ya kuona ila kwa hisia tu.

Watafitiwa wamerejelea sehemu za uume kipofu kwa sababu sehemu hizo hazina macho lakini huelekezwa na vilevile kutokana na mazoea "hupenyeza njia," na kumaliza hamu ya kimapenzi pindi tu hali hiyo inapochipuka. Mawazo haya yanashadidiwa na maana ya dhana sitiari inayofafanua kuwa dhana moja inayozungumziwa hueleweka zaidi kwa kuifananisha na kulinganisha na dhana nyingine. Sitiari hii hufumba ujumbe waliokusudia kutoa wasemaji hali ambayo huwawezesha kuzungumza masuala ya ngono bila kuvunja maadili ya kijamii.

17. *Mtaimbo*

Kwa mujibu wa muktadha wa kimatumizi, kauli hii japo inaonekana wazi kiujumbe, imefumba ujumbe aliokusudia msemaji kwa walengwa. Maana ya kimsingi ya dhana ya mtaimbo ni ufito mrefu wa chuma. Hurejelea chuma nzito na ngumu inayotumiwa na fundi wa vyuma au wahalifu kuvunjia mahali fulani.

Sehemu ya uume imerejelewa kwa kifaa hiki, kwa sababu ya umbile la uume na vilevile umbo ambalo sehemu hii huchukua wakati mhusika ana ashiki na hamu ya kujamiiana. Wasaili waliendelea kusema kuwa tendo la kujamiiana lisipotekelezwa kwa makubaliano kati ya wahusika huweza kuharibu sehemu za siri za mwanamke.

Vilevile ilibainika kuwa jamii za Kiafrika zimemchukulia mwanamke kama mtu wa kuadhibiwa katika kila muktadha hata wakati wa kujamiiana ni kumwadhibu mwanamke jambo ambalo limesababisha vijana kurejelea sehemu hizi kama mtaimbo. Hata hivyo dhana hii ilidhihirisha umilisi wa lugha na utendaji walio nao vijana wa chuo Kikuu cha Moi.

18. *Mkuki*

Maana ya kauli hii ni silaha ambayo hutumika kwa kumchoma mtu vitani au wakati wa kupambana na adui. Kutokana na maelezo haya mkuki umerejelewa uume kwa

sababu ya umbo la uume wakati wa kujamiiana. Ilibainika kwamba katika ngono kuna lile tendo la ‘‘kuweka na kutoa,’’ tendo ambalo huacha madhara kama ugonjwa na mimba kama yalivyo madhara ya mkuki hudhihirika kwa adui au mnyama. Haya yalisababisha uume kulinganishwa na dhima ya mkuki katika jamii za Kiafrika.

Kutokana na kauli hii na maelezo yake, ilibainika wazi kwamba jamii za Kiafrika zinamthamini mwanamume. Zimempa mtazamo wa umiliki na ulinzi katika jamii. Watafiti waliongezea kwamba uume hutekeleza ulinzi na umiliki katika jamii kwamba wenzao wanapojua kuwa huyu ni mpenzi wa fulani huheshimu hivyo la si hivyo huweza kuleta mgogoro na hata kusababisha vita na mauaji. Kando na maelezo haya ilibainika kwamba kauli hii ya kisitiari imechangia au imerahisisha mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI, ngono na masuala husika bila kutia aibu machoni na masikioni mwa wasikilizaji.

19. *Nyundo*

Katika muktadha wa kawaida, nyundo ni kifaa ambacho hutumika katika kugongelea misumari kwenye mbao, ukuta na mabati. Pia hutumika katika kupasua mawe. Kutokana na utafiti wetu ilibainika kuwa, umbo la kifaa hiki limetumiwa kurejelea uume. Vilevile dhima ya kifaa hiki imetumika kurejelea nafasi ya uume katika masuala ya ngono. Maelezo haya yalibainisha ubunifu walio nao wajua lugha husika, jambo ambalo limewapa uwezo wa kuhamisha dhana kutoka muktadha mmoja hadi mwingine na kulipa maana sawia na maana ya kimsingi ya neno husika.

Ilibainika kwamba matumizi ya kauli hii ni muhimu kwa sababu huficha siri kwa kutumia nyundo ambacho ni kifaa cha kawaida, lakini ambacho kimetumika katika musuala ya ngono kuashiria heshima na upole katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika.

20. *Silaha*

Muktadha wa kauli hii ni kuhusu suala la uhusiano wa kimapenzi, hivyo basi walengwa wa kauli hii wanaweza kutumia tajriba na mazingira yake kung'amua kwa urahisi kusudio la wazungumzaji.

Kimsingi, silaha ni kifaa au zana inayotumika kupigia au kupigania na ambayo ina uwezo wa kudhuru au kuua au kuepusha mtu kutoka kwa madhara fulani. Silaha imefananishwa na sehemu za uume kwa sababu ya dhima zake. Wasailiwa walisema kwamba uume wao ni silaha kwani kunapokuwa na mgogoro wowote kati ya wapendanao wanapojamiiana mgogoro husuluhishwa. Maelezo haya yameshadidiwa na msemo huu ambao wasailiwa walisikika wakisema kwamba, '*afadhali mtu aumie kila mahali lakini silaha ibaki intact bila hii wee ni Kazikwisha.'*

### 4.2.4 Msamiati wa kurejelea VVU/UKIMWI

21. *Ugonjwa wa kigeni*

Hali ya Ukosefu wa Kinga Mwilini, ni hali ya utata kulingana na wasailiwa. Walidai kuwa ni ugonjwa unaohusishwa na mataifa ya ughaibuni kwa sababu hali hii iligunduliwa huko kwanza kabla ya kusambaa katika nchi za Afrika.

Wasailiwa walidai kuwa hali hii si yao na wanaichukia sana, kwa vile 'imewanyima' raha na ni ya kuogofya mno. Hata hivyo, hawapendi kuzungumza kuhusu hali hii waziwazi. Sababu kuu ya wao kurejelea hali hii kwa kauli 'ugonjwa wa kigeni,' ni kutokana na woga wa kifo na maradhi yanayosababishwa na hali hii. Hivyo basi, wasailiwa hutumia sitiari wanapowasiliana kuhusu VVU/UKIMWI ili kuepuka kuwadhuru au kuwashutumu wengine. Jambo hili vilevile limewasaidia vijana kuwasiliana bila tatizo. Pia, limechangia katika kuonya vijana dhidi ya kuiga mitindo hasi kutoka nchi za ughaibuni, hali ambayo huweza kusababisha maambukizi zaidi ya

ugonjwa wa VVU/UKIMWI. Hata hivyo, kauli hii imewawezesha kukamilisha mawasiliano kuhusu ngono na masuala husika katika miktadha tofautitofauti.

22. *Ukedi*

Ukedi, ni ugonjwa unaosababisha vidonda katika ngozi au mwili wa binadamu. Wasaili walidokeza kuwa mtu apoambukizwa virusi vya UKIMWI mwili wake hukosa kinga kwa sababu viini hivyo hushambulia kinga katika mwili wa mwathiriwa, hali ambayo humwacha katika hali hatari ya kupata aina zote za magonjwa katika jamii.

Mtu aliyekumbwa na hali hii ya VVU/UKIMWI huendesha yaani kuhara, hukonda kama sindano kisha hutokwa na vidonda mwilini. Hii ndiyo sababu iliyochangia ugonjwa wa ukedi kutumika katika kurejelea hali ya VVU/UKIMWI. Kauli hii ya kisitiari imeweza kuhifadhi nyuso za wazungumzaji na wasikilizaji na pia zinadhihirisha upole kuliko kutumia neno bayana, hivyo basi kufanikisha mawasiliano ya kupiga vita ugonjwa huu.

23. *Kutokuwa sawa*

Kuwa sawa na kutokuwa sawa ni kauli zilizobainika kutoka kwa mazungumzo ya vijana, katika muktadha wao wa mawasiliano juu ya masuala ya ngono na wakati wanatongozana na wanataka kufanya tendo la ngono bila kutumia kondomu/ kinga. Kauli ya *kuwa sawa* katika mazungumzo ya vijana ni ile hali ambapo wahusika au mhusika hana ugonjwa wa zinaa na kauli ya *kutokuwa sawa* ni ile hali *ya kuwa mgonjwa*. Vijana hutumia kauli hizi kuulizana kama mtu ako sawa yaani amepimwa na akapatikana hana VVU. Hivyo basi, kama hayuko sawa ana VVU/UKIMWI au hali zingine ambazo haziwezi kuruhusu kushiriki tendo la ngono bila kinga.

Kauli hizi zimeweza kuwatambulisha vijana katika jamii na kuwawezesha kuwasiliana bila kumtia mhusika yeyote katika mazingira ya mawasiliano ya aibu kwa sababu ni mwiko kuyazungumzia masuala ya ngono bayana katika jamii za Kiafrika. Vilevile umilisi na ubunifu wa lugha miongoni mwa vijana uliweza kubainika.

24. *Waya*

Maana asilia ya dhana hii, ni kifaa kinachotumiwa katika kupitisha sauti au umeme kutoka sehemu moja hadi nyingine. Kwa kawaida umbo lake ni jembamba. Vijana wamerejelea hali ya VVU/UKIMWI na waya, kwa sababu ya njia ambayo ugonjwa huu husambazwa kutoka kwa mwathirika hadi kwa mhusika aliye sawa.

Hali hii vilevile imerejelewa na waya kwa sababu, mwathiriwa wa hali hii akiwa amezidiwa na ugonjwa huu hukonda mithili ya waya, kwa sababu virusi hivi huangamiza mtu kwa kuua kinga ya mwilini. Mwili hudhoofika na kuishiwa nguvu kama mtu aliyepigwa na umeme. Kwa mfano, katika utafiti huu vijana walisikika wakitaniana hivi: *wee chunga usije ukala waya au tayari unayo mwilini...*

### 4.2.5 Msamiati wa kurejelea kondomu

25. *Mpira*

Maana ya msingi ya leksimu hii ni rasilimali ambayo hutumika kutengeneza mipira. Maana dokezi ni mfuko mdogo wa mpira ambao huvaliwa katika tupu ya kiume au kike wakati wa kushiriki tendo la ngono kwa ajili ya kinga ya mimba au maambukizi ya magonjwa mbalimbali ya zinaa. Ilibainika kuwa sababu kuu ya vijana kurejelea kondomu kwa leksimu mpira ni kutokana na rasilimali za uundaji wa kondomu.

Tulibaini kwamba kauli hii iliyobuniwa na vijana imeweza kuwatambulisha katika kundi fulani la kijamii na vilevile kuwawezesha wahusika kuwasiliana bila kuvunja mila na desturi za jamii husika kwa kutumia dhana ambayo ni ya kawaida.

26. *Ala*

Leksimu *ala*, ni kifaa kilichotengezwa kwa ngozi au kitambaa kigumu au turubai ambacho hutumia kuhifadhia silaha. Vijana walirejelea kondomu kama *ala* kwa sababu kwamba, dhima ambazo kifaa *ala* hutekeleza ni zilezile ambazo kondomu hutekeleza.

Kondomu inafaa 'kuhifadhi' silaha (uume) ili isije ikagusana na nyama au ngozi ya mshiriki wa kike katika tendo la ngono au wote wawili. Hali ambayo huweza kusababisha maambukizi ya VVU/UKIMWI miongoni mwa washiriki. Ilibainika kwamba, dhana hii ilifanikisha mawasiliano baina yao bila kuvunja mila na desturi katika jamii za Afrika..

27. *Uo*

Leksimu uo katika maana msingi ni mfuko ambao hutumika kuhifadhia au kuficha ala za vita kama mishale. Kutokana na dhima hii, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi walirejelea kondomu kama uo, jambo ambalo pia lilirahisisha mazungumzo baina yao. Katika hali hiyo, kuhamisha maana ya dhana moja kutoka muktadha asilia hadi muktadha pokezi na kuweza kuwasilisha maana lengwa ni hali ambayo ilidhihirisha umaarufu na ubunifu wa hali ya juu wa vijana. Aidha, tendo hili limeweza kuwatambulisha katika jamii, kuhifadhi mila na desturi za jamii husika na vilevile kuweza kuwasiliana juu ya VVU/UKIMWI bila kutia aibu hadhira husika na hata jamii kwa jumla.

28. *Kifuniko*

Maana msingi ya dhana ya kifuniko, ni kifaa kinachotumiwa kuziba sehemu ya juu au uwazi uliopo kwenye chombo ili kuhifadhi kilichomo kisiingiwe na uchafu au kumwagika. Kauli hii ilibuniwa kuerejelea kondomu kwa sababu, shughuli za kondomu ni sawia na zile za kifuniko.

Kutokana na utafiti, ilibainika kwamba kauli hii ilirahisisha mawasiliano baina ya wahusika katika jamii na pia ilidhihirisha umaarufu wa vijana wa kutumia lugha katika mawasiliano yao kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika. Mfano wa mazungumzo ya vijana yaliyonakiliwa:

Kijana 1: Msupa niaje,
Kijana 2: Fiti, sema
Kijana 3: Leo, tukawe miradi, *kifuniko* ninacho
Kijana 4: (*akitabasamu kwa aya*)

### 4.2.6 Msamiati wa kurejelea mtu aliye na VVU/UKIMWI

29. *Foksi/paka mapepe*

Maana ya kimsingi ya foksi/paka mapepe, ni mnyama ambaye huchakura mapipani na kula vyakula vilivyooza. Mapepe (pupa) ni kauli inayoashiria tabia ya mtu mlafi. Watafitiwa wana imani kwamba tabia mbaya ya kutaka *'kuchakura'* kila kitu ndiyo humfanya mtu kufanya mapenzi na kila mtu bila kutumia mpira au bila kujua hali ya mtu kabla ya kushiriki ngono naye. Hali ambayo husababisha kuenea kwa ugonjwa huu wa VVU/UKIMWI.

Watafiti walitumia kauli hii kuashiria mwathiriwa, kwa sababu kulingana na tajriba yao na kiwango cha elimu ni mtu tu aliye na pupa ya ngono ambaye huweza kuyatekeleza haya. Walieleza kwamba ni vizuri mtu kujipima na kupima mpenziwe au kutumia kondomu katika tendo la ngono, ili kupunguza maenezi ya ugonjwa huu

au kuepukana kabisa na maswala ya ngono yaani ***'kuchill'*** . Hata hivyo, sitiari hii imewawezesha kuwasiliana kwa urahisi kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika bila kuzua tatizo katika utamaduni wa jamii husika jambo ambalo limechangia katika uhamasisho wa jamii juu ya janga hili.

30. *Teksi bubu/gari kubwa*

Kauli hizi katika maana asilia, ni teksi yaani gari ya kukodisha linaloendeshwa bila kupinga ilmradi dereva yeyote yupo. Gari kubwa, ni gari maalumu aina ya lori ambalo hubeba mizigo sampuli yote na ambazo si chini ya tani tatu.

Watafitiwa walitumia kauli hizi kuashiria tabia za wanajamii wanaofanya mapenzi au kushiriki ngono za kiholela na kila mtu bila hata kujua hali yao ya UKIMWI. Watafitiwa waliwarejelea watu walioathirika kutokana na tabia kama hizo kama teksi bubu kwa sababu wao waliabiri *gari au lori* lolote bila kujali ni la wapi, limewahi kubeba kina nani, wa sampuli gani.

Waliendelea kueleza kwamba, kitendo kama hiki ndicho husababisha maenezi ya ugonjwa huu. Hata hivyo, kauli kama hii imewasaidia katika kukashifu tabia mbaya kama hizi katika jamii. Kitendo ambacho kimechangia kukashifu mienendo mibaya katika jamii husika.

31. *Chokoraa*

Kwa kawaida, leksimu hii humaanisha watu wanaoishi mijini bila makao. Chokoraa hula chochote kutoka kwa mapipa au mahali popote akipatapo. Wasailiwa wametumia neno hili kurejelea mtu aliyeathirika na ugonjwa/hali hii amefananishwa na chokoraa, kwani wasailiwa walidai kuwa mtu aliyeathirika kutokana na tabia za 'kurandaranda' mtaani bila kutumia kinga.

Hivyo basi kutokana na kauli hii, tuligundua kwamba vijana wana mtazamo tofauti katika jamii kwamba mtu anafaa kula mahali pasafi, ambapo anamjua mpishi wa chakula hicho ni nani na wangapi ‘wamepikiwa’ kutoka chungu hichohicho kimoja. Mtazamo huu kuhusu ugonjwa huu kwa kiasi fulani umechangia katika kupunguza maambukizi ya VVU/UKIMWI.

32. *Mama/dada huruma*

Mama au dada huruma, ni watu walio na huruma sana katika jambo lolote. Vijana wamerejelea waathiriwa wa hali ya VVU/UKIMWI kwa kutumia kauli hii, kwa sababu wao huchukuliwa kuwa watu ambao hawezi kusema la katika tendo la ngono kwa yeyote aliye na haja. Tabia kama hizi zimesababisha kupotoka kwa maadili katika jamii.

Kauli hii ilibainisha mtazamo wa vijana kuhusu hali ya VVU/UKIMWI katika jamii kwamba watu wangekuwa na msimamo imara ambao umeongozwa na maadili ya kijamii basi tungeweza kupunguza maambukizi zaidi ya VVU/UKIMWI katika jamii.

**4.3 Hitimisho**

Sura hii imejadili dhana ya sitiari kama kipengele kimojawapo cha lugha ambacho kimetumiwa na watafitiwa katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika. Aidha, tumefafanua uhusiano uliopo kati ya kilinganishi neno (tumizi) na kilinganishwa (sitiari).

# SURA YA TANO

# TASFIDA KATIKA MAWASILIANO YA VVU/UKIMWI MIONGONI MWA WANAFUNZI

## 5.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia tumejadili dhana ya sitiari na mifano ya dhana zilizotumika kiisitiari. Katika sura hii tumefafanua dhana ya tasfida kulingana na yaliyoandikwa kuhusu msamiati wa tasfida. Tumeeleza aina mbalimbali za tasfida kwa kuangalia uainishaji wa tasfida zilizokusanywa na kutoa mifano katika lugha ya Kiswahili. Vilevile katika sura hii tumejadili uhusiano uliopo kati ya kilinganishi na kilinganishwa na sababu za kuhusisha kilinganishi na kilinganishwa katika muktadha wa mawasiliano.

## 5.1 Dhana ya Tasfida

Neno tasfida linatokana na neno la Kigiriki (euphemia), maana yake ikiwa "matumizi ya maneno mazuri," kwa masikio. Dhana ya tasfida imeelezwa na wanaisimu wengi kwa njia tofautitofauti. Kwa mfano, kwa mujibu wa Islam na wenzake (2009), tasfida ni matumizi ya lugha kwa njia ya kuepuka kutaja mambo yanayohusiana na uchafu wa matusi au karaha ya aina fulani.

Lugha huwa haitumiwi kwa njia wazi kutokana na miiko ya jamii inayohitaji baadhi ya mambo kuwekwa siri au kusemwa kiungwana au kiadabu. Watu wa kila jumuiya huwa na tabia ya kutaja mambo yanayofikiriwa hayafai kutajwa hadharani kwa kuyafunika kwa maneno tofauti. Kwa mfano Waswahili hutumia kauli kama, *kwenda haja kubwa* kwa maana ya kwenda kunya.

Hivyo basi, matumizi ya kauli ya *kwenda haja kubwa*, ni matumizi ya maneno masafi katika masikio ya wasikilizaji badala ya kauli kunya.

Wamitila (2008), anasema kuwa tasfida ni mbinu inayotumiwa katika maongezi au lugha ya kila siku kufichia ubaya, uozo au uovu fulani kwa kutumia maneno au lugha ambayo inapunguza makali au uozo, ubaya au uovu unaozungumziwa. Tasfida ni mbinu inayotawala au kutumika kwa mapana si tu katika lugha ya kila siku bali pia katika matini mbalimbali.

Anaendelea kusema kwamba tasfida ni neno au mfululizo wa maneno ambayo huchukua nafasi ya kusikitisha, ambayo si safi au mawazo ya kushangaza kwa maneno laini na ya heshima. Kwa mfano: *"kuondoka kutoka maisha"* ni kauli itumikayo badala ya kifo. Tasfida humsaidia mnenaji kujieleza kwa njia ya kupendeza na kumfurahisha mtazamaji na msikilizaji.

Wamitila (2012), anasema kuwa tasfida ni matumizi ya maneno ya kupunguza ukali au uzito fulani. Mtunzi anapotumia lugha nyingine badala ya lugha inayoudhi au ya kimatusi tunasema kuwa pana tasfida. Allan na Burridge (1991) wanasema kwamba neno tasfida ambalo ni tafsiri kutokana na *'euphemism'* hutokana na uambatanishi wa viambajengo vya Kigiriki'*eu'* kumaanisha 'nzuri' na '*pheme*'ambalo humaanisha kuzungumza. Kwa hivyo neno tasfida kwa tafsiri ya '*eupheme*' humaanisha kuzungumza kwa maneno mazuri au kuzungumza kwa usemi usioudhi na kumkera mtu.

Gatambuki (2009) akirejelea mawazo ya Bright (1985), Allan na Burridge (1991) anaeleza kuwa tasfida ni mbinu ya kutumia maneno mazuri, matamu, yanayopendeza, yaliyotiwa nakshi yakavutia. Pia anasema ni kutokusema maneno moja kwa moja ili kuepuka kudhuru uso wa msikilizaji.

Harry (1954) anasema kwamba lugha huashiria mfumo wa jamii husika, na kwa hivyo kuna uhusiano wa lugha na jamii ambapo lugha hiyo hutumika. Katika kila jamii

huwa kuna namna lugha hutumiwa na kuleta aibu ama hata kuwa vigumu kuyatumia maneno fulani katika lugha kwani ni mwiko. Kwa sababu hii, wazungumzaji wa lugha huweza kukwepa hali hiyo kwa kutumia lugha inayoonekana nzuri au yenye adabu nayo huitwa tasfida. Hivyo basi tasfida ni hali ya kutumia maneno yenye adabu.

Tunakubaliana na maelezo haya kwa sababu utafiti wetu ulidhihirisha kwamba wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi wameunda tasfida kutoka kwa mazingira yao, yaani kutokana na shughuli zaowanazokumbana nazo kila wakati ili waweze kuwasiliana kwa urahisi, kwa upole na kwa adabu bila kumshtumu yeyote mwenye kuathirika kwa njia moja au nyingine kutokana na hali hii ya VVU/UKIMWI. Hivyo basi tunaweza kusema kwamba tasfida ni maneno yanayoundwa na kila jamii ili kurahisisha mawasiliano, kuyafanikisha na pia kuhifadhia nyuso za wanaowasiliana.

Katamba (1985) anaeleza tasfida kama neno linalotumika kufafanua lugha, mawazo na dhana ambazo hupunguza chuki inayoletwa na tamaduni za jamii au kundi lolote la watu. Nakubaliana naye kwani katika mawasiliano kunaweza kuzuka hali za kutoelewana kutokana na matumizi ya lugha yasiyo na adabu au hata yasiyozingatia miiko za jamii za Kiafrika. Nakubaliana na Katamba (1985) kwamba tasfida zinapotumiwa hupunguza chuki na aibu inayotokana na matumizi ya maneno bayana bila kuyavisha nguo hivyo basi kupuuza miiko na hali za wanajamii. Katamba anaendelea kusema kwamba tasfida ni neno la upole na upole huzuia chuki na kutoelewana kwa watu katika jamii fulani au watu katika vikundi mbalimbali.

Ortony (1993), anasema tasfida ni kule kusema kitu kwa namna ambayo mtu huchukua tahadhari ili asiseme mambo ambayo huchukiza na kumwaibisha mzungumzaji au hadhira yake. Maelezo haya yalinifaa kwani vijana waliibua tasfida

na sitiari ambazo huwasaidia kuwasiliana kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika bila kumwaibisha mzungumzaji, msikilizaji, wazungumzaji au hata hadhira.

Leech (1983) anaeleza tasfida ifuatavyo, hali ya kutoa maana hasi na kutia maneno urembo/ kuyavisha nguo au nakshi ili yaonekane kuwa mazuri. Anaelezea zaidi kwa kusema kwamba mambo haya huwa katika kila jamii kutoka zamani ili kukwepa mijadala ambayo haifurahishi wengine. Mambo kama ngono, kifo, magonjwa na sehemu mbalimbali za mwili wa binadamu huwa ni mwiko kuzataja waziwazi jambo ambalo huifanya jamii lugha husika kuunda tasfida ili kuwasiliana kwa upole, bila kumshutumu yeyote. TUKI (1990) inasema tasfida au usafidi ni matumizi ya maneno ya staha badala ya yale halisi. Kwa mfano**,** mdudu ni neno la staha na lenye upole linalotumika katika mjadala wa VVU/UKIMWI badala ya neno UKIMWI.

Wardhaugh (2002) anasema kwamba lugha ya tasfida huruhusu watumizi lugha kufunika hali katika maisha na kuziwasilisha kwa njia ifaayo, kwa upole na kwa njia kubalifu kwa hadhira. Tasfida huruhusu wanajamii kuzungumza vitu visivyofaa kwa njia ifaayo ili kuvipunguza makali. Kwa mfano tasfida hutumika katika kueleza kitendo cha kujamiiana, kifo, sehemu za siri za kiume na za kike, hali ya ugonjwa wa VVU/UKIMWI. Tasfida pia huwawezesha watumizi lugha kuvipa vitu visivyofaa vibandiko na hata majina ya kuvifanya vipendeze.

Ullman (2005) anasema kwamba kila utamaduni huwa na mambo ambayo hayazungumzwi wazi ambayo huitwa miiko. Haya ni mambo au chochote kilichokatazwa katika jamii kwa sababu za kidini au za kiutamaduni. Katika matumizi ya lugha watu huyakwepa matumizi ya miiko na kujikita kwa kutumia lugha inayoonekana kuwa nzuri katika miktadha tofauti kulingana na mazingira, na hii ndiyo huitwa tasfida. Kutokana na utafiti wetu tumetambua kwamba tasfida huundwa

na watumizi lugha wa jamii yenye utamaduni mmoja. Tasfida hizi huundwa kama njia mojawapo ya kueleza mambo au kusema jambo kwa njia ya kutumia maneno au lugha ya adabu. Kwa mambo yanayoonekana mabaya au yanayoaibisha na kudunisha, tasfida hutumiwa kama njia ya kupunguza makali ya maneno kwa upole na adabu ili kuhifadhi uso wa mtu mwingine.

## 5.2 Uainishaji wa Tasfida

Kuna aina nyingi za tasfida. Katika utafiti huu tuliangazia aina mbili; yaani chanya na hasi. Rawson (1981) aliainisha tasfida katika kategoria chanya na hasi, hata kama yaliyotasfidiwa yanahusiana na miiko au la. Tasfida chanya kulingana na Rawson hutiwa chuku na huonekana muhimu sana kuliko vile ilivyo. Rawson anadai kuwa Waingereza na wamarekani hupendelea tasfida ambazo zimetiwa chuku hasa kutasfidi kitu ambacho hakipendezi na kinadhuru.

Rawson anaendelea kusema kuwa, tasfida zinazohusu watu wanaofanya kazi ndogondogo na duni huinua hadhi ya kazi hizo ili kusitiri nyuso za wafanyikazi wa kazi hizo au kuzifanya kazi zenyewe zionekane nzuri. Tasfida chanya hutiwa nakshi katika matumizi ya misamiati ya kisiasa, kijeshi na hali mbalimbali katika jamii kama VVU/UKIMWI. Katika huu utafiti tulikusanya tasfida za aina hizo mbili: chanya na hasi.

### 5.2.1 Tasfida zinazowakilisha ngono

33. *Mazungumzo ya vijana niliyoyasikia:*

*Kijana 1: Bwana wee, nina maumivu sana.*
*Kijana 2: Hahahaha bana wee* ***ulienda bafuni*** *vivyo hivyo bila* ***ninii****? Shauri yako umekanyaga* ***waya moto.***

Kauli “ulienda bafuni,” ilitumika kwa maana kwamba mtu anapoenda bafu, huvua nguo na kujifunga kanga. Ilibainika kwamba hali hii ilitumiwa kurejelea tendo la

ngono, kwani wasailiwa walichukulia kwamba mtu anaposhiriki katika tendo la ngono huvua nguo au mavazi, hali ambayo ilisababisha vijana kufananisha kwenda bafuni na tendo la ngono.

Kutokana na mazungumzo haya tunapata ya kwamba watafitiwa wameweza kuvisha nguo kauli fulanifulani katika jamii. Kwa mfano, kitendo cha ngono kurejelea kama ulienda vivyo hivyo bila kutumia kondomu au kujua hali zenu za VVU, basi umekanyaga *waya moto* yaani umepata maambukizi ya VVU/UKIMWI na tasfida *ninii* kuashiria *kondomu*. Aidha, kauli hizi zilibainisha uhifadhi wa tamaduni unaotokana na matumizi ya tasfida na wingi wa umaarufu wa matumizi ya lugha kati na baina ya vijana katika jamii husika.

34. *Kusuluhisha mgogoro wa ardhi*

Maana msingi ya kauli hii, ni kuja pamoja kwa kundi fulani la watu ili kusuluhisha jambo fulani katika jamii. Kutokana na kauli hii, ilibainika ya kwamba vijana wametumia kurejelea tendo la ngono kwa sababu, shughuli hii husababisha watu kutamangana au kuja pamoja kwa nia moja, kulingana na tajriba yao.

Watafitiwa walieleza kwamba, wakati kuna mgogoro au kutokubaliana kati ya ‘wapendanao’ juu ya jambo fulani tendo la ngono ‘husuluhisha’ yote, kati ya wapendanao. Yaani tendo la ngono limepewa uhai, kwamba ina uwezo wa kuleta makubaliano katika uhusiano wa watu katika jamii mbalimbali katika Afrika. Ilibainika kwamba vijana walihusisha matendo halisi yanayotendeka katika jamii ili kurejelea masuala wanayokumbana nayo kila wakati katika jamii. Hali hii ilibainisha dhana ya utambulishaji wa vijana katika jamii husika.

35. *Kuja pamoja*

Maana ya kimsingi ya kauli hii, ni kitendo cha kuungana na kukaribiana kwa watu wawili au zaidi. Watafitiwa walitumia kauli hii kurejelea tendo la ngono katika mazungumzo yao. Sababu zilizobainika ni kwamba, wanapokuwa na ashiki ni lazima wakutane ndipo tendo hili liweze kutendeka.

Aidha, walidokeza kuwa kauli *kuja pamoja* ni ya kawaida ambayo huwawezesha kuwasiliana bila aibu. Yale ambayo wametekeleza ni kuhamisha maneno hayo katika maana halisi hadi maana dokezi katika muktadha tofauti. Kitendo hiki huwawezesha kuhifadhi mila na desturi za jamii husika kwa kuvisha maneno nguo ili yasiwatie wanajamii aibu. Watafitiwa walikubali kuwa wameweza kuwasiliana juu ya ngono bayana kwa kutumia maneno (tasfida) ambayo ni ya kawaida katika miktadha mbalimbali ya kijamii. Suala ambalo ni mwiko kulizungumza bayana katika jamii za Afrika limewezeshwa kwa kutumia kauli ambazo vijana wameibua.

36. *Kuja nyumbani*

Maana halisi ya kauli hii, ni kule kurejea nyumbani au makao ya mhusika. Vijana walitumia kauli hii kurejelea tendo la ngono, kuwakilisha ile hali ya mtu kutaka shughuli ya ngono, kwa hivyo mtu huja nyumbani yaani kwa mpenzi wake asije akaenda "nje," akapata maambukizi ya magonjwa ya zinaa na maambukizi ya UKIMWI.

Kutokana na utafiti wetu, tuligundua kwamba kauli hii inayowakilisha tasfida hutumika mara kwa mara, hata kwa watumiaji wa lugha wenye umri wa makamo wanaposuluhisha mgogoro wa ndoa. Watatuzi wa mgogoro huuliza wahusika (mke na mme) kama mzee wa boma *huja nyumbani* na *kula nyumbani*, wakirejelea tendo la

ngono. Wasailiwa walisikika wakitaniana, *cheza kama wazee wetu, bana kuja nyumbani muhimu.*

Kauli hii kuja nyumbani ilidhihirisha wingi wa ubunifu wa vijana katika mazingira yao ya kila siku, jambo linalowezesha kujitambulisha na kuwasiliana kwa njia bora na 'safi' zaidi.

37. *Kufanya mapenzi*

Leksimu hizi huwakilisha maana ya hisia nzito zinazotokana na mvuto fulani baina ya mtu mzima mmoja na mwingine wa jinsia tofauti. Watafitiwa walitumia kauli hii *kufanya mapenzi* kuwakilisha tendo la ngono. Sababu za kutumia kauli hii ni kwamba lazima wapenzi au wahusika katika tendo lile wawe na hisia nzito zitakazosababisha kuwa na fikra za kushiriki katika tendo la ngono. Kauli hii imewezesha mawasiliano kuhusu ngono kuzungumziwa bayana bila kuvunja miiko iliyowekwa na jamii fulani, hivyo basi kufanikisha kampeni dhidi ya maambukizi ya magonjwa ya zinaa na hali ya VVU/UKIMWI.

38. *Kucheza mechi*

Kucheza mechi ni hali ya mashindano katika mchezo wa kandanda, ambapo wachezaji katika timu mbili hushiriki ili kupata ushindi katika shindano hilo. Watafitiwa walitumia kauli hii kuwakilisha tendo la ngono. Kutokana na utafiti ni kwamba, tendo la ngono limechukuliwa kama mechi baina ya timu A (mke), timu B (mume) na kutokana na 'shughuli' hiyo, wote hujitahidi (hushiriki) kwa minajili ya kumfurahisha mwenzake hali ambayo watafitiwa waliitumia kurejelea tendo la ngono. Kauli hizi ni za kawaida ambazo hata zikatajwa bayana hazitaleta aibu katika nyuso za wasikilizaji, hivyo basi kuwezesha mazungumzo baina ya watafitiwa kutendeka bila tashwishi.

39. *Kufumbua fumbo*

Leksimu kufumbua, ni kitenzi au tendo la kutatua jambo fulani lililosimbwa katika namna fiche. Hivyo basi, usemi katika hali hii hutolewa kwa njia ya kimafumbo na huhitaji kufumbuliwa. Tendo hili hushirikisha makundi mawili au watu katika pande mbili yaani wa kufumba na wa kufumbua. Katika hali ya kawaida fumbo hutumiwa kuelezea kauli ambazo huficha maana fulani. Huwa kuna jambo ambalo limefumbwa ambalo msikilizaji anahitajika kulifumbua labda kwa kutoa jibu au kutoa ufumbuzi (maelezo) unaotakiwa.

Shughuli hii imetumika kurejelea tendo la ngono, labda kwa sababu hutendeka katika mahali fiche kwa sababu ni kitendo cha siri sana kulingana na mila na tamaduni katika jamii nyingi za Afrika. Hali hii imetumiwa na watafitiwa kurejelea tendo la ngono. Yaani tendo la ngono ni kufumbua fumbo kati ya wapendanao.

Matokeo haya yalibainisha kwamba jamii za Afrika zimethamini tamaduni zake, kwamba kutaja ngono na masuala husika bayana katika miktadha anwai ni jambo la mwiko lisilokubalika katika jamii husika.

40 *Kuchinjia mmoja*

Leksimu hii ni kitenzi, chenye maana ya kuondoa sehemu ya udongo wa juu wa kifaa kilichofinyangwa. Kauli hii ilitumika kurejelea tendo la ngono. Wakati wa kushiriki tendo la ngono, ikiwa mshiriki wa kike ni bikira "sehemu ya juu huweza kuondolea" yaani kuvunja ubikira. Kutokana na utafiti ilibainika kwamba, tasfida hii ilibuniwa kwa misingi ya tamaduni za Afrika kwamba kijana wa jinsia ya kike lazima awe bikra ndiposa *kitumbua chake kiweze kuchinjika na kulika.*

Hivyo basi kutokana na dhana hiyo ya ubikra watafitiwa walifananisha ngono kwa kauli hizi: kuchinja, kudondoa, kuvuna mazao yaliyokomaa na kuyaacha yale ambayo

hayajakomaa yaendelee ‘kuiva’. Kauli hii pia iliweza kubainisha umahiri wa wanafunzi wa kutumia lugha na vipengele vyake yaani kuhamisha maneno au kauli za kawaida kutoka kwa muktadha halisi hadi muktadha lengwa.

41. *Kukuna nazi*

Maana halisi ya neno nazi ni tunda lililo ndani ya kifuu ambacho kimezingirwa na kumbi lenye nyama nyeupe na maji katikati. Kitenzi kuna kinaashiria kukwaruza ngozi kwa kutumia kifaa kiitwacho mbuzi ambacho kina ncha ambayo imenolewa kwa ajili ya kukuna nazi.

Watafitiwa wametumia maelezo haya kurejelea tendo la ngono. Sababu ambazo walitoa juu ya uhamisho maana huu ni: shughuli zifanywazo wakati wa kukuza nazi ni zilezile zitekelezwazo wakati wa kufanya tendo la ngono. Yaani uume umefananishwa na ncha yenye makali ambayo ‘hukuna’ na kupata utamu kutoka kwa sehemu za siri za kike jinsi mnazi hukunwa kwa minajili ya kupata nazi. Kutokana na utafiti huu, ilibainika kwamba, vijana wameweza kuhamisha kauli za kawaida kutoka kwa muktadha wa kawaida hadi muktadha lengwa. Y*aani wamevisha maneno nguo* jambo ambalo limewawezesha watafitiwa kuwasiliana juu ya masuala nyeti kwa namna inayokubalika katika jamii za Afrika ambazo zina makataa ya kuyataja masuala fulani fulani bayana.

### 5.2.2 Tasfida zinazohusikana sehemu za siri za mwanamke

Utafiti huu ulielekezwa na Nadharia ya Umaanisho ya Paul Grice (1978, 1995) na nadharia ya Mawasiliano ya Kiutambulisho ya Giles (1972 & 1982). Nadharia ya Umaanisho inaeleza jinsi watumiaji lugha katika mawasiliano hufahamu kauli tofauti ambazo hazihusiani katika diskosi na kuzifasiri kama zilivyokusudiwa. Aidha, anadai kuwa msikilizaji huwa na uwezo wa kufasiri na kuratibu ujumbe wa kiisimu na usio

wa kiisimu katika ufahamu wake. Naye Giles (1982, 1972) katika nadharia yake, anarejelea dhana ya utambulisho kama kigezo maalumu kinachotumiwa kumtambulisha mtu, kundi la watu, jamii au taifa fulani.

Katika mkabala huo, utafiti huu uligundua kwamba wanafunzi wamehamisha maneno kutoka muktadha mmoja hadi mwingine tofauti hivyo basi kuzua maana tofauti. Ujuzi huu hufaulu kulingana na uwezo wao wa kutumia lugha ambalo huwasaidia kujitambulisha na kujitofautisha kutoka kwa wanajamii wengine. Vilevile watafiti walitambua kwamba, tasfida na sitiara zilizokusanywa zilionyesha kwamba wanawake wanadunishwa na kudhalilishwa katika jamii. Tulikusanya sitiari na tasfida 14 zinazohusiana na sehemu za siri za mwanamke, ila tuliweza kuchanganua nne tu.

42**.** *Kisima safi*

Maana ya kimsingi ya kauli hii ni shimo ambalo huchimbwa kwenda chini kwa minajili ya kuchota na kuhifadhi maji kwa minajili ya matumizi ya nyumbani. Watafitiwa wamerejelea sehemu za siri za mwanamke yaani uuke kama *kisima safi* kwa sababu hubeba 'maji' ambayo ni uhai jinsi ambavyo uuke ni njia ambayo wanawake hutumia kuchukua mimba na kutunzwa hadi kuzaliwa. Hata hivyo walidokeza kwamba ukitaka kunywa maji maenge *chimba kisima* chako mwenyewe, na kila mtu *anywe* maji kutoka kwa *kisima* chake. Kwa kufanya hivi basi watafitiwa walisema kwamba kusambaa kwa VVU/UKIMWI litathibitishwa.

Hivyo basi, sehemu za mwanamke zimefananishwa na kisima ambacho huleta uhai kulingana na watafitiwa. Haya, vilevile yamedaiwa na mwimbaji mmoja wa Kitanzania anayeitwa Faustin Munishi ambaye ameimba wimbo mmoja ambao unasema kwamba: *Uchimbe kisima chako mwenyewe, unywe maji yako pekee yako,*

*usidanganyike nao wengine utaambukizwa wee. Maji ya kisima cha watu wengi yameingiwa na mdudu, utayapewa bila kuomba usidanganyike wee.*

Tuliposikiza huo wimbo tuligundua kwamba umetumia tasfida kwa wingi, mfano; unywe kwa maana ya ngono, *chimba* kwa maana ya *ngono,* kisima ~*uuke, mdudu~VVU/UKIMWI.*

43. *Kinu cha uzima*

Maana msingi ya dhana *kinu,* ni kifaa kilicho na shimo ambacho huwekwa viungo ambavyo hupondwa au kutwangwa kwa kutumia *mchi* yaani mti mdogo ulio na umbo lake. Watafitiwa wamerejelea kauli hii uuke kwa sababu ya umbo lake, na dhana kwamba halikamiliki pasipo na mchi (uume) ambao hutekeleza dhima yake. Mfano katika matumizi; *'Sherehe za jana usiku za "freshas night" zilikuwa shwari,tulitwanga viungo kwa kinu, mchi umewakawaka moto.'* Kauli hii inarejelea tendo la ngono walioshiriki.

Ilibainika kwamba kurejelea sehemu za uuke (kinu), kunaonyesha hali ya udunishaji wa mwanamke katika jamii. Aidha, dhana ya kinu imepanuliwa maana, kwa sababu, kinu ni kifaa ambacho katika miktadha tofauti hutekeleza majukumu tofauti na yale ambayo tumeyaeleza hapa. Tasfida hii iko katika kundi la tasfida hasi, tasfida ambazo ni za kudunisha ingawa zinahifadhi nyuso za wasikilizaji, hata hivyo ilibainika kwamba, hurahisha mawasiliano kati na baina ya wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu VVU/UKIMWI, ngono na masuala husika katika jamii.

44. *Kitumbua lika*

Kitumbua ni chakula, mfano wa mkate bapa mtamu unaotengenezwa kwa kutumia unga wa nafaka na viungo mbalimbali. Huliwa kwa chai au vinywaji vya aina yake au mchuzi. Vitumbua huwa haviliki vikiingiwa mchanga.

Watafitiwa walitumia dhana ya kitumbua kurejelea uuke, kwa sababu ya umbo la vitumbua kamili ambavyo vinadhihirisha lile umbo na 'utamu' wake. Aidha, walidai kuwa vitumbua vya wanawake haviliki *vikiingiwa na mchanga* kwa maana ikiwa binti si bikira. Kutokana na kauli hii buniwa, ilibainika kuwa wahusika wanaume wana taasubi za kiume. Wasailiwa wa jinsia ya kike, walitaka kujua jinsi ya kupima ubikira wa mwanamume jinsi nao wapimao ubikira wa wanawake. Hata hivyo, kauli hii ina umuhimu katika utafiti huu na iliweza kutuonyesha mtazamo wa jamii kwa mwanamke na mwanamume na pia kufanikisha mawasiliano ya ngono katika jamii bila kuvunja miiko ya jamii husika.

45. *Kabati*

Kabati ni chombo ambacho binadamu hutumia kwa kuhifadhi vyombo vyake nyumbani. Chombo hiki kimetumika kurejelea sehemu za siri za mwanamke. Sababu ni kwamba, ni mahali ambapo sehemu za siri za mwanamume huingia na zisionekane hadi *shughuli* zote zitapokamilika. Vilevile ni njia ambayo hupitisha mbegu za mwanamume kutoka sehemu moja hadi sehemu lengwa, na hivyo huweza kuchukua mimba, ambayo huhifadhiwa katika tumbo la uzazi mpaka muda wa kuzaliwa. Wasailiwa walitumia dhana hii kurejelea uuke kwa sababu ya shughuli halisi za chombo hiki katika muktadha wa nyumbani.

### 5.2.3 Tasfida zinazowakilisha sehemu za siri za wanaume (Uume)

Uchunguzi huu ulihakiki jumla ya tasfida 5 zilizohusiana na sehemu za siri za wanaume. Tasfida zilizokusanywa zilionyesha kwamba  wanaume wanachukuliwa kama watendaji na walinzi.

*46 Shoka*

*Kataa….kata, kata*2*
*Kata usiogope..,kata*2*
*Kata mti ni wako… kata*
***Shoka** tia makali…tia*
*Kataa…kata.kata*2*

Kimsingi ‘shoka’ ni kifaa ambacho hutumiwa katika kukata miti katika mazingira ya nyumbani. Katika mfano wa hapo juu, neno shoka limetumiwa kurejelea sehemu ya siri ya mwanamume kama inavyodhihirika katika wimbo huo ambao huimbwa katika mazingira ya harusi. Wimbo huo tuliudondoa kutoka kwa klabu cha uigizaji, ‘Moi University know AIDS Association’.

Kauli hii hutumiwa katika mawasiliano ya kawaida kwa maana ya kawaida, lakini tulibaini kwamba watafitiwa wametumia kauli hii kurejelea uume kwa sababu ya umbo la shoka na dhima yake katika mazingira ya nyumbani. Hivyo basi kurahisisha mawasiliano juu ya UKIMWI na masuala husika katika jamii ambazo imetenga maneno mengine kutumika wazi au bayana katika miktadha mbalimbali kwa sababu kwamba yanavunja maadili ya kijamii.

47. *Mshale sumu*

Leksimu mshale, ni kifaa cha kudungia ambacho kinaweza kutoboa shimo. Hutumika katika vita baina ya maadui, mshale huwadhuru zaidi ukiwa una sumu. Watafitiwa walitumia mshale sumu kurejelea sehemu za uume kwa sababu ya umbo lake na dhima yake katika jamii, kwa kuwa huweza kudunga na kutoboa sehemu ya siri ya mwanamke na tena kuacha sumu ikiwa ‘mshiriki’ ana ugonjwa wa zinaa.

Kauli hii imetumiwa kitasfida, tendo ambalo limetekeleza upanuzi wa maana na kuwawezesha wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Moi kuweza kuwasiliana bila woga

wala kuvunja miiko na desturi za jamii za Afrika ambazo zimeweka makataa ya kutaja masuala haya bayana.

Tulipochunguza matumizi ya kauli *mshale sumu* kwa kurejelea sehemu za siri za wanaume kitasfida katika lugha ya Kiswahili, tulitambua kwamba imelinganishwa na vifaa vyenye makali ya kukatia na kuchimba. Huu ni mtazamo wa mwanamume katika jamii kwamba yeye ni mlinzi na mtendaji.

Mifano mingine ya tasfida ni: *bunduki, risasi na wembe*. Kauli hizi zote zilitumiwa kurejelea uume. Ni vifaa na kazi yake huwa ni kuchimba, kutoboa na kukata. Kauli hizi zimepewa upanuzi wa kimaana katika muktadha tumizi. Kile kinachokatwa hapa ni sehemu za siri za mwanamke.

Aidha, ilibainika kwamba kauli teuliwa hupatikana kwenye mazingira halisi ya watumizi. Tasfida kama kipengele cha lugha kimetumiwa kuhifadhi nyuso za wengi, hivyo basi kuwezesha mawasiliano kutekelezwa miongoni mwa wanafunzi kuhusu masuala ya UKIMWI, ngono na mengineyo. Ambapo kuyataja bayana ni mwiko katika jamii za Kiafrika.

### 5.3 Tasfida za VVU/UKIMWI

Utafiti huu uligundua kwamba wanafunzi wameibiua tasfida anuwai katika kueleza dhana ya VVU/UKIMWI. Vipengele hivi huwa na majukumu mengi kama kufunika aibu na kurahisisha mazungumzo.

48. *Kuungua/kuchomeka*

Kauli hizi zimetumiwa kurejelea hali hii ya VVU/UKIMWI, kwa sababu mtu anapopatwa na hali hii, kinga za mwilini huuliwa na virusi hivyo na kuacha mwili bila kinga. Hali hii husababisha mwili kushikwa na magonjwa anuwai, yakiwemo ya

kufanya ngozi ya mwathiriwa kukauka na kuonekana kama aliyeungua. Hali hii ilisababisha watafitiwa kurejelea ugonjwa huu kama kuungua au kuchomeka. Aidha, kauli hii ilitumika kukashifu tendo la ngono za mapema na bila kinga katika jamii miongoni mwa vijana wa Chuo Kikuu cha Moi.

49. *Kufa polepole*

Maana msingi ya kauli hii ni hali ya kudhoofika kimwili polepole. Hali hii husababisha maafa ya mtu kufa polepole japo kwa hakika. Kauli hii inadhihirisha matumizi ya lugha kwa namna ya kufumba maana kusudiwa. Kauli 'kufa polepole' imetumika kurejelea hali ya VVU/UKIMWI. Katika jamii, waathiriwa wa hali hii, hukosa kinga mwilini hali ambayo husababisha waathiriwa kudhoofika polepole hadi kufariki. Kwa hivyo, katika muktadha wa maingiliano kati na baina ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi wanapotoa kauli hii, wanajaribu kuwasiliana juu ya maswali nyeti kwa siri au mafumbo ili kuficha ukali wa maneno.

Kutokana na kauli hii, *kufa polepole* tunapata kwamba, maana kusudiwa hujitokeza kwa kufananisha dhana moja kupitia ufafanuzi wa dhana nyingine. Mfano ni *kufa polepole,* kurejelea VVU/UKIMWI. Haya yanafafanuliwa vyema na nadharia ya Umaanisho ya Paul Grice (1978, 1975). Grice anaeleza jinsi watumiaji lugha katika mawasiliano hufahamu kauli tofauti ambazo hazihusiani katika diskosi na kuzifasiri kama zilivyokusudiwa. Aidha, anadai kuwa msikilizaji huwa na uwezo wa kufasiri na kuratibu ujumbe wa kiisimu na usio wa kiisimu katika ufahamu wake.

50. *Kuumwa na mbuzi*

Kauli *kuumwa na mbuzi* imetumika kurejelea hali ya VVU/UKIMWI, kwa maana kwamba, meno ya mbuzi hayapendezi yatazamwapo kwa sababu ya sura yake.

Vilevile huwa na sumu kama inadhihirika pale aumapo mimea, mimea hiyo hukauka yaani hainawiri tena.

Katika maingiliano ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi, walitumia kauli *kuumwa na mbuzi* kurejelea hali ya VVU/UKIMWI, kwa sababu virusi hivyo huathiri afya nzuri ya mwathiriwa. Maelezo haya yanafafanuliwa vyema na nadharia ya utafiti ya Utambulisho wa Kimawasiliano. Inadokeza juu ya mahusiano yaliyopo kati ya lugha, muktadha na utambulisho, kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya matumizi ya lugha, muktadha na utambulisho wa kundi lengwa. Katika utafiti wetu ilibainika kwamba vijana hutumia lugha kwa namna yao, hali ambayo huwatambulisha katika jamii husika.

Aidha, kauli hii, *kuumwa na mbuzi* ni maneno ya kawaida tuyatazamapo lakini wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi wameweza kusitiri maana mle ndani jambo ambalo limeweza kuhifadhi tamadumi na mila za jamii. Maelezo haya yanaunga mawazo ya nadharia ya Umaanisho kwamba usemi huwa na maana mbili: maana isimu na maana kulingana na msemaji.

51. *Kukanyaga waya wa stima*

Kauli hii ya kukanyaga *waya wa stima* imetumika kurejelea VVU/UKIMWI, kwa maana kwamba mtu anapokanyaga *waya wa stima* hukauka na kufa papo hapo na wakati wote hukanyaga bila kutarajia. Hivyo basi kauli hizi zimetumiwa kurejelea hali ya na VVU/UKIMWI kwa sababu, mtu hupata hali hiyo pasipo kutaka ambayo huangamiza kinga mwilini mwake. Hali hii inapompata mtu, hudhoofika na kusalia mifupa bila nyama mithili ya waya wa stima.

Hali hii imewatia vijana woga sana, hata hivyo ni mojawapo ya kauli ambazo zimewezeza mawasiliano kati na baina wanafunzi katika harakati ya kuwasiliana na wenzao juu ya hali hii kwa kuashiria kauli ya kawaida mno; *kukanyaga waya wa stima* ambayo hubeba maana kusudiwa na watafitiwa. Waya ya stima ni hatari kwani mtu ashikapo kwa mikono mitupu hufa papo hapo, hali ambayo watafitiwa walidokeza kwamba mtu anaposhiriki ngono bila kutumia kinga ni sawa na kugusa stima na mkono mtupu.

52. *Kurogwa na dunia*

Kurogwa ni imani fulani ya baadhi ya jamii za Kiafrika, ambapo mtu anapodhoofika kiafya huchukuliwa kwamba amefanyiwa mazingaombwe au amechimbiwa 'mizizi'. Kauli hii ilitumika zaidi kurejelea hali ya VVU/UKIMWI nyakati za awali, kwa sababu jamii haikuelewa hali hii. Kukosa kuelewa hali ile ya VVU/UKIMWI, kulisababisha jamii kuchukulia kwamba, mgonjwa aliyekuwa na dalili za kiajabuajabu huwa amerogwa.

Hata baada ya jamii kuelimishwa juu ya VVU/UKIMWI, watafitiwa walitumia kauli *kurogwa na dunia* kurejelea VVU/UKIMWI, japo kwa maana tofauti yaani kusimba maana kwa kauli hii. Kauli hii iliwawezesha kuzungumzia masuala nyeti ya jamii ambayo kuyazungumza bayana huleta ukali na unyanyapaa kwa msikilizaji.

**5.4 Tasfida Zinazorejelea Kondomu**

Tuligundua kwamba, maingiliano ya wasailiwa kuhusu ngono na VVU/UKIMWI hayawezi kukamilika bila kutaja kondomu. Kondomu ni mfuko mdogo wa mpira ambao huvaliwa katika sehemu za siri za kiume au kike wakati wa tendo la ngono ili kukinga maambukizi ya ugonjwa wa zinaa, VVU/UKIMWI na mimba. Hivyo basi

utafiti huu ulikusanya jumla ya tasfida 12, lakini tuliweza kujadili 5 (tano). Maelezo ya matokeo ya utafiti juu ya suala hili ni kama yafuatayo:

53. *Kabuti zito*

Kabuti ni leksimu yenye maana ya, koti zito la kujikinga dhidi ya baridi kali au mvua, ili baridi na mvua isije ikamdhuru mhusika. Kauli hii imetumika kurejelea kondomu kwa sababu ya dhima yake, yaani kukinga miili ya washiriki kukutana ili wasije wakaambukizana ikiwa *hali zao si sawa.*

Neno, *kabuti zito,* ni la kawaida tu katika mazingira ya kawaida, lakini wasailiwa wamelihamisha kutoka kwa msamiati wa mavazi yaani muktadha wa kinyumbani hadi muktadha wa kiafya, kauli ambayo iliwawezesha watafitiwa kuwasiliana bila kuvunja miiko ya jamii husika. Hili lilidhihihirisha ujuzi wa lugha miongoni mwa wasailiwa na hisia za kitamaduni walizo nazo watafitiwa. Maelezo haya yanafafanuliwa vyema na nadharia iliyoungoza utafiti huu ya, Mawasiliano Kiutambulisho, ambayo inadokeza kwamba tamaduni na tajriba ni vigezo muhimu sana katika mawasiliano.

Watafitiwa kuibua istilahi za tasfida kwa minajili ya kuwasiliana kuhusu masuala ya VVU/UKIMWI ambayo ni mwiko kuyataja bayana katika jamii za Kiafrika. Ni kutokana na tajriba za wazungumzaji ambapo waliweza kuhamisha istilahi kutoka kwa muktadha wa maana msingi hadi muktadha tofauti na kuweza kudokeza maana kusudiwa.

54. *Ngao*

Kutokana na utafiti wetu, istilahi *ngao*, ni kifaa kitumiwacho katika vita kati ya maadui. Wasailiwa walitumia kauli hii ngao kurejelea kondomu, kwa sababu ya dhima ya ngao. Yaani kifaa hiki kimeitwa ngao, kwa sababu hukinga maambukizi ya

magonjwa ya zinaa na VVU/UKIMWI. Tendo la ngono pia limerejelewa na leksimu 'vita.'

Kutokana na utafiti, mtafiti aligundua kwamba watafitiwa huibua istilahi za kitasfida kutoka kwa mazingira yao husika. Tulibaini kuwa kauli zilizoibuliwa zinafanikisha mawasiliano kati na baina ya wasailiwa wa Chuo Kikuuu cha Moi, kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika.

55. *Bomba la medali*

*Bomba la medali*, ni kifaa chenye uwazi ndani, kama mwanzi, kilichotengenezwa kwa chuma au plastiki au mchanganyiko wa saruji na kokoto ambacho hutumika kusafirisha viowevu. Maana ya kimsingi ya medali, ni thamani ya shaba, fedha au dhahabu anayopewa mshindi katika mashindano ya mchezo au mtu anayepongezwa kwa mafanikio fulani.

Kauli hii *bomba la medali* imetumika kurejelea kondomu kutokana na jinsi bomba huundwa ili isiweze kumwaga kile kibebwacho na vilevile umbo la bomba. Kondomu pia huchukuliwa kuwa bomba la medali, yaani huzuilia manii isiweze kumwagika kwenye sehemu za siri za mwanamke. Tendo hili linaweza kusababisha maambukizi ya magonjwa ya zinaa na VVU/UKIMWI kutoka kwa mhusika mmoja hadi kwa mwingine. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, kauli 'medali' ilitumiwa kurejelea uume.

Kutokana na tasfida rejelewa, tuligundua kwamba, wanaume katika jamii za Afrika wanachukuliwa kuwa wa thamani na hivyo hawataki kuhatarisha maisha yao. Kutokana na maoni ya wasailiwa wa kiume, wasailiwa wa jinsia ya kike ndio husambaza hali hii ya VVU/UKIMWI. Hivyo basi tuligundua kwamba matumizi ya

tasfida bomba la medali, kumesisitiza umuhimu wa wanaume katika jamii za Afrika. Hivyo basi husisitiza pia matumizi ya kondomu ili kulikabili janga hili la UKIMWI.

56. *Kifaa*

Leksimu *kifaa* ina maana ya chombo kinachotumiwa kufanya shughuli yoyote ile au fulani. Wasailiwa walitumia kauli hii *kifaa* kurejelea kondomu, kwa sababu ni hitaji muhimu katika tendo la ngono, licha ya maana kwamba tangu hali hii ya VVU/UKIMWI igunduliwe wasailiwa wamedai kwamba tendo la ngono haliwezi kutekelezwa bila kifaa, ili kupunguza maenezi ya magonjwa ya zinaa na VVU/UKIMWI.

Katika utafiti huu, ilibainika kwamba, kauli hii iliwezesha mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI miongoni mwa wasailiwa hutekelezwa bila kikwazo chochote, kwa sababu kauli hii ni ya kawaida, itumikapo katika mawasiliano haikwamizi mawasiliano.

57. *Kibana mwili*

Maana msingi ya *kibana mwili* ni aina ya kipande cha bati au plastiki kinachoweza kushikilia mahali bila ya kulegea. Wasailiwa walirejelea kondomu kibana mwili, kwa sababu hubana sehemu za siri za uume na uuke, hali iliyochangia wasailiwa kutumia kauli hii kurejelea kondomu.

Aidha, kupitia kwa kauli hii, imebainika kwamba wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi huteua maneno/kauli za kutumiwa kulingana na muktadha, mada na hadhira lengwa. Uteuzi huu ndio unaowezesha kauli hii kuwasilisha jumbe nyeti kwa urahisi; jumbe ambazo hazingeweza kuwasilishwa katika muktadha wa mazungumzo ya kawaida kwa kutumia maneno bayana. Hivyo basi huwezesha kupiga kampeni dhidi ya ugonjwa au hali hii ya VVU/UKIMWI katika jamii.

### 5.5 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia tasfida za Kiswahili zinazotumiwa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi kati na baina yao katika mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika. Tumejadili tasfida anuwai: tasfida za ngono au kujamiiana, uume, uuke na VVU/UKIMWI. Aidha, tumeonyesha sababu za kuibua tasfida hizo kwa kila kitajwa, ambapo tulibaini kwamba tasfida zilizoibuliwa kwa kusudi la kurejealea masuala nyeti katika VVU/UKIMWI, zinaakisi mielekeo na imani ya wanajamii mbalimbali. Pia tuligundua kwamba mwanamume amerejelewa na tasfida ambazo zinaakisi matarajio ya jamii kwa jinsia ya kiume. Dai hili limetokana na baadhi ya mifano kama ifuatayo inayorejelea uume: mkuki, mshale, wembe, shoka, bunduki, mti na silaha.

# SURA YA SITA

# DHIMA YA SITIARI NA TASFIDA KATIKA MAWASILIANO YA VVU/UKIMWI MIONGONI MWA WANAFUNZI

## 6.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumeshughulikia umuhimu wa sitiari na tasfida katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika, katika maingiliano kati na baina ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi. Nimefanya hivi kwa kuchanganua data nilizokusanya kutoka nyanjani, huku nikichunguza dhima ya kila moja jinsi ilivyobainika katika mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI. Hivyo basi, nimeangalia dhima ya kauli zilizotumiwa kurejelea tasfida na zile za kisitiari. Haya yaliwezekana kwa sababu tuliegemea matumizi ya vipengele hivi katika miktadha mbalimbali inayohusiana na masuala haya ya VVU/UKIMWI.

## 6.1 Dhima ya Sitiari katika Mawasiliano ya VVU/UKIMWI

Katika sehemu hii, mtafiti ameshughulikia matokeo ya utafiti kwa mujibu wa lengo la tatu: Kupambanua nafasi ya sitiari katika mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika. Nafasi ya kauli za kisitiari imebainishwa kwa kudondoa kauli za kisitiari na kufafanua nafasi yake kwa misingi ya nadharia teule. Hii ni katika kuthibitisha kwamba, mawasiliano ni njia kuu ya kupitisha ujumbe husika katika jamii.

Kila jamii huwa na kaida za utamaduni zinazoitawala. Jamii mbalimbali huwa na mbinu ambazo hutumiwa katika kujitambulisha na kujitofautisha. Hivyo basi, jamii huweza kutambuliwa kwa mambo kadhaa yakiwemo matumizi ya lugha, imani, mavazi na vyakula vyao. Hivyo basi, kauli za kisitiari katika mawasiliano kati na baina ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi ilibainika kutekeleza yafuatayo:

### 6.1.1 Kufikirisha jamii

Ilibainika kuwa kauli za kisitiari zilizoibuliwa na vijana katika mawasiliano yao ya kila siku huwa na jukumu la kufikirisha katika harakati za kupitisha ujumbe, mbali na kurahisisha mawasiliano katika jamii husika. Ili kuweza kung'amua ujumbe huu uliofumbwa, msikilizaji hushurutika kuwaza na kuwazua na kutafakari kuhusu yaliyosemwa. Wasikilizaji hutafakari ili kutambua kilichokusudiwa na msemaji, msikilizaji huhitajika kutafakari kwa undani ili kutambua maana ya ujumbe husika.

Hali hii inafafanuliwa na Nadharia ya Umaanisho ya Paul Grice (1978, 1975) na nadharia ya Mawasiliano ya Kiutambulisho ya Giles (1972, 1982). Katika nadharia hizi, wanaeleza jinsi watumiaji lugha katika mawasiliano hufahamu kauli tofauti ambazo hazihusiani katika diskosi na kuzifasiri kama zilivyokusudiwa. Aidha, anadai kuwa msikilizaji huwa na uwezo wa kufasiri na kuratibu ujumbe wa kiisimu na usio wa kiisimu katika ufahamu wake. Hivyo basi, msikilizaji huweza kung'amua maana iliyokusudiwa katika kauli ya msemaji kutegemea muktadha wa usemaji pamoja na vidokezo anavyotoa msemaji wa kauli husika.

### 6.1.2 Hukuza na kufunza maadili

Kutokana na utafiti, ilibainika kuwa kutumia lugha kisitiari katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika ni hali ambayo inaambatana na haja ya kuzingatia maadili katika jamii za Afrika. Vijana wametumia sitiari na tasfida katika mazungumzo yao juu ya suala la VVU/UKIMWI. Wanafanya hivyo ili kuficha makali ya ujumbe wao waliokusudia kuwasilisha sababu ya tamaduni na mila za jamii za Kiafrika wanamotoka wazungumzaji.

Mtafiti aliweza kutambua na kubainisha jinsi kauli za kisitiari hutoa ushauri kwa wanajamii. Baadhi ya kauli zinazoonyesha utoaji wa mawaidha ni: foksi/paka

mapepe, teksi bubu/gari kubwa, chokoraa na mama/dada huruma. Japo kauli hizi zinaonekana kukejeli anayerejelewa kwazo, kwa upande mwingine zinalenga kutoa nasaha kwa jamii ili wabadili hali walizo nazo, wajichunge ili wasije wakapata hali ya VVU/UKIMWI itakayowasababishia kurejelewa kwa kejeli kwa matumizi ya kauli zilizoorodheshwa hapo juu.

Kauli zilizonukuliwa katika sura ya nne, zinazorejelea ngono zinaashiria ujumbe kwa njia fiche katika mawasiliano ya vijana. Walibuni sitiari hizi ili kuashiria tendo la ngono (*kulima, mkutano, Mombasa raha n.k*) hali ambayo inaashiria matumizi ya lugha ya kawaida inayodhihirisha heshima. Dhana ya kufanya mapenzi inafananishwa na mkutano, kulima, kutafuna na hata raha watu wapatayo wanapotembea mjini Mombasa. Mawazo haya yanafafanuliwa na dhana sitiari, inayodokeza kuwa sitiari hutumiwa katika kuelewa maana ya jambo fulani kupitia ulinganishi wa dhana moja na nyingine.

### 6.1.3 Kuweka mipaka miongoni mwa wanajamii

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, imedhihirika kwamba, jamii za Afrika huwa na mipaka mbalimbali kijinsia, kirika na kinasaba. Kupitia kwa utafiti huu basi, hali hii inabainika wazi. Data zilizokusanywa ziliangazia pakubwa suala la mahusiano ya kijamii likiwemo lile la kijinsia. Mahitaji na matamanio ya wanajamii yalidhihirika kutokana na kauli za kisitiari zilizobuniwa na vijana katika mawasiliano yao ya VVU/UKIMWI.

Aidha, kauli zilizoibuliwa ziliangazia jinsi binadamu anavyofikiria na anavyouona ulimwengu wake. Ilibainika kwamba binadamu hutumia maneno kuweka wazi fikra, tendo na mtazamo wake wa mazingira na ulimwengu kwa jumla.

Kutokana na hoja hii ilibainika kuwa wanaume wamepewa hadhi ya juu katika jamii, wameangaziwa kama mwenye nguvu, watenda, walinzi, yaani wameangaziwa kama viumbe muhimu katika jamii. Katika upande wa jinsia ya kike wameshadidiwa kama viumbe wamilikiwa, dhaifu, wanaosababisha migogoro katika jamii. Hivyo basi, watafitiwa wametumia kauli zinazoashiria ujenzi wa mipaka ya kijinsia katika jamii.

Hata hivyo, ilibainika kuwa kauli za kisitiari zilizorejelewa zilidhihirisha jinsi mtu anavyofikiria na kuuona ulimwengu wake yaani mazingira halisi. Kutokana na utafiti huu pia, ilibainika kwamba kauli zilizorejelea ujenzi wa mipaka ni za kijinsia.

### 6.1.4 Kuendeleza utamaduni wa jamii

Ilibainika kuwa dhima kuu ya lugha, ni kuwasiliana na kuhifadhi utamaduni wa jamii husika. Hivyo basi, vijana kubuni sitiari za kuwasiliana kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika, ni jambo ambalo lilisababishwa na utamaduni wa jamii husika. Hivyo basi, watafitiwa lazima wajumuishe masuala ambayo hayakinzani na utamaduni ambamo vipengele hivyo vya lugha hutumika.

Kuna baadhi ya masuala ambayo hayaruhusiwi kuangaziwa hadharani katika jamii za Afrika, hivyo basi matumizi ya sitiari katika mawasiliano hukuza na kuendeleza masuala ya kitamaduni miongoni mwa jamii za Afrika. Ilibainika kwamba watafitiwa waliibua sitiari ambazo hutumia kauli ambazo zinaambatana na mila na desturi za jamii za Kiafrika. Mfano wa hali hii ni kuwa kuna baadhi ya masuala ambayo ni mwiko kuyataja hadharani kwa mfano *kuma* (uuke), *kutombana (ngono*). Hii ni katika juhudi za kuepuka kukiuka desturi za jamii mbalimbali za Afrika.

### 6.1.5 Kitambulisho cha jamii

Ilibainika kuwa matumizi ya sitiari miongoni mwa vijana huzua umaarufu fulani, yaani vijana wameweza kujitambulisha na kujitenga na jamii husika kupitia umaarufu

huu wa kuibua kauli za sitiari za kuwasiliana kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika katika jamii. Hata hivyo, iligunduliwa kwamba sitiari husaidia katika mpangilio wa masuala katika matapo ya jinsi tunavyofikiria na kuuona ulimwengu wetu kama binadamu.

**6.2 Dhima ya Tasfida katika Mawasiliano ya VVU/UKIMWI**

Kutokana na utafiti wetu tuligundua umuhimu ufuatao wa vipengele hivi katika mazungumzo ya kawaida ya vijana: tulibaini kwamba tasfida humsaidia mnenaji kujieleza kwa njia ya kupendeza na kumfurahisha mtazamaji na msikilizaji. Mfano: mawingu kumaanisha dalili za mtu aliye na virusi vya UKIMWI badala ya kusema huyu mtu amekonda kama ng'onda kutokana na VVU/UKIMWI. Kuchimba kisima hutumiwa kumaanisha tendo la ngono badala ya kusema *kutombana*. Hivyo basi tuligungua kwamba mtu anapotumia vipengele hivi huweza kujieleza kwa njia ya kupendeza na ya upole zaidi.

Kutokana na utafiti, tuligugundua kwamba kipengele hiki yaani tasfida huchukua nafasi ya kuchukiza, ambayo si safi au mawazo ya kushangaza kwa maneno laini na ya heshima. Mfano**:** badala ya kusema kondomu unaweza kutumia vipengele kama ngao, upendo kinga, je, una yako? na kabuti. Kutokana na mifano hii tulibaini kwamba matumizi ya kauli hizi huwezesha mazungumzo ya VVU/UKIMWI kutekelezwa katika hali ambayo si ya kuchukiza.

Utafiti wetu ulituonyesha kwamba kipengele hiki cha tasfida huleta ulinganishi na uhamishaji wa maana kutoka muktadha mmoja hadi mwingine, jambo ambalo limechangia kukuza na kuhifadhi lugha ya Kiswahili. Mfano kabati badala ya kuma, mtaimbo badala ya *mboro*.

### 6.2.1 Kupunguza kutoelewana

Kutokana na utafiti tulibaini kwamba kipengele hiki kimechangia kupunguza kutoelewana na machukizo yanayotokana na matumizi ya maneno au dhana za miiko kwa kutojali hali za wengine. Kauli za kitasfida zilizoibuliwa na watafiti zinazua upole, na upole kwa kawaida huzuia chuki, hivyo basi vipengele hivi huwasaidia wazungumzaji kuwasiliana kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika bila kuona aibu kwa mzungumzaji, msikilizaji au hadhira.

### 6.2.2 Kupunguza Makali

Kutokana na utafiti huu, tulibaini kuwa tasfida ni kipengele ambacho hutia maneno urembo au huyavisha maneno nguo au nakshi ili yaonekane kuwa mazuri. Hivyo basi kipengele hiki cha lugha kimewezesha watumiaji wa lugha husika kufunika hali katika maisha na kuziwasilisha kwa njia ifaayo, kwa njia kubalifu kwa hadhira. Jambo hili limerahisisha mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI, hivyo basi kurahisisha uhamasisho kwa wanajamii juu ya janga hili.

Tasfida pia huwawezesha watumiaji wa lugha husika kuvipa vitu visivyofaa machoni na masikio vibandiko na hata majina ya kuvifanya vipendeze, hivyo basi kuhifadhi tamaduni na desturi za Kiafrika kwani kutaja sehemu za siri bayana, tendo la ngono na hali ya VVU/UKIMWI ni kitendo cha aibu sana na mwiko. Hivyo basi, kuibua kipengele hiki ni jambo ambalo limechangia katika uhifadhi wa mila na tamaduni za Afrika. Hivyo basi, tasfida ni kipengele cha lugha ambacho huficha au kufunika maneno ya mwiko, kwa mfano badala ya kusema *kutombana* wanatumia tasfida kama**:** kuja nyumbani, kula nyumbani, kulima, kukuta vitu, mkutano; uuke: kapedo, chakula, tunda na ua.

Aidha, kutokana na utafiti, tuligundua kwamba, tasfida ni matumizi ya maneno mazuri, matamu, yanayopendeza, yaliyotiwa nakshi yakavutia, hivyo basi kauli zilizobuniwa kurejelea vipengele vya utafiti huepusha kudhuru nyuso za wasikilizaji.

Pamoja na hayo, tulibaini kwamba kauli za kitasfida zilizoibuliwa na watafitiwa, hutumika kuipamba lugha na kuongeza utamu katika lugha inayotumika katika kuunda au kutoa msisitizo wa maana pamoja na kuunda dhana mpya katika lugha husika jambo ambalo husababisha upanuzi wa maana na ukuzaji msamiati wa lugha husika. Tasfida pia hutumika kupunguza makali na kuweka ulaini wa mambo au kuficha matusi au kuziba uchafu. Mfano, badala ya kusema *kutomba* (ngono), wanafunzi walitumia: kucheza mechi, mpigo na Mombasa raha.

Kulingana na utafiti wetu, tuligundua kwamba baadhi ya tasfida zilizowakilisha uuke yaani sehemu za siri za kike ni za kudunisha na kumfanya mhusika wa jinsia ya kike aonekane duni. Haya yaliafikiwa tulipolinganisha vipengele vilivyobuniwa kuwakilisha sehemu za siri za uume na zile uuke. Mifano ya tasfida na sitiari hizo ni pamoja na mkuki, shoka, bunduki, silaha, kisu, mti (uume) na sehemu za kike kama vile kinu, migingo, sufuria na kitumbua.

Tasfida hupunguza woga na ukali, mfano ugonjwa wa UKIMWI unaogopwa sana, hivyo basi kwa kutumia vipengele hivi uoga na ukali hupunguzwa. Mifano ya vipengele hivi ni kama vile kuungua, ukedi, kuchomeka na waya wa stima.

Kutokana na matumizi ya tasfida, mtu huweza kujenga uso chanya katika mawasiliano na huweza kujikinga na kuinua hadhi yake katika fikra za wazungumzaji, jambo ambalo hukuza heshima miongoni mwa wazungumzaji. Hivyo basi kuwezesha mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika, kutekelezwa

kati na baina ya wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Moi, jambo ambalo limechangia katika kupiga vita ugonjwa huu.

Matokeo ya utafiti huu, yalibaini kwamba baadhi ya kauli za kitasfida zilizoibuliwa zimedhihirisha hali ya kuweka siri, hivyo basi kuwezesha mawasiliano kati na baina ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi kuwasiliana na kuhamasishana kuhusu masuala ya VVU/UKIMWI na namna ya kuyaangamiza yasiweze kudhuru wengi.

### 6.3 Hitimisho

Kutokana na utafiti, ilibainika kwamba uibukaji wa vipengele hivi (tasfida na sitiari) umewezesha mawasiliano kutekelezwa katika jamii mbalimbali za Afrika kwani ni mwiko kutaja VVU/UKIMWI na masuala husika bayana, hivyo basi kupunguza maambukizi na unyanyapaa nchini. Hili limewezeshwa kwa sababu, wasia juu ya hali hii huweza kutolea kwa jamii bila vizingiti vingi. Aidha, uchunguzi huu umebainisha kuwa vijana nchini hasa kutoka Chuo Kikuu cha Moi hutumia sitiari na tasfida katika mazungumzo yao kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika ili kusimba maana iliyokusudiwa. Hali hii inasababishwa na masuala kadhaa ambayo yanafungamana na jamii za Afrika.

Utafiti huu umebainisha kuwa kuna baadhi ya masuala ya kijamii ambayo hayafai kuwekwa wazi kwa sababu kadhaa. Msukumo wa kuficha maana kusudiwa katika kauli miongoni mwa wanafunzi wa idara ya Kiswahili hutokana na haja ya kuendeleza tasfida na sitiari katika jamii. Lugha yoyote ile hufungamana na utamaduni wa jamii, kwa hivyo, ili kukuza matumizi ya lugha ya heshima kizazi baada ya kizazi, vijana katika Chuo Kikuu cha Moi wameonyesha usimbaji wa maana kusudiwa katika kauli za kawaida ambazo zimeweza kuonyesha dhima anuwai za sitiari na tasfida katika kupiga vita ugonjwa huu ambao umeangamiza wengi.

# SURA YA SABA

# MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

## 7.0 Utangulizi

Hii ndiyo sura ya mwisho ambayo imetoa muhtasari wa utafiti. Katika sura hii nimetoa muhtasari wa tasnifu, mahitimisho ya matokeo, mchango wa utafiti, nimetoa mapendekezo ya tafiti zijazo na hitimisho.

## 7.1 Muhtasari wa Tasnifu

Kwa muhtasari, tasnifu hii ina sura saba. Katika sura ya kwanza, mtafiti alishughulikia msingi wa utafiti huu. Masuala yaliyojadiliwa katika msingi wa utafiti ni pamoja na kufafanua usuli wa utafiti, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, umuhimu wa utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti na hitimisho.

Katika sura ya pili, maandishi mbalimbali yaliyowahi kutafitiwa hapo awali na watafiti wengine yalihakikiwa na mtafiti. Maandishi kama vile tasnifu, majarida, vitabu na maelezo katika mitandao yalikuwa nguzo kuu katika kumfahamisha mtafiti kuhusu masuala aliyohitaji kujua kuhusu sitiari na tasfida kando na kuonyesha pengo la utafiti ambalo kwalo mtafiti alipata ilhamu za kutekeleza utafiti huu. Aidha, kipengele cha nadharia kilichoongoza utafiti huu kilishughulikiwa katika sehemu hii.

Sura ya tatu ilimulika mbinu na njia za utafiti zilizotumiwa katika kukusanya na kuchanganua data ya utafiti huu uliohusu uhakiki wa sitiari na tasfida zinazotumika katika mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika, miongoni mwa wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Moi.

Katika sura ya nne na tano matokeo ya utafiti yaliwasilishwa na kuchanganuliwa kulingana na malengo. Nadharia teule zilitumiwa katika uchanganuzi wa matokeo ya

utafiti nazo ni: Nadharia ya Umaanisho ya Paul Grice (1978, 1995) na nadharia ya Mawasiliano ya Kiutambulisho ya Giles (1972 & 1982). Kauli za tasfida na sitiari katika mawasiliano teule kati na baina ya wanafunzi kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika, ziliweza kubainishwa na kuchanganuliwa kwa misingi ya nadharia teule. Haya yalifanywa kwa minajili ya kubainisha jinsi wanafunzi huwasilisha masuala ya VVU/UKIMWI na masuala husika kwa kutumia sitiari na tasfida. Ilibainika kwamba, mawasiliano haya hutokea kwa njia ya moja kwa moja na wakati mwingi kauli hizi huwa na usimbaji wa maana ambayo huhitaji mpokeaji wa ujumbe kung'amua kusudi la mwenye kuwasilisha ujumbe huo. Hili lilifafanuliwa zaidi na nadharia ya Grice, ambayo inadokeza kwamba kuna aina mbili za maana katika usemi au kauli yoyote. Maana hizi ni maana ya lugha na maana ya msemaji. Anaendelea kueleza kwamba, maana ya lugha ni maana inayotokana na vipashio vya sentensi ilhali maana ya msemaji ni maana inayoibuka kutokana na matumizi ya maneno hayo katika sentensi.

Sura ya sita ilihusu dhima ya sitiari na tasfida kama zinavyojitokeza katika mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika. Hapa nimeeleza dhima ya sitiari na tasfida jinsi zilivyojitokeza katika utafiti. Katika sura ya saba nimetoa muhtasari, mahitimisho, mchango wa utafiti na kupendekeza mambo muhimu yanayotokana na utafiti huu na kutoa mapendekezo ya tafiti za baadaye.

## 7.2 Mahitimisho ya Utafiti

Utafiti huu umekuwa na matokeo yafuatayo ambayo yanaendana na malengo mahususi ya utafiti.

### 7.2.1 Matumizi ya sitiari katika kukuza mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika

Lengo la kwanza la utafiti lilichunguza sitiari na tasfida zinazotumika miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI. Katika utafiti huu ilibainika kuwa wanafunzi hutumia sitiari katika mawasiliano yao ya kila siku hasa wanapozungumzia masuala ya ngono na VVU/UKIMWI miongoni mwa mengine. Ilibainika kwamba, hili linatokana na hali yao ya juu ya ubunifu wa lugha, hali ya kutaka kuheshimiana miongoni mwa mengine.

Katika utafiti huu niligundua kuwa wanafunzi husika hutumia msamiati maalum kurejelea masuala nyeti kama: sitiari za kurejelea ngono, uuke, uume, kondomu, hali ya VVU/UKIMWI na mwathiriwa wa hali hii ya UKIMWI.

### 7.2.2 Nafasi ya tasfida katika kuendeleza mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi

Kwa kuangazia lengo la pili, ilibainika kwamba kipengele hiki cha lugha (tasfida) huundwa kutokana na hali mbalimbali katika jamii, vitu na vifaa vilivyo katika mazingira ya wazungumzaji husika. Utafiti huu umethibitisha kuwa mawasiliano kati na baina ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi kuhusu VVU/UKIMWI hujumuisha kauli za kitasfida katika kuwasilisha ujumbe kusudiwa kwa jamii husika.

Kauli hizo huwa na maneno ya kawaida lakini maana yake kimuktadha hueleweka kwa misingi ya nadharia za Umaanisho na Mawasiliano Kiutambulisho. Hivyo basi, kauli za kitasfida zilizoibuliwa zilitumika katika kuashiria masuala ya: kingono, uuke, uume, kondomu pamoja na mwathiriwa.

### 7.2.3 Dhima ya sitiari na tasfida katika kukuza mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi

Kulingana na matokeo ya utafiti, ilibainika kuwa, kila kauli ya kisitiari au ya kitasfida inayotolewa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI na masuala husika hulenga kutekeleza jukumu mahsusi katika jamii. Hii ni baada ya maana iliyokusudiwa kuweza kubainishwa kupitia kwa mihimili mahususi ya nadharia teule katika uchunguzi. Hivyo basi, mintarafu ya lengo la tatu, ilibainika kuwa sitiari na tasfida kwa jumla zilitumiwa ili kuhifadhi uso wa msikilizaji na mzungumzaji, kukuza maadili katika jamii na kufanikisha mawasiliano bila taklifu.

Utafiti wetu vilevile ulionyesha hali za kijamii kama: tamaduni, umri, jinsia na nyanja mbalimbali huathiri uibuaji na matumizi ya vipengele hivi. Utafiti huu ulionyesha umahiri au ubunifu walio nao wanafunzi na ujuzi wa kutumia lugha pasipo na sheria. Lugha ni chombo chenye ubunifu. Hali hii humwezesha binadamu, kwa mfano, kuunda kauli chungu nzima kutokana na idadi ndogo ya vitamkwa vinavyopatikana katika lugha. Vilevile kutokana na maneno machache watu wanaweza kuunda sentensi zisizo na idadi kamili. Sifa hii ya lugha huchangia kuipa lugha uhai, jambo ambalo huifanya lugha kuwa chombo ambacho kinajitosheleza katika mawasiliano ya jamii. Aidha, ubunifu husaidia lugha kuendelea kupanuka kila uchao kwa kupokea na kuingiza kauli mpya katika lugha husika.

Uchanganuzi wa matokeo uliongozwa na nadharia ya Umaanisho. Nadharia hii ilikuwa ya umuhimu sana, kwa sababu pragmatiki hulenga maana kulingana na msemaji. Aidha umaanisho hushughulikia maana inayojitokeza kutokana na maneno ya msemaji. Grice (keshatajwa) anasema kuwa msemaji husema au hutoa maana

ambayo haijitokezi katika vipashio vya kisarufi katika semi mbalimbali lakini hupata maana kutokana na muktadha tumizi.

## 7.3 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu unaohusu matumizi ya sitiari na tasfida ni tunu katika mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu na unatoa mchango mkubwa sana katika taaluma ya mawasiliano na ukuruba unaowahusu wanajamii. Kwa mfano, katika utafiti wetu, imebainika kuwa matumizi ya sitairi na tasfida ni muhimu sana katika kuhifadhi siri, kupunguza makali katika mawasiliano na pia kurahisisha mawasiliano miongoni mwa wahusika kwa kiwango fulani kuhusu VVU/UKIMWI na masuala husika.

Vilevile, utafiti huu utachangia umuktadhishwaji wa tamathali hizi mbili, yaani tasfida na sitiari katika matumizi ya lugha katika maingiliano halisi. Aghalabu muktadha hudhibiti uteuzi wa msamiati faafu katika mawasiliano fulani.

Aidha, utafiti huu unachangia taaluma ya diskosi hasa kwa kurejelea matumizi ya lugha katika hali halisi ya maingiliano hususan, maingiliano baina ya wanafunzi wanapowasiliana kuhusu VVU/UKIMWI.

## 7.4 Mapendekezo ya Utafiti

Kutokana na matokeo ya data tuliyokusanya tumetambua kwamba, matumizi ya tasfida na sitiari ni muhimu sana katika kila jamii, kwa sababu kila jamii inatia juhudi za kuimarisha na kuyaendeleza maadili. Maadili ni muhimu katika jamii kwa sababu yanahifadhi na kulinda jamii finyu na jamii pana.

Suala la matumizi ya lugha kuhusu VVU/UKIMWI ni suala pana, hivyo basi, kuna haja ya kuendeleza utafiti zaidi ili kutambua tamathali za usemi kama vile tashhisi, mafumbo na semi ili kubainisha matumizi na athari zake katika ugonjwa huu.

Kutokana na utafiti wetu ilibainika kwamba, matumizi ya tasfida na sitiari katika mazungumzo hulenga kurahisisha mawasiliano, kuwasiliana kwa njia mwafaka, kuhifadhi uso wa msikilizaji na kuwasiliana kwa upole. Ni kwa sababu hii ambapo tunapendekeza zaidi kila sera inayotagusana na binadamu kutilia mkazo mafunzo ya tasfida na sitiari. Sera kama za elimu, za matibabu, makanisa na mashirika ya kibinafsi, kuzingatia mafunzo ya tasfida na sitiari kutapunguza vifo, unyanyapaa, vita na chukizo inayoletwa na kutofautiana kwa mazungumzo na lugha isiyo na upole. Vilevile kuna haja ya utafiti kuhusu mabadiliko katika lugha kutekelezwa katika isimu jamii nchini Kenya.

Aidha, tunapendekeza watafiti wa baadaye wakusanye data zaidi kutoka taaluma na miktadha mbalmbali na waichambue kwa kutumia misingi mingine ya kinadharia kuhusu masuala yaliyojadiliwa hapa.

## 7.5 Hitimisho

Sura hii imetoa muhtasari wa utafiti, mchango wa utafiti pamoja na mapendekezo ambayo mtafiti mwingine anayenuia kufanya utafiti wa aina hii anaweza kufaidika nayo.

**MAREJELEO**

Allan, K., & Burridge, K. (1991). *Euphemism and dysphemism.* New York: Oxford University Press.

Allan, K., & Burridge, K. (2006). *Forbidden Words. Taboo and the Censoring of Language.* Cambridge: Cambridge University Press.

Blommaert, J. (2005). *Discourse: A critical introduction.* Cambridge: Cambridge University Press.

Bloomfield, L. (1976). *Language.* (13th Impression). London: George Allen and Unwin Ltd.

Brown, G., & Yule, G. (1983). *Discourse Analysis.* Cambridge: Cambridge University Press.

Brown, P., & Levinson, S. (1978). *Politeness! Some universal in language usage.* Cambridge: Cambridge University Press.

Bwanali, A.K. (2008). *"Language and HIV and AIDS*" in: Openspace-A Digest of the Open Society Initiative for Southern Africa. Vol.2 Issue 3. November 2008. pp.64-70.

Chiraghdin. S., & Mnyampala, M. (1977*). Historia ya Kiswahili.* Nairobi*:* Oxford University Press.

Fowler, B, (1971), "*The New Stylistics," Style and Structure in literature*. Blackwell: The pitman Press.

Fromkin,V., & Rodman, R. (1972, 1988). *An Introduction to language (4th. Ed).* Fort Worth: Holt, Reinhart & Winston.

Gatambuki, M. G. (2010). A cognitive linguistic analysis of gikuyu euphemisms. Unpublished. M.A thesis. Nairobi: Kenyatta University.

Gibbe, A.G.(1990). *Ufumbaji katika Ushairi wa Kiswahili*. *Jarida la Kiswahili.* Dar es Salaam: Education Service centre.

Gibbs, R.W. (1994). *Poetics of Mind: Figurative Thought, Language and Understanding.* New York: Cambridge University Press.

Giles, H. (Ed.). (1984). The dynamics of speech accommodation. *International Journal of the Sociology of Language*, 46.

Giles, H., & Coupland, N. (1991). *Language: Contexts and consequences*. Pacific Grove, CA: Brooks/Cole.

Giles, H., & Johnson, P. (1987). Ethnolinguistic identity theory: A social psychological approach to language maintenance. *International Journal of the Sociology of Language*, 68, 69–99.

Giles, H., & Powesland, P. F. (1975). *Speech styles and social evaluation*. London: Academic Press.

Giles, H., Coupland, N., & Coupland, J. (1991). *Accommodation theory: Communication, context, and consequence.* Cambridge: Cambridge University Press.

Giles, H., Mulac, A., Bradac, J. J., & Johnson, P. (1987). Speech accommodation theory: The first decade and beyond. In M. McLaughlin (Ed.), *Communication year book* (Vol. 10, pp.13–48). Beverly Hills, CA: Sage.

Giles, H., Taylor, D. M., & Bourhis, R. Y. (1973). Towards a theory of interpersonal accomodation through speech: Some Canadian data. *Language in society*, 2, 177–192.

Giles, H., Williams, A., & Coupland, N. (1990). *Communication, health and the elderly: Frameworks, agenda and a model.* London: Academic Press.

Giles, N. C., & Wiemann, J. M. (Eds.), (1983). *Communication, health and the elderly* (pp. 1–29). Manchester, England: Manchester University Press.

Grice, H. P. (1975). *Logic and Conversation.* Cambridge, MA: Harvard University Press.

Grice, H. P. (1989b*). Further notes on logic and conversation.* In *Studies in the way of words* (41-57). Cambridge, MA: Harvard University Press

Grice, H. P. (1991). *Studies in the Way of Words*. Cambridge, MA: Harvard University Press.

Halliday. M. A. K. (1978). *Language, Context, Text: Aspects of Language a Social Semiotic Perspective.* Oxford: Oxford University Press.

Halliday. M. A. K. (1978). Language as a Social Semiotic: *The social interpretation of Language and Meaning*. London: Cambridge University Press.

Harry, H. (1954). *Language in culture.* Chicago: The University of Chicago Press.

Hawkes, T. (1977). *The Structuralism and Semiotics*. London: Methuen.

Hudson, D. (1995). *Language and society.* London: Macmillan Publishers.

Hymes, D. (1964). *A language, culture and society.* New York: Harper and Row.

Jilala, H. (2008). The Artistic uses of metaphors in constructind meaning and messages in new generations songs in Tanzania. Tasnifu ya M.a., Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (haijachapishwa)

Kandagor, M. (2013). *Nafasi ya Lugha na Vyombo Vingine vya Kimawasiliano katika vita dhidi ya UKIMWI. Kioo cha Lugha.* 11: 91-104.

Kangisa, J. (2006). *Women writers' use of metaphor as gender rhetoric in discourse on HIV/AIDS and sex related issues*: The case of totanga patsva (we start a fresh) by Zimbabwe women writers. www.preacahersfiles.com

Kobia, J. M. (2008). *Metaphors on HIV/AIDS discourse among oluluyia speakers of western Kenya.* Phd thesis. Eldoret: Masinde Muliro University of Science and Technology.

Kothari, C. (2004) *Research methodology* (2nd Edition). New Delhi: New age International Limited Publishers.

Kothari, C.R. (2008) *Research methodology: Methods and Techniques. 2nd Edition.* New Delhi: New age International Limited Publishers.

Kumar, R. (2007). *Research Methodology: A Step by Step Guide for Beginners*. Australia: Pearson Education.

Lakoff, G., & Johnson, M. (1980). *Metaphors we live by*. Chicago: University of Chicago Press.

Leech, G. (1977). *Language and tact. Trier*: University of Trier.

Leech, G. (1983). *Principles of pragmatics:* London: Longman.

Leech, G. (2007). *Politeness: Journal of Politeness Research*. (3, 167-206). London: Longman.

Levine, R.A. (1973). *Culture, Behaviour and Personality*. Chicago: Aldine Publishing Company.

Levinson, S. C. (1983). *Pragmatics.* Cambridge: Cambridge University Press.

Levinson, S. C. (1983). *Conversational implicature. In Pragmatics* (97-166) Cambridge: Cambridge University Press.

Levinson, S. C. (2000). *Grice's program*. *In Presumptive meanings: The theory of generalized conversational implicature* (12-21). Cambridge, MA: The MIT Press.

Mazrui, A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi. Nairobi*: East African Publishers.

Mazrui, A.M., & Shariff, I. N. (1994). *The Swahili: Idiom and Identity of an African People*. Trenton & Newjersey:. Nairobi: Africa World Press.

Mesthrie, R. (ed) (2002). *Coincise Encyclopedia of Sociolinguistics*. Amsterdam: Longman.

Mohamed, K. S. (1983). *Historia ya maendeleo ya Kiswahili Zanzibar*. Lugha ya Kiswahili Toleo Jipya. Dar es salaam: TUKI.

Momanyi, C. (2004). Urban disparities in HIV/AIDS infection. *The bugged towns of Kenya*. Pp 102-105.

Moto, F. (2004). Towards a study of the lexicon of sex and HIV/AIDS. *In Nordic Journal of African studies* 13.3 (2004): 342 – 362

Mowadza, A. (2004). *Stigma and HIV/AIDS discourse in Zimbabwe* , 11(2) 420 – 439.

Mugenda, O. (2003). *Research Methods, Quantitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.

Mutiso, K. (2005). *The nature of forbidden language*. A paper presented at the symposium organized by the university of Nairobi.

Mwangi, P. (2003). *A description of non cooperatives in legal English in Kenya based on Grice's principle of cooperation.* Unpublished M.A Thesis, University of Nairobi.

Njeri, S. (2007). *A pragmatic analysis of gikuyu lexical euphemisms in HIV/AIDS discourse.* Unpublished M.A thesis, University of Nairobi.

Nyandiba, C. (2013). *Uchanganuzi wa mikakati ya kiisimu ya mawasiliano katika diskosi za VVU/UKIMWI miongoni mwa Abagusii.* Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu Cha Moi.

Ogechi, N. O. (2005). The language of sex and HIV/AIDS among University Students in Kenya. *Stichproben – Vienna Journal of African Studies 9, 123-149.*

Ortony, A. (1993). *Metaphor and Thought*. Cambridge: Cambridge University Press.

Oso, W. Y., & Onen, D. (2005). *Writing Research Proposal and Report*: *A Handbook for beginning researchers.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Price, L. (2002). *Critical Discourse analysis*. London: Sage Publishers.

Parker, R., & Aggleton, P. (2003*). HIV and AIDS-related stigma and discrimination: A conceptual framework and implications for action*.

Rawson, H. (1981). *A Dictionary of Euphemisms and other Double Talk*. New York: Crown Publishers.

Rawson, H. (1998). "Euphemisms." In G. Gashgarian (8th Ed.), Exploring of Language. USA: Addisson-Wesle Educational Publishers Inc.

Richards, S. (1965). *Semantics.* New York: MacGraw Hill Book Company.

Roberts, B. (1970). *Semantics and Language Analysis.* New York: Bobbs Merrill Company Library USA.

Robinson, P. (1972). "*AIDS and Its .Metaphors*." The new York Times.

Skinner, D. (2004). Stigma, discrimination and implication for people living with HIV/AIDS in South Africa. *In Journal of the Social Aspects of HIV/AIDS.*

Sontag, S. (1989). *AIDS and Its Metaphors.* Strauss and Giroux: New York.

Stockwell, P. (2008). *Sociolinguistics. A resource book for students*. London: Routledge.

Susan, S. (1989). *Illness as metaphor. Aids and it metaphors.* Farrar: Strauss and Giroux.

Trudgill, P. (2000). *Sociolinguistics: An introduction to language and society (4th ed.*) London: Penguin books.

Trudgill P. (2002). *Socialinguistics: An Introduction to Language and Society (5th ed.*) London: Penguin books.

Turner, M. & Richards J. (2006). *The Literary Mind*. Oxford: O.U.P.

TUKI. (1990). *Kamusi sanifu ya isimu na lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

TUKI. (2006). *English swahili dictionary* (3rd edition). Dar es Salaam: TUKI.

Ullman, S. (1962). *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. Oxford: Basil Blackwell.

Ullman, S. (1970). *Semantics and Language Analysis*. New York: Bobbs Merrill Company Library.

UNAIDS (2020). Report on the global AIDS epidemic. Nations Children's Fund, Joint United Nations Programme on HIV/AIDS and World Heaalth Organization.

UNAIDS (2008). Young People and HIV/AIDS, Opportunity in Crisis. United Nations Children's Fund, Joint United Nations Programme on HIV/AIDS and World Heaalth Organization.

USAID (2009). The language of multiple concurrent partners, sex, and HIV/AIDS in Lesotho: Opportunities for Dialogue promotion: The C-change website.

Usami, M. (2006). *Discourse on politeness and cross-cultural pragmatics*. *Readings in Second Language Pedagogy and Second Language Acquisition. In Japanese Context*, 19-41.

Van Dijk, T. A. (1997). *Discourse as social Science* (Vol. 2). SAGE Publication Ltd.

Visser, M., Hsu, C. Y., & Kalinskaya, S. (2003). *The story behind the headlines: HIV/AIDS in a leading South African newspaper.* Retrieved February, *3*, 2006.

Wafula, R.M and Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta foundation.

Walpole, R. H. (1991). *Semantics: The nature of words and their meanings*. New York: W.W. Norton and Company.

Wambua, R. S. (2009). *Variation in dialectical use of and attitudes toward taboo words and euphemism in kikamba*. Unpublished M.A project. Nairobi: University of Nairobi.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K.W. (2003*). Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publishers.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus publication Ltd.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi. Msingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*: Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Wamitila, K. W. (2013). *"Mikakati ya Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili*". Nairobi: Vide Muwa Publishers Ltd, Kenya.

Wardhaugh, R. (1999). *Proper English: Myths and Misunderstanding about Language.* Oxford: Blackwell Publishers.

Wardhaugh, R. (2002). A*n introduction to sociolinguistics* (4th ed). Oxford: Blackwell Publishers.

Whalley, G. (1953). *Poetic Process*. London: Routledge & Kegan Paul.

Whiteley, W. (1969). *Swahili the rise of a national language.* London*:* Methuen and co. Ltd.

Whiteley, W. (1974). *Language in Kenya.* Nairobi: Oxford University Press.

WHO (2008). *The global programme on AIDS, Social and Behavioural Research*.www.unaids.org

Wodak, R. (1995). *Critical Linguistics and Critical Discourse Analysis. In Verschueren. Handbook of Pragmatics* (204-210). Amsterdam: John Benjamins.

Wodak, R. (2006). *New Directions in Critical Discourse Analysis*. Amsterdam: John Benjamins.

# VIAMBATISHO

**Kiambatisho A: Kiambatisho cha mwongozo wa mahojiano na watafitiwa**

1.Taarifa binafsi

Jinsia………………………………………………………………………………

Umri…………………………………………………………………………………

Mwaka wa masomo.......………………………………………………………………

2. Umewahi kushiriki katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI?

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

a. Ikiwa ndio, ni lugha ya aina gani iliyotumika, toa mifano.

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

b. Ikiwa la, je ungeshiriki ungetumia lugha ya aina gani?

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………….............

c. Eleza kwa kutoa mifano.

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

3.Orodhesha tasfida zinazotumiwa na wanafunzi katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI…………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

4.Orodhesha sitiari zinazotumiwa na wanafunzi katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

5. Eleza  msimamo wa utamaduni wako kuhusu mawasiliano ya VVU/UKIMWI

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

**Kiambatisho B: Baadhi ya Data**

**1. Uuke**

i) Migingo
ii) Sufuria
iii) Shamba
iv) Maua ya Maulana
v) Chakula
vi) Kwenda bafuni
vii) Kuuma na kutafuna
viii) Kufanya mapenzi
ix) Kusulihisha mgogoro wa ardhi
x) Kuja pamoja
xi) Mkutano
xii) Kuja nyumbani
xiii) Kula nyumbani
xiv) Kufumbua fumbo
xv) Kucheza mechi
xvi) Kunywa maji yako

2**. Ngono**

i)Mkutano
i) Lima
ii) Kuuma
iii) Tafuna
iv) Mombasa
v) Bao
vi) Mpigo
vii) Sarakasi

3.**Uume**

i) Msumeno
ii) Kipofu
iii) Mtaimbo
iv) Mkuki
v)Nyundo
vi)Silaha

4. **VVU/UKIMWI**

i. Ugonjwa wa kigeni
ii. Mdudu
iii. Ukedi
iv. Kutokuwa sawa
v. Waya
vi. Ngoma

5. **Kondomu**
   i. Mpira
   ii. Ala
   iii. Uo
   iv. Kinga
   v. Kifuniko

**6. Sitiari zinazowakilisha wale ambao wameathirika**
   i. Foksi/paka mapepe
   ii. Teksi bubu
   iii. Chokoraa
   iv. Mama/dada huruma